# MUUNDO WA KIMAANDIKO

# WA

# MAKANISA YA KRISTO

**Na**
**JIM MASSEY**

**Kimechapishwa na**
**World Evangelism Team**

Nakala kwa lugha ya Kiswahili
Swahili Gospel Team
2024-2025

Mhariri
Shadrack S. Msambaza

Mawasiliano
+255 (0) 764 792 979
+255 (0) 765 098 981

# DIBAJI

Karibu katika somo linalohusu Mpangilio wa Kimaandiko wa Makanisa ya Kristo. Hili ni somo muhimu. Biblia inamafundisho ya kutosha katika somo hili. Kila somo lina sehemu [nakala ya Kiingereza inahusisha sehemu ya maswali pia ambayo humu imeondolewa]: (1) Muhtasari wa somo (haya ni maelezo mafupi), na (2) Mjadala wa somo.

Walimu wanapaswa kutumia mbinu ya "uchorongaji" kufundisha. Kila mada katika muhtasari inapaswa kufafanuliwa moja baada ya nyingine. Hili litawezekana ikiwa sehemu ya mjadala wa somo itakuwa imesomwa na kueleweka vizuri kabla ya darasa. Kisha baada ya muhtasara kuwa umejadiliwa vizuri, mada ya muhtasari zinapaswa "kuchorongwa" au kurudiwa mara nyingi na darasa zima au na washirika katika darasa. Mazoezi mazuri katika muhtasari kutasababisha somo hilo kukumbukwa.

Wanafunzi wanapaswa kutumia Biblia zao kusoma na kuelewa kila mstari ulioorodheshwa. Kumbuka kwamba Biblia ndiyo mamlaka pekee katika makanisa ya Kristo. Kitabu hiki cha mafunzo kinaweza kuwa si sahihi, lakini Neno la Mungu ni kweli sikuzote. Kitabu hiki ni cha kukuongoza tu kwenye mafundisho ya Biblia kuhusu mada ya uongozi kanisa.

Kitabu hiki kinaweza kutumika kwa darasa au kwa masomo ya binafsi. Ni kwa ajili ya washirika na wasio washirika. Na wote wanaotumia mafundisho hayo wafanye hivyo kwa kumuomba Mungu ili wapate hekima. Yesu alisema, ***"Mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru"*** (Yohana 8:32).

**Mwandishi**

# UTANGULIZI

Nimemjua Jim Massey kwa miaka mingi. Ama kwa hakika, alikuwa mwalimu wangu wa Kigiriki niliposoma Chuo cha Kikristo cha Alabama huko Montgomery, Alabama, Marekani. Tangu wakati huo, amejidhihirisha kama mmisionari huko Nigeria na Trinidad. Akiwa njiani alifundisha pia katika Lubbock Christian College na Sunset School of Preaching, Lubbock, Texas, U.S.A., na kwa sasa anafundisha katika Chuo cha Kimataifa cha Biblia cha Florence, Alabama, Marekani.

Akiwa amefanya kazi katika nyanja mbalimbali za misheni, na kukabiliwa na ukosefu wa vitabu vya masomo mengi ya kufundisha ambayo yalihitajika sana, basi alijibu kwa kuandika kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, nyenzo zake zimepata njia ya kwenda sehemu nyingi za ulimwengu ambapo hutumiwa kwa mafanikio makubwa. Tunatoa shukrani zetu kwake kwa kufanya kazi hii ipatikane kwetu na tunaituma kwako tukiwa na uhakika kwamba itafanya mambo mengi mazuri.

Kwa kuwa kanisa bado ni changa Afrika Mashariki, na bado liko katika mchakato wa kukua na kuwa komavu kiroho, basi kitabu hiki kinaweza kufanya mema mengi kwani kinawahimiza ndugu kufuata kwa karibu Maandiko kuhusu kanisa. Msisitizo hauko kwenye mfumo fulani wa kutengenezwa na mwanadamu, bali kwa ule utokao kwa Bwana. Ili kuwa kanisa la Kristo basi ni lazima tufuate utaratibu wa kimaandiko. Wakati huo huo, kitabu hiki kitakuwa kizuri kwa marafiki zetu wa kidini ili waweze kuona mpangilio wa kimaandiko wa kanisa, pia kitawasaidia kuona jinsi shirika lao la kanisa lilivyo geni kwa yale ambayo Biblia inafundisha. Mara tu mtu anapoona tofauti hiyo, basi hakika angependelea njia ya Bwana kuliko njia ya mwanadamu.

Nakutia moyo usome na kujifunza sura za kitabu hiki ukiwa na Biblia. Kwa kweli, mwandishi amejaribu kukuelekeza katika neno la Mungu ili kukuwezesha kuona kwamba hiki ndicho kinachofundishwa kuhusu somo husika.

Kwa hiyo ninafuraha kukipendekeza kitabu hiki kwako na ni maombi yangu kiweze kutumika sana. Ikiwa ndivyo, hakika kitathibitika kuwa na matunda.

J. C. Choate
New Delhi
Feb. 29, 1980

# UTANGULIZI WA AWAMU YA PILI

Kitabu hiki ni kinafaa kwa kazi ya utumishi. Kinagusa kila Nyanja ya muundo wa kanisa na kujibu kila aina ya maswali ambayo yanahusiana na mada hii. Kinaonyesha kile Mungu anachohitaji kwa watu wake katika jukumu la kutoa uongozi kwa kanisa. Sioni jinsi ambavyo mtu anaweza kupitia nyenzo hii, pamoja na Maandiko ya Agano Jipya, bila kuja na dhana ya kimaandiko ya kanisa la Bwana.

Kwa sababu ya uhitaji wa elimu ya namna hii katika maeneo mengi, kwa kupitia ruhusa ya Massey, tunachapisha kitabu hiki hapa. Kisha tunafanya kipatikane kwa watu wote kila mahali, hata kutuma nakala nyingi katika maeneo ya umisheni duniani bure. Tunatumaini kwamba hii itakuwa ni njia ya kuwasaidia watu wengi waaminifu kujifunza mapenzi ya Mungu kuhusu kanisa.

Tunakualika usome na kujifunza masomo haya na kisha utusaidie kufikisha ujumbe wa kitabu hiki kwa watu wengi kadiri iwezekanavyo.

J. C. Choate
Winona, MS
January, 1985

# YALIYOMO


MAMLAKA YETU NI IPI KATIKA MFUMO WA UTAWALA WA KANISA? ........ 1

KWA NINI TUNAPASWA KUJIFUNZA MUUNDO WA KANISA? .......... 4

UKWELI WA MWANZO KUHUSU MUUNDO WA KANISA .................. 6

KANISA NI NINI?........ 8

KANISA NI KITU GANI?........ 11

JE! KANISA LOTE........ 13

LINA MUUNDO GANI? ........ 13

MUUNDO WA KANISA HAPA ........ 15

DUNIANI UKOJE?........ 15

MPANGILIO WA KUSANYIKO LA MAHALI PAMOJA UMEPANGILIWAJE? ........ 20

NI KWA NAMNA GANI MAKANISA YA MAHALI PAMOJA YANAJITEGEMEA? ........ 23

KWA NINI MUNGU ANATAKA MAKUSANYIKO YAJITEGEMEE?.... 26

KANISA LINALINGANA VIPI NA SERIKALI ZA KIRAIA?.................. 28

NI KWA NINI WANADAMU........ 30

HUWAFUATA VIONGOZI? ........ 30

KWA NINI MFANO NI MUHIMU KATIKA KANISA? ........ 33

NI NANI AMBAO NI MIFANO........ 35

KATIKA KANISA? ........ 35

KUNA NAFASI ZIPI ZA KAZI ........ 38

KATIKA KANISA? ........ 38

MAJINA YA WAZEE NI YAPI? .................................................................. 41
NAMNA GANI MARA NYINGI WAZEE WANAKOSEWA KUFAHAMIKA? .................................................................. 44
JINSI MADHEHEBU YANAVYOHARIBU UONGOZI WA KANISA ..... 47
JINSI MAKANISA YA KRISTO YANAVYOWEZA KUHARIBU UTALAWA WA KANISA .................................................................. 50
NI AINA GANI YA MAKUSANYIKO YANAYOJIANDAA NA UONGOZI? .................................................................. 53
SIFA ZA WAZEE (I) .................................................................. 56
SIFA ZA WAZEE (II) .................................................................. 59
SIFA ZA WAZEE (III) .................................................................. 62
SIFA ZA WAZEE (IV) .................................................................. 66
SIFA NA KAZI ZA MASHEMASI .................................................................. 69
NJIA AMBAZO HAZIFAI .................................................................. 72
KUCHAGUA VIONGOZI .................................................................. 72
JINSI ROHO MTAKATIFU ANAVYOWEKA WAZEE ............................ 75
MAAGIZO YA MUNGU KWA WAZEE .................................................. 79
DALILI ZA HATARI KATIKA MUUNDO WA KANISA ......................... 83
JINSI UTAWALA WA KANISA ULIVYOHARIBIWA MWANZONI ...... 86
NAMNA YA KUENDESHA KIKAO .................................................. 89

## SOMO LA 1

# MAMLAKA YETU NI IPI KATIKA MFUMO WA UTAWALA WA KANISA?

MUHTASARI

1. *Sio kile kinachoonekana bora.*
2. *Sio kile wanachofanya wengine.*
3. *Bali Agano Jipya peke yake.*

### MJADALA

***1. Sio Kile Kinacoonekana Bora.*** Kusoma kokote lazima kuwe na mamlaka maalum. Maswali yoyote lazima yawe na chanzo cha majibu kinachoaminika. Lazima kuwe na mamlaka maalum, ambayo wote wanaweza kuitegemea ili kuwa sahihi. Kwa kuwa somo letu ni somo la dini, tunauliza, mamlaka yetu ni ipi tunaposoma kuhusu muundo wa Kanisa? Ni kipimio gani kitakachotumika ili kuwa na uhakika kwamba maswali yatapewa majibu sahihi? Baadhi watasema kwamba kila mtu ameachwa achague kile ambacho atafikiri ni sahihi katika dini. "Wewe fanya tu kile kinachoonekana kuwa bora," watu hao ndivyo wanavyosema. "Kila mtu ni kipimio chake mwenyewe. "Fuata mpango wowote unaofanya vizuri." Lakini maoni ya mtu sio kipimo cha Mungu katika dini. Biblia inasema, ***"….njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake; kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu"*** (Yeremia 10:23). ***"Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti."*** (Mithali 14: 12). Bwana Yesu alisema Maagizo ya wanadamu hufanya ibada isiwe na maana (Mathayo 15:9). Kwa hiyo, katika jambo lolote la kidini,

maoni ya mwanadamu sio mamlaka. Katika muundo wa Kanisa watu wengi watasema kwamba mipango yao ndiyo mizuri. Wengine watadai kwamba njia zao zinafaa zaidi. Lakini maoni ya watu sio ya kutegemewa. Hatuwezi kujua ukweli kwa kuuliza ni kipi kinaonekana bora kwetu wenyewe.

***2. Sio Kile Wanachofanya Wengine.*** Imani ya pili kuhusu mamlaka ya kidini ni kwamba kile kinachofanywa na wengi lazima kitakuwa sahihi. Wale wanaoamini katika mpango fulani wa uongozi wa Kanisa wataeleza jinsi gani watu wengi wanavyofuata mpango huo, au ni kwa mda gani mpango wao umekuwa ukifanya kazi. Lakini hili ni wazo lingine lisilo sahihi la uongozi katika dini. Maoni ya watu wengi sio ya kuaminika, tena kuliko maoni ya mtu mmoja. Yesu alisema kwamba, wengi hudhani ya kuwa wako sahihi, lakini Yeye hakuwajua (Mathayo 7:22). Watu wengi wanafuata njia za uongo, bali wachache ndio hutumia njia sahihi (Mathayo 7:13, 14). Waisraeli walitaka mfalme ili wawe kama mataifa yanayowazunguka. Lakini kwa kujaribu kuwa kama wengine, walikataa mpango wa Mungu wa kutawala watu wake (1 Samweli 8:5 - 7). Kanisa sio lazima liangalie watu wanaolizunguka ili kuwa kama wao. Kanisa ni kundi lilioitwa litoke (2 Wakorinto 6: 17). Ni watu wa kipekee (1 Petro 2:9). Uharibifu mwingi unaoingia katika mfumo wa Kanisa la Bwana unaingia kwa sababu ya waumini dhaifu wanataka kuwa kama madhehebu yanayowazunguka. Wanatamani mipango na njia ambazo wengi wanafuata. Lakini vitu ambavyo wengi huvifanya sio kipimio cha Mungu cha ukweli.

***3. Agano Jipya Pekee.*** Kipimio pekee cha kweli cha mamlaka ya kidini ni Agano Jipya. Sio Katekisimu, au kitabu cha Sala, wala mafundisho mengine yoyote. Yesu ana mamlaka yote mbinguni na duniani (Mathayo 28:18). Alimpeleka Roho Mtakatifu kuwaongoza mitume wake katika kweli yote (Yohana 16:13). Hivyo, kile kilichoandikwa katika Maandiko kimevuviwa na Mungu na kinatosha kwa kila tendo jema kwa Wakristo (2 Timotheo 3:16-17). Watu

hawapaswi kuongeza wala kupunguza katika kitabu cha Mungu (Ufunuo 22:18, 19). Wote lazima wakae katika fundisho la Kristo na sio kuyapita (2 Yohana 9, 10). Watu hawapaswi kabadili au kugeuza Injili (Wagalatia 1:7-9). Lazima ieleweke pia kwamba Agano la Kale halina mamlaka kwa Wakristo. Lilikuwa ni kiongozi tu kutuleta katika imani katika Kristo, lakini sasa watu hawako chini ya kiongozi tena (Wagalatia 3:24,25). Sheria iliondolewa isiwepo tena na kugongomelewa msalabani (Wakolosai 2:14). Wakristo wako chini ya Agano Jipya na bora, Agano jipya la Bwana wetu Yesu Kristo (Waebrania 8: 6-13). Kwa hiyo, sheria za Agano la Kale, za sikukuu ya mavuno, na nyingine hazipaswi kutumika kuruhusu vitu hivi ndani ya Kanisa kwa siku hizi.

Somo hili la utawala wa Kanisa, litaheshimu Agano Jipya, kama mamlaka pekee iliyovuviwa kutoka kwa Mungu. Vitu vilivyandikwa katika masomo haya lazima vihakikishwe katika Biblia kama ndivyo ilivyo (Matendo 17: 11). Mthibitishe kila mwalimu na kila fundisho kwa kutumia mamlaka ya Neno la Mungu (1 Yohana 4:1). Leo hatuoni mamlaka ya Mungu katika wanadamu, bali katika Maandiko. Kile tu ambacho kimethibitishwa kutoka katika kitabu cha Mungu, kimethibitishwa na Mungu. Lazima tuishindanie imani, iliyotolewa mara moja tu katika Biblia (Yuda 3). Lazima tuseme kama ***"mausia ya Mungu yanavyosema"*** (1 Petro 4:11). Mungu si Mungu wa machafuko bali wa amani (1 Wakorintho 14:33). Wale wanaoheshimu mamlaka ya Mungu, watafundisha kile ambacho Bibia inafundisha na kukataa kufundisha kingine chochote kisichoruhusiwa katika Maandiko. Watu wa Mungu lazima waseme pale ambapo Biblia inasema, na wanyamaze pale ambapo imenyamaza. Lazima wafanye mambo ya kibiblia kwa njia ya kibiblia. Na kuita majina vitu vya kibiblia kwa majina ya kibiblia. Wakiliheshimu Neno la Mungu kama mamlaka pekee katika dini, Unaombwa kusoma masomo yafuatayo kuhusu Muundo wa Kanisa.

Chunguza kila andiko kutoka katika Biblia yako. Ni neno la Mungu ni neno la kweli (2 Timotheo 2: 15).

## SOMO LA 2

# KWA NINI TUNAPASWA KUJIFUNZA MUUNDO WA KANISA?

MUHTASARI

1. *Kuondoka katika imani tangu awali, kulikuwa ndani ya Muundo.*
2. *Kiburi cha kibinadamu kinaharibu uongozi kwa urahisi.*
3. *Makusanyiko mara nyingi huwa yanakuwa ama mazuri, au mabaya kama viongozi wake walivyo.*

## MJADALA

***1. Kuondoka katika imani tangu awali,*** *kulikuwa ndani ya Muundo.* Biblia ilitabiri watu kupotelea mbali na imani (1 Timotheo 4: 1). Baadhi watabadilisha na kugeuza Injili ya kweli (Wagalatia 1:6-9). Mtume Paulo aliwaonya Wazee wa kanisa kutoka Efeso kwamba waliangalie kundi ambalo kwalo wao ni waangalizi (Matendo 20:28).

Tunajifunza kutoka katika historia ya kanisa, kwamba katika miaka michache tu unabii huu ulitimilika. Watu walianza kuacha imani. Walimu wa uongo walianza kuwapotosha wafuasi. Viongozi wa kanisa walianza kuongoza kwa njia ambazo Mungu hakuzikusudia. Walianzisha aina ya uongozi au mfumo ambao unapatikana katika kanisa Katoliki na madhehebu mengine. Ulikuwa ni uongozi wa kanisa ambao uliharibiwa kwanza.

Moja ya njia za kwanza ambazo watu waliacha Biblia, ilikuwa ni katika mambo ya muundo wa kanisa. Wazee walianza kutawala zaidi ya kanisa moja. Halafu maaskofu wakawatawala wazee wengine. Watu wakaendelea kubadili mpango wa Biblia kuhusu uongozi wa kanisa, mpaka hatimaye papa akachaguliwa. Hakuna Papa katika Biblia, lakini watu wametoka katika imani.

Mara zote huwa kuna hatari kwamba watu wataharibu mfumo wa kweli wa kanisa. Inapotokea watu kuacha Maandiko, mara nyingi inaanzia katika uongozi. Ndiyo maana kujifunza mfumo wa uongozi wa kanisa ni muhimu sana. Kwa kuelewa wengine walivyoacha ukweli, tutaweza kuepuka makosa yao.

***2. Kiburi cha kibinadamu kinaharibu uongozi kwa urahisi***. Kiburi kwa hapa ni kule kutaka kujitukuza. Ni majaribu makubwa kwa kiongozi yeyoye. Mtu fulani anapokuwa na madaraka, anataka madaraka makubwa zaidi. Kiongozi anapokuwa na mamlaka fulani, anataka mamlaka zaidi. Hii ndiyo sababu uongozi ndani ya kanisa umeharibika.

Watu ni walewale katika vizazi vyote. Kiburi ni hatari sana kwa kila mtu. Mama yao mitume Yakobo na Yohana alitaka watoto wake wakae katika pande zote za Yesu katika ufalme wake (Mathayo 20:20-28). Mitume walikuwa kama watu wa leo, wote wanapenda mamlaka. Tunahitaji nafasi za umaarufu. Asili ya binadamu haitabadilika

Hii ndiyo maana hatari ya kuharibu mpango wa Mungu wa uongozi wa kanisa, ni hatari iliyopo sasa. Watu wataingia kanisani mara kadhaa, kwa matumaini ya kuwa viongozi. Wengine watakuwa waumini ikiwa tu wameahidiwa nafasi za uongozi. Watu mara nyingi hawaridhishwi na kuwa mtumishi mnyenyekevu ndani ya kanisa. Badala yake wengi watatafuta mamlaka makubwa wanayoweza kuyafikia. Wataharibu mpango wa Mungu ilimradi tu wawe na nafasi kubwa kwa ajili yao. Kiburi cha binadamu kinaharibu uongozi wa kanisa. Kwa hiyo, mafunzo haya ni ya muhimu.

***3. Makusanyiko mara nyingi huwa yanakuwa ama mazuri, au mabaya kama viongozi wake walivyo.*** Mtume Paulo aligundua hili pale alipowaita wazee kutoka Efeso ili aongee nao (Matendo 20:17-30). Alijua kwamba makanisa mengi hufuata viongozi wema na kuwa makanisa imara au kufuata viongozi dhaifu au wabaya na kuwa makanisa mabaya. Hii ndiyo sababu mpango wa Roho Mtakatifu ni kuwa na wazee wazuri au waangalizi wazuri katika kila kusanyiko (Matendo 20:28). Uongozi imara unapelekea kuwa na kanisa imara.

Lakini uongozi mzuri hauji bila jitihada kubwa. Ni matokeo ya kufundisha sana na kutenda. Viongozi wa watu wa Mungu, lazima wawe wamejitayarisha vizuri na wamefundishwa vizuri. Kazi yao ni kazi muhimu sana hapa duniani.

Paulo alimuelekeza Timotheo ayakabidhi mambo aliyojifunza kwa watu waaminifu, watakaofaa kuwafundisha wengine pia (2 Timtheo 2:2). Kuwafundisha watu ambao nao watawafundisha na wengine, katika mpango wa Mungu wa uongozi. Kwa sababu hizi, mafunnzo haya juu ya jinnsi Biblia inavyofundisha kuhusu muundo wa kanisa ni ya muhimu.

**SOMO LA 3**

# UKWELI WA MWANZO KUHUSU MUUNDO WA KANISA

**MUHTASARI**

1. *Kila taasisi lazima iwe na viongozi.*
2. *Kila taasisi lazima iwe na wafuasi.*
3. *Na kila kundi lazima litoe ushirikiano kwa kundi lingine*

## MJADALA

***1. Kila taasisi lazima iwe na viongozi.*** Yesu mara kadhaa aliwahurumia makutano waliomfuata kwa sababu walikuwa ni kondoo wasiokuwa na mchungaji (Mathayo 9:36). Na hata makundi ya wanyama kama kondoo lazima wawe na viongozi. Ndivyo ilivyo hata katika makundi ya binadamu. Mungu aliona kuwa familia ilihitaji kiongozi hivyo, akamfanya mume kuwa kichwa (Waefeso 5:23). Mataifa lazima yawe na watawala, na Mungu ameweka kuwe na wafalme na maliwali (1 Petro 2:13, 14). Kundi la vibarua hufanya kazi nzuri sana kama wana viongozi wazuri. Mambo haya yanatuonyesha kwamba, mpango wa taasisi lazima iwe na viongozi.

***2. Kila taasisi lazima iwe na wafuasi***. Yesu alisema kwamba mji au nyumba yoyote ikifitinika juu ya nafsi yake haitasimama (Mathayo 12:25). Hata kama kuna viongozi wazuri, kila kundi lazima liwe na wafuasi pia. ***Kufuata*** ni muhimu pia kama ilivyo kwenye ***kuongoza.*** Wakati fulani watu hawaangalii wafuasi kuwa ni wenye umuhimu. Lakini viongozi ni wazuri kwenye nini kama hakuna wa kuwaongoza? Wafuasi wanahitaji kufundishwa jinsi ya kufuata. Mungu anawategemea wafuasi wawe wafuasi wema. Lazima wafundishwe namna ya kufuata.

***3. Kila kundi lazima litoe ushirikiano kwa kundi lingine***. Viongozi wazuri na wafuasi wazuri wanajua namna ya kufanya kazi pamoja na kwa uzuri. Viongozi lazima wajue wajibu wao vizuri na wafuasi nao wajue kazi zao. Kila mmoja aelewe ni kipi anawajibika kukifanya na kipi hapaswi kukifanya. Viongozi lazima watambue nafasi ya wafuasi, na wafuasi lazima waheshimu kazi za viongozi. Hii italeta mahusiano mema miongoni mwao wote.

Biblia inafananisha taasisi ya kanisa na mwili wa binadamu. Mwili una viungo vingi, na kila kiungo kina kazi kwenye mwili (1 Wakorintho 12:12). Mguu usijisikie kwamba sio muhimu kwa kuwa sio

mkono (mst. 15). Wala jicho lisiuambie mkono kwamba sikuhitaji. Hata vile viungo vidogo kabisa vina kazi na vina umuhimu katika mwili (mist. 20-26). Mambo haya ni ya kweli kama ilivyo kwenye mwili wa kiroho wa Kristo, yaani kanisa (mst. 27).

Lazima kusiwepo na kuoneana wivu baina ya viongozi na wafuasi, lazima viongozi wawajali wafuasi. Wote wafanye kazi pamoja kwa kufanya vizuri majukumu yao ambayo kila mmoja ana uwezo nayo. Kijitabu hiki kitakuwa ni kitabu cha; kuongoza, kufuata na kushirikiana pamoja.

## SOMO LA 4

# KANISA NI NINI?

MUHTASARI

1. *Kanisa la Jangwani.*
2. *Kanisa au Mwili wa Kristo.*
3. *Kanisa la sehemu.*
4. *Kusanyiko.*

### MJADALA

***1. Kanisa la Jangwani.*** Neno "kanisa" lina maana ya "kundi la watu walioitwa watoke" na halimaanishi jengo. Sauli wa Tarso alilitesa kanisa kwa kuwatesa "wanaume na wanawake" (Matendo 8:1-3). Wafuasi wa kanisa ndio kanisa. Lakini sio wanaume wote na wanawake wote ni kanisa, ila wale tu ambao ni "watu walioitwa watoke." Biblia inapotumia neno "kanisa" mara zote inaongelea "kundi la watu walioitwa." Stefano alikuwa anahubiri kuhusu Waisraeli

walioitwa kutoka Misri kwenda Jangwani. Watu hawa waliitwa watoke katika utumwa na vifungo hivyo, akawaita ***"kanisa la Jangwani"*** (Matendo 7:38). Hii inatusaidia kuona maana ya kweli ya kanisa. Naam, kundi hili huko jangwani halikuwa kanisa la Kristo la Agano Jipya. Walibatizwa wawe wa Musa kwa kuvuka Bahari ya Shamu na kufunikwa na wingu (1 Wakorinto 10:1,2). Kanisa ambalo Yesu alilijenga halikuja mpaka alipokuja duniani na kurudi Mbinguni (Mathayo 16:18). Dini ya Agano la kale ilikuwa ni dini ya Kiyahudi (Wagalatia 1:13,14). Haukuwa Ukristo bali ulikuwa ni utangulizi wa Ukristo (Wagalatia 3:24-25).

Zaidi sana kanisa ambalo Biblia inaliongelea sio madhehebu. Hapakuwepo na madhehebu nyakati za kanisa la Agano Jipya. Madhehebu yote yameanzishwa na watu nyakati fulani baada ya Yesu kujenga kanisa lake. Madhehebu ni migawanyiko iliyoanzishwa na watu kinyume cha mafundisho ya Biblia kwamba sote tuwe na umoja (Yohana 17:20-21). Migawanyiko hii ilianza kuinuka pale waamini walipoanza kuwafuata waalimu wao (na kujiita kwa majina yao) badala ya kujiita kwa jina la Kristo (1 Wakorinto 1:10-13). Kwa hiyo, katika Biblia mara zote kanisa ni kundi la watu walioitwa. Na wala si jengo wala madhehebu. Kanisa la Jangwani lilikuwa ni kundi la Agano la Kale la Wayahudi walioitwa.

***2. Kanisa au Mwili wa Kristo***. Tunapokuja katika Agano Jipya tunajifunza kuhusu kanisa la Kristo. Yesu alisema nitalijenga kanisa langu (Mathayo 16:18). Biblia inasema kwamba kanisa hili lilinunuliwa kwa damu ya Yesu (Matendo 20:28). Alilipenda na kujitoa kwa ajili yake (Waefeso 5:25). Kila mtu anayeokolewa anaongezwa na Bwana katika kanisa hili (Matendo 2:47). Linaitwa mwili wa kiroho wa Kristo, na yeye ni kichwa chake (Wakolosai 1:18, 24). Kundi hili linalojumuisha Wakristo wote, kwa kweli ni "kundi la walioitwa." Wametolewa katika mambo ya giza na kuingizwa katika ufalme wa Kristo (Wakolosai 1:13). Wamekuja kutoka katika mambo ya kidunia

na wakawa watu waliojitenga (2 Wakorinto 6:17). Kundi hili la watu walioitwa, Biblia inaliita kanisa Mwili wa Kristo.

***3. Kanisa la mahali fulani***. Namna nyingine ambayo Agano Jipya inalitumia neno “kanisa” linarejelea kundi la Wakristo wenyeji. Hili ni kusanyiko la watu walioitwa katika kijiji au mji mmoja. Tunasoma kuhusu ***“kanisa la Mungu lililoko Korintho”*** (1 Wakorintho 1:2). Tunaona kwamba yale ***“makanisa saba yaliyoka Asia”*** (Ufunuo 1:11). Paulo anatuma salamu kutoka kwa makusanyiko kama hayo anaposema, ***“makanisa ya Kristo yawasalimu”*** (Warumi 16:16). Kundi la waumini walioitwa katika eneo lolote ni kanisa la mahali hapo.

***4. Kusanyiko***. Njia ya nne ambayo Biblia inatumia neno “kanisa” ni kuongelea Kusanyiko. Watu wanapoitwa kutoka katika nyumba zao na kuingia katika mkusanyiko, pia wanaitwa “kanisa”. Kumbuka “kanisa” ni kundi la watu “walioitwa”. Paulo anaongelea kanisa linapokusanyika, katika 1 Wakorintho 14:23. Anasema wanawake na wanyamaze katika kanisa (kusanyiko). Anasema ni aibu kwa wanawake kunena katika kanisa au kusanyiko (mist. 34, 35). Kusanyiko ni kundi la Wakristo walioitwa, ambao wamekuja pamoja kukusanyika.

Hizi ni njia nne, ambazo Bibia inazitumia kufafanua neno “kanisa.” Mara zote huwa linamaanisha “kundi la watu walioitwa.” Tafadhari kumbuka matumizi haya manne ya neno kanisa tunapoendelea kujifunza kuhusu uongozi wa kanisa. Na mara zote tuongee pale tu Biblia inapoongea na tunyamaze pale ambapo imenyamaza. Tunaweza kuepuka kuchanganyana kwa kuongelea kanisa kama vile tu Biblia inavyoliongelea. Ebu tuondokane na mawazo ya makanisa ambayo hayapatikani katika Biblia.

## SOMO LA 5

# KANISA NI KITU GANI?

MUHTASARI

1. *Kila Mkristo yuko chini ya Kristo, ambaye ni kichwa.*
2. *Watu wote wako sawa chini ya Kristo.*
3. *Upendo, nia, na ushirikiano miongoni mwa wote.*

## MJADALA

***1. Kila Mkristo yuko chini ya Kristo, ambaye ni kichwa.*** Somo la mwisho limefundisha kwamba, kanisa limeundwa na kila Mkristo duniani. Kanisa lote ni mwili wa kiroho wa Kristo, likiundwa na waumini wa makusanyiko yote. Yesu ni kichwa cha mwili huu mkubwa wa waumini (Wakolosai 1:18, 24). Kristo ni kichwa pekee cha mwili wake, kama vile mwili wetu wa kibinadamu ulivyo na kichwa kimoja tu. Kila Mkristo anawajibika kwa Kristo, ambaye ni kichwa, kama viungo vyote vya mwili wa nyama, vinavyotii kichwa. Kristo Yesu amepewa mamlaka yote mbinguni na duniani (Mathayo 28:18). Anatoa maelekezo yake kwa mwili wake kupitia neno lake, yaani Biblia (Mathayo 28:19). Kila Mkristo wa kweli, katika dunia yote, anawajibika kwa Kristo ambaye ndiye kichwa, na yeye ni sehemu ya mwili wake wa kiroho, yaani Kanisa.

***2. Kila Mtu yuko sawa na mwingine katika Kristo.*** Kama viungo vya mwili wa Kristo, Wakristo wote wako sawa. Hawana kichwa isipokuwa Kristo peke yake. Hawako chini ya mamlaka yoyote isipokuwa neno lake. Hakuna Mkristo mmoja mwenye mamlaka, cheo au nafasi juu ya Mkristo mwingine katika kanisa lote. Hakuna Mkristo

au kundi la Wakristo wanaowaendesha Wakristo wengine. Wote wako sawa chini ya Kristo ambaye ni kichwa. Kuna uwezo tofauti, ambao tumepewa, lakini hakuna aliye juu ya mwingine (1 Wakorintho 12:4-6). Na kuna kazi tofauti kutegemea uwezo wa kila mmoja, lakini hakuna Mkristo aliyeinuliwa juu ya mwingine (1 Wakorintho 12:12-24). Kila Mkristo katika kanisa lote, au mwili wa Kristo yuko sawa na mwingine chini ya Kristo aliye kichwa kimoja tu.

***3. Upendo, nia, na ushirikiano miongoni mwa wote.*** Wakristo wote wapendeni Wakristo wengine kama ndugu. Wote wako katika familia ya Mungu (1 Yohana 3:1). Wakristo wote wana nia ya kuona viungo vingine vikifanya kazi vizuri. Viungo vyote hivyo ni sehemu katika mwili mmoja (1 Wakorintho 12:12-13). Watu wa rangi zote, makabila yote, wako sawa katika mwili wa Kristo, na wanawake wana thamani machoni pa Mungu kama wanaume (Wagalatia 3:26-28). Kama viungo vya mwili mmoja, Wakristo wanafurahishwa na waamini katika makusanyiko yote. Hakupaswi kuwa na aina yoyote ya mgawanyiko katika mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12:25). Viungo vyote vina uangalizi uleule kwa kila kimoja. Kama kiungo kimoja kikiugua, viungo vingine vyote vinaugua pamoja na hicho. Na kama kiungo kimoja kikiheshimiwa, viungo vingine pia vinafurahi pamoja na hicho (1 Wakorintho 12:25-26). Kiungo kimoja katika miili yetu kinapojeruhiwa, mwili mzima unahuzunika juu yake. Hali kadhalika katika mwili wa kiroho wa Kristo, sisi sote ni viungo kila mmoja kwa mwenzake. Lazima tuwe na upendo, nia njema na ushirikiano na viungo vingine katika mwili wote wa Kristo.

## SOMO LA 6

# JE! KANISA LOTE LINA MUUNDO GANI?

MUHTASARI

1. *Hakuna utawala wa kidunia wa Kanisa.*
2. *Hakuna makao makuu duniani.*
3. *Jitihada zozote za kuunganisha kanisa lote ni dhambi.*

## MJADALA

***1. Hakuna utawala wa kidunia wa kanisa.*** Kanisa lote, au mwili wa Kristo, halina utawala wa kidunia. Lina kiongozi wa Mbinguni, na mamlaka ya Mbinguni (Mathayo 28:18). Kwa njia hii limekuwa tofauti na makanisa ya kimadhehebu ambayo yana makao makuu ya kidunia na kiongozi mkuu wa kidunia kama vile Papa au askofu mkuu. Mamlaka yao ni mamlaka ya kibinadamu iliyoandikwa katika Katekisimu na au katika vitabu vya sala, vikiandikwa na mkutano mkuu. Lakini Biblia haimwiti mtu yeyote kuwa kichwa, bali Kristo pekee (Waefeso 1:21-23). Mwili wa Kristo hauna mfumo wa kidunia, ukiwa na maofisa juu ya Wakristo wote. Kanisa halina wilaya wala Sinodi, au migawanyo mingine. Waamini wake hawakutani kuamua mambo yao katika mikutano mikuu. Huu wote ni uharibifu na mabadiliko ambayo yameletwa na watu. Badala ya muungano wa kidunia na Wakristo wengine, Wakristo wote wana muungano wa kiroho miongoni mwao na pamoja na Kristo. Kila Mkristo na kila

kanisa liko huru chini ya Kristo. Lakini kanisa lote, au mwili wa Kristo halina muundo wa uongozi wa kidunia.

***2. Hakuna makao makuu duniani.*** Makao makuu ni pale anapokaa kiongozi mkuu. Kwa sababu Kristo Yesu ndiye kichwa pekee cha kanisa lake, Mbinguni ndipo makao makuu (Waebrania 12:2). Makanisa ya kimadhehebu yana makao makuu ya kidunia. Huyo mkuu anakaa hapo na anatawala sehemu zote za madhehebu hayo. Hii inaonyesha tofauti nyingine kati ya kanisa la Bwana na makanisa yaliyoanzishwa na binadamu. Hakuna uwanja mkubwa wa kanisa au uwanja wa shule ambao ni makao makuu ya kanisa. Kanisa la kwanza litakalojengwa katika uwanja huo, halitakuwa muhimu tofauti na makanisa mengine. Hakuna kulipa malipo kwa ajili ya makao makuu ya kidunia. Hakuna makao makuu yanayotuma wahubiri au kuwabadilisha au kuwahamisha vituo. Hakuna mahali ambapo waamini wote katika makanisa huja pamoja kwenye mikutano mikuu ili kuamua miongozo ya makanisa. Badala yake Mbinguni, ambapo Kristo ndiye kichwa, ni sehemu pekee kwa makanisa ya Kristo.

***3. Jitihada zozote za kuunganisha Kanisa lote ni dhambi.*** Watu na hata makusanyiko wanaweza wakajaribu kulipatia kanisa la Bwana utawala wa kimadhehebu. Kanisa kubwa linaweza kujaribu kuyatawala makanisa madogo katika eneo lake. Tamaa hii inaweza kupelekea kujaribu kuunda kanisa moja kimataifa. Kwa sababu Wakristo wengi walikuwa katika madhhebu, inakuwa vigumu kwao kusahau utawala wa kibinadamu wa madhehebu yao. Wanapenda mikutano mikubwa. Watu wanapenda kutawala makanisa mengi. Wanapenda ofisi na maofisa kama makanisa ya kimadhehebu yanayowazunguka. Lakini mambo haya yanakiuka muundo halisi wa kanisa. Yanaharibu serikali halisi ya kanisa ambayo inapatikana katika Biblia. Hatupaswi kwenda zaidi ya mafundisho ya neno la Kristo (2 Yohana 9). Tusithubutu kuibadili Injili (Gal 1:6-9). Hatupaswi

kuongeza wala kupunguza katika mpango wa Biblia (Ufunuo 22:18-19). Jaribio lolote la kuunganisha kanisa lote ni dhambi.

## SOMO LA 7

# MUUNDO WA KANISA HAPA DUNIANI UKOJE?

MUHTASARI

1. *Kanisa la mahali ndilo lenye muundo hapa duniani.*
2. *Mafundisho yote ya Biblia kuhusu muundo wa kudumu wa uongozi wa Kanisa, unahusu Kanisa la Mahali.*
3. *Hakuna maofisa hapa duniani nje ya Kanisa la mahali.*

**MJADALA**

***1. Kanisa la mahali ndilo lenye muundo hapa duniani.*** Masomo mawili yaliyopita yalionyesha kwamba kanisa halina mfumo wa uongozi wa kidunia. Kanisa la mahali, ndilo lenye uongozi wake na muundo wake. Mtume Paulo aliwaita wazee kutoka katika kanisa la Efeso (Matendo 20 :17). Alisema kwamba walichunge kundi au kanisa, ambalo kwalo Roho Mtakatifu amewaweka kuwa waangalizi (Matendo 20:28). Roho Mtakatifu huwafanya wanaume kuwa waangalizi wa kusanyiko moja la mahali fulani tu. Biblia haisemi kwamba kutakuwepo waangalizi wa kanisa lote au mwili wa Kristo. Katika 1 Petro 5:2 wazee waliambiwa walilishe kundi la Mungu lililoko kwao. Hawakuwa na wajibu kama wazee, isipokuwa kwa kusanyiko lililoko kwao ambalo kwalo walikuwa waangalizi. Maandiko haya yanaonyesha kwamba Mungu amepanga viongozi katika kila kusanyiko moja tu.

Wakati mwingine watu wanaweza kufikiri kwamba mipango yao ya kuunganisha kanisa ni mizuri. Wengi wangependa kuunganisha kanisa lote leo hii. Lakini upumbavu wa Mungu ni hekima kuliko ya binadamu (1 Wakorinto 1:25). Zipo sababu nyingi na nzuri kwa nini kanisa mahali tu ndio liwe na uongozi wake. Watu lazima waheshimu mpangilio wa Mungu na kuheshimu hekima ya Mungu na kufuata mpango wa Mungu. Kanisa mahali tu ndilo lina mfumo wa uongozi hapa duniani, lakini kanisa lote hakuna.

***2. Mafundisho yote ya Biblia kuhusu muundo wa uongozi wa Kanisa, unahusu Kanisa la Mahali tu***. Pale Maandiko yanaposema juu ya ofisi za kudumu na viongozi katika kanisa, huwa yanarejelea kanisa moja tu. Mwanzoni mwa kanisa, kabla Maandiko hayajakamilika, kulikuwa na viongozi wa muda. Katika 1 Wakorintho 12:28 Biblia inaonyesha kwamba Mungu aliweka wengine ndani ya kanisa; ***"wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu walimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa na masaidiano na maongozi na aina za lugha."*** Lakini karama za Roho Mtakatifu zilizowezesha kufanyika miujiza zilikuwa za muda. 1 Wakorintho 13:8-10 yanafundisha kwamba ufunuo kamili wa Mungu, yaani Biblia, utakapokuja, ulio kwa sehemu utakoma. Karama za miujiza zilipokoma viongozi wa kudumu wa kanisa waliendelea. Nafasi ndani ya kanisa ambazo Mungu alipanga ziendelee, hazikutegemea nguvu za miujiza. Tunaposoma sifa za wazee wa kanisa, nguvu za kufanya miujiza, haitajwi. Wanaume wanaweza kuwa wazee bila nguvu za kufanya miujiza.

Ofisi zote za kudumu ndani ya kanisa zilikuwa ni kwa ajili ya kanisa moja tu. Utume na unabii vilikuwa vya muda katika mwili wote wa Kristo vilikoma haraka. Lakini wazee waliwekwa katika kila kanisa (Matendo 14:23). Tito aliachwa Krete ili kusimika wazee katika kila mji (Tito 1:5). Aya hizi zinaonyesha kwamba wazee walikuwa ni kwa ajili ya kanisa la mahali tu na sio kwa mwili wote wa Kristo. Wazee

toka Efeso walitakiwa kulichunga kundi ambalo kwalo Roho Mtakatifu amewaweka kuwa waangalizi (Matendo 20:28). Kundi hili lilikuwa ni kanisa moja tu, la pale Efeso (Matendo 20:17). Wazee wameamriwa kuchunga kundi la Mungu lililoko kwao (1 Petro 5:2). Hawana mamlaka juu ya kanisa lote. Tunavyoendelea mbele kusoma muundo wa kudumu wa kanisa la Bwana, tutaona mafundisho kwa ajili ya mviongozi wa kanisa moja. Maandiko yote yanayoshughulika na muundo wa kudumu wa uongozi wa kanisa, unaongelea kanisa moja tu.

***3. Hakuna viongozi hapa duniani nje ya kanisa la mahali***. Yesu Kristo bado ni kiongozi wa kanisa akiwa Mbinguni. Mitume wa Bwana na manabii wanaendelea kuwa na nafasi muhimu katika kanisa kwa sababu bado tunafuata mamlaka ya Maandiko yao yaliyovuviwa. Lakini viongozi hawa walio juu ya kanisa lote wako Mbinguni. Hawana wawakilishi au warithi hapa duniani. Viongozi wote wa kanisa kwa leo wako katika kanisa husika tu. Tunalijua hili kutokana na ukimya wa Maandiko. Biblia haitoi maelekezo kabisa kwa viongozi zaidi ya wale walio katika kusanyiko hilo husika tu. Kwa kuwa Biblia inatuwezesha kutenda kila tendo jema, tunajua kwamba Mungu alimaanisha kuwa kanisa lote lisiwe na viongozi wakuu juu yaw engine wote (2 Timotheo 3:16-17). Biblia inaposema, tunasema na inaponyamaza, tunanyamaza. Lazima tukae katika mafundisho ya Kristo na sio kwenda zaidi ya kile kilichoandikwa (2 Yohana 9).

## SOMO LA 8

# JE! MITUME NA MANABII WALIKUWA WATU GANI?

MUHTASARI

1. *Walikuwa ni viongozi maalum katika uanzishwaji wa kanisa.*
2. *Nguvu yao ya kutenda miujiza ilikoma.*
3. *Walikuwa ni viongozi wa muda tu sio viongozi wa kudumu.*

### MJADALA

***1. Walikuwa ni viongozi maalum katika uanzishwaji wa kanisa.*** Vitu vyote hapa duniani vilianza kwa miujiza. Mwanadamu na hata dunia vimeanza kwa miujiza. Lakini leo mwanadamu na hata dunia vinaendelea kwa mipango ya Mungu ya asili, bila miujiza. Kwa hali kama hiyo, kanisa pia lilianza kwa miujiza. Lakini kanisa linasambaa na kuendelea kwa mipango ya Mungu bila miujiza. Neno la Mungu lililetwa kwanza kwa miujiza. Lakini sasa tunayo Biblia inayoweza kufundishwa bila kuhitajika miujiza.

Mitume walikuwa viongozi wa kutenda miujiza mwanzoni mwa kanisa. Mungu aliwapa uwezo maalum ili kuthibitisha neno lake na kutumika kuweka misingi ya kanisa lake. Yesu aliahidi kwamba mitume wangeongozwa na Roho Mtakatifu katika kweli yote (Yohana 16:13). Mitume na manabii walikuwa ni wa lazima kama sehemu ya msingi au chanzo cha kanisa (Waefeso 2:20). Biblia inasema kwamba watu kama mitume na manabii, waliwekwa na Mungu kwanza katika kanisa (1 Wakorintho 12:28). Miujiza yao ilikuwa ni ishara kwamba walikuwa ni mitume (2 Wakorintho 12:12). Miujiza yao ilithibitisha kwamba kile walichofundisha kilitoka kwa Mungu (Waebrania 2:3-4).

Ofisi hizi na viongozi hawa walikuwa ni wa lazima kwa kuanzishwa kwa kanisa. Lakini nafasi zao na miujiza yao haina ulazima kwa leo.

***2. Nguvu yao ya kutenda miujiza ilikoma.*** Tunajua kwamba hakuna mitume katika kanisa hapa duniani leo hii kwa sababu nguvu zile za kutenda miujiza zimekoma. Ilikuwa ni mpango wa Mungu, kwamba miujiza ingekoma pindi madhumuni yake yatakapokuwa yametimia. Unabii, kunena kwa lugha, na ujuzi wa miujiza vitakoma (1 Wakorintho 13:8-10). Hivi vyote vingekoma baada ya ufunuo kamili wa Mungu kuja, ambao ni Biblia. Mungu alitoa karama hizi, mpaka pale tu, ambapo imani ilipokamilishwa (Waefeso 4:8, 11-13). Sasa kwa kuwa Biblia imekamilika tunao ufahamu kamili wa Mwana wa Mungu. Imani imetolewa mara moja tu, kwa watakatifu (Yuda 3). Ukweli kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, umeshathibitishwa moja kwa moja, tena kwa miujiza (Yohana 20:30-31). Kitu kilichokwisha kuthibitishwa, hakihitaji kuthibitishwa tena. Ukweli wa neno la Mungu umeshathibitishwa. Na ukweli ukithibitishwa mara moja basi umethibitishwa moja kwa moja. Leo Maandiko yanatukamilisha kwa kila tendo jema (2 Timotheo 3: 16-17). Nguvu ile ya kutenda miujiza ya mitume imekoma kwa sababu lengo lake limeshatimizwa. Kwa kuwa nguvu ile ya mitume imekoma, basi hakuna mitume tena hapa duniani leo hii.

***3. Walikuwa ni viongozi wa muda tu sio viongozi wa kudumu***. Karama za miujiza zilitolewa kwa ajili ya uanzishwaji wa kimiujiza wa kanisa. Karama hizi ziliwapa wanadamu mamlaka ya kuwa mitume na manabii. Lakini karama za miujiza zimekoma, na hata unabii umekoma. Kwa hiyo, leo hakuna nguvu ile ya mitume na manabii, na hakuna haja ya mitume na manabii kwa sasa. Ofisi hizi hazikukusudiwa kuwa za kudumu. Mungu hakukusudia mitume na manabii kuwa na warithi. Nafasi zao zilikuwa za lazima kwa ajili ya kuanzisha kanisa tu, na sio hadi kwa kuenea kwa kanisa. Kwa sababu tunaamini Biblia, tunaamini kwamba miujiza ilitokea, na kwamba

mitume na manabii waliishi. Kwa sababu kama hiyo, tunaamini kwamba miujiza ilikoma, na kwamba mitume na manabii hawapo tena. Biblia inafundisha waziwazi kwamba miujiza ilitokea na miujiza ilikoma. Biblia inaonyesha waziwazi kwamba mitume na manabii walitolewa na kwamba mitume na manabii walitwaliwa. Biblia hiyo hiyo inafundisha vyote. Hii ndiyo maana hatumuoni mtume wala nabii katika kanisa leo hii. Hizi zilikuwa ni ofisi za muda na sio za kudumu. Yeyote anayedai kuwa ni mtume au nabii leo hii ni muongo (Ufunuo 2:2). Hata tangu mwanzo kumekuwa na mitume wa uongo (2 Wakorintho 11:13). Watu mara zote wataonekana na miujiza na ishara za uongo (2 Wathesalonike 2:8-9). Wengi watadai kutenda miujiza na matendo ya ajabu, lakini Yesu hakuwajua (Mathayo 7:22-23). Mitume na manabii walikuwa ni wa muda tu, na sio viongozi wa kudumu katika kanisa.

## SOMO LA 9

# MPANGILIO WA KUSANYIKO LA MAHALI PAMOJA UMEPANGILIWAJE?

MUHTASARI

1. *Kila kusanyiko linajitegemea lenyewe.*
2. *Viongozi wanaongoza kusanyiko moja tu la mahali pamoja.*
3. *Makusanyiko hayapangiliwi yakiwa pamoja.*

## MJADALA

***1. Kila kusanyiko linajitegemea.*** Makanisa ya Kristo yako huru kutoka katika utawala wa madhehebu. Yanajitahidi kwenda moja kwa moja kwenye mpango wa Mungu kwa ajili ya kanisa la Biblia. Wanaomba kwa ajili ya kuzaliwa kwa kanisa sahihi kama lilivyo katika Agano Jipya. Wanafanya kazi kurejeza kila mpango wa Bwana kwa ajili ya kanisa. Mojawapo ya sehemu hizi muhimu kurejezwa ni mpango wa kimaandiko wa makanisa husika. Tunapojifunza uhalisia wa kweli wa uongozi katika kanisa la Agano jipya, tufuate utawala sahihi leo. Somo lililopita lilionyesha kuwa viongozi wote wa kimaandiko wa kanisa wako katika kanisa husika. Ilifundishwa kuwa hakuna viongozi hapa duniani waliopo nje ya kusanyiko husika, makusanyiko haya hayapo chini ya wajumbe wa kamati tendaji. Kila kusanyiko lina viongozi wake lenyewe kutoka kwenye kusanyiko hilo. Hakuna utawala wa nje unaoongoza kanisa.

Neno "kujitegemea" lina maana ya "kujitawala mwenyewe." Kanisa linalojitegemea ni lile ambalo linajiongoza lenyewe. Halina nguvu ya utawala wa juu kutoka nje juu yake. Linachagua viongozi wake lenyewe, linapanga wainjilisti wake lenyewe, likitumia fedha zake lenyewe, na kuwanidhamisha washirika wanaokwenda kinyume na utaratibu, linajitegemea kwa kila njia bila uangalizi wa nje wa binadamu. Liko chini ya Kristo pekee. Kitabu chake cha mamlaka ni Biblia pekee. Linafanya ibada zake lenyewe, vikao vya kanisa, na mipango ya kazi. Kila kusanyiko husika lazima lijitegemee ili lirejeze uongozi wa Kanisa la Agano Jipya leo.

***2. Viongozi wanaongoza kanisa moja tu la mahali husika.*** Mojawapo ya kuondoka katika utawala wa kanisa la kimaandiko lilikuja pale viongozi walipoanza kuongoza zaidi ya kusanyiko moja. Hili lilibadilisha kutoka katika mpango wa Biblia mapema uliopelekea viongozi wa wilaya kutawala makanisa katika maeneo fulani. Matendo haya baadaye yalipelekea kuwepo Papa. Ili kurejeza mpango wa kibiblia wa utawala, ni lazima viongozi wasifanye kazi kwenye

kusanyiko zaidi ya moja. Ikiwa mpango wa Mungu utafuatwa, utazuia kuondoka ambapo kulipelekea Kanisa la Kikatoliki la Kirumi. Makanisa mengi ya Kiprotestanti yana viongozi wanaoongoza kanisa zaidi ya moja. Haya yana sifa nyingi kama vile "mawakala" au "mashemasi wanaosafiri." Kazi yao ni kuangalia baadhi ya makundi ya sehemu husika. Mara kwa mara husafiri kutoka kanisa moja hadi lingine katika wilaya au eneo lao. Lakini viongozi wa kimaandiko ni lazima waongoze katika kanisa la mahali pamoja. Makanisa makubwa ya Kristo yanajaribiwa kutaka kuongoza makusanyiko madogo na machanga. Makanisa ya mjini yanajaribu kutawala mambo ya makanisa ya karibu huko vijijini. Wanaweza kuwatuma wazee kuyaongoza makanisa dhaifu. Lakini huu ni mpango wa kimadhehebu. Ni hatua ya kuelekea kuhujumu mpangilio wa kanisa. Kwa kweli kusanyiko haliwezi kujitegemea ikiwa wazee kutoka kanisa lingine watajaribu kulitawala.

***3. Makusanyiko hayawezi kupangiliwa pamoja.*** Washirika wengi wa makanisa ya Kristo hapo awali walitumia miaka mingi katika makanisa ya kimadhehebu. Uzoefu huu wa muda mrefu unawatoa katika uelewa mzuri wa mpangilio wa kweli wa kanisa. Wanataka makanisa ya Kristo yapangiliwe pamoja kama makanisa yao ya awali yalivyokuwa. Hivyo, wanapenda mkataba wa makanisa katika eneo moja. Wanataka makundi yaliyopangiliwa yenye viongozi na waweka hazina. Mara kwa mara hufanya huduma za pamoja ambazo huvuruga huduma zao za ndani. Lakini hakuna makusanyiko katika Agano Jipya yameunganishwa pamoja. Kila moja linajitegemea kabisa katika utawala. Kristo aliandika barua saba katika makanisa saba ya Asia (Ufunuo 1:11). Kila kanisa lilitumiwa barua tofauti. Ingawa makusanyiko yalikuwa katika eneo moja, hakukuwa na ushirika wa makanisa. Hakukuwa na kundi la viongozi waliotawala makanisa yote saba. Kila kusanyiko katika kila mji lilijitegemea. Wakati mpango wa Agano Jipya wa uongozi wa kanisa unafuatwa, makusanyiko hayataungamanishwa pamoja.

## SOMO LA 10

# NI KWA NAMNA GANI MAKANISA YA MAHALI PAMOJA YANAJITEGEMEA?

MUHTASARI

1. *Kujitawala lenyewe.*
2. *Kujihudumia lenyewe kifedha.*
3. *Kujieneza lenyewe.*

### MJADALA

***1. Kujitawala lenyewe.*** Njia mojawapo ya muhimu ambayo makusanyiko yanajitegemea ni kwa kujitawala yenyewe. Hili limeonyeshwa katika masomo kadhaa yaliyopita. Kupoteza haki ya utawala binafsi ni njia fulani kwa kanisa kuacha kutawala mambo yao wenyewe, muda mchache ujao litapoteza mifumo mingine ya kujitegemea. Wakati wanadamu wanachukua majukumu ya kanisa, kanisa linapoteza uhuru wake wa kweli. Lakini kwa kutawala mambo yake yenyewe si njia pekee ya uhuru binafsi katika kanisa husika. Makanisa mengi hufanya maamuzi yao yenyewe lakini bado yanaendelea kutegemea misaada ya kifedha kutoka nje pamoja na mambo mengine. Utawala binafsi utaliongoza kanisa kujisaidia lenyewe na kuwa na uhuru kamili.

Hata hiyo, tofauti moja ya muhimu ni lazima ieleweke hapa. Kamwe kusanyiko haliwezi kupokea utawala kutoka nje bila kupoteza uhuru wake. Lakini kanisa linaweza kupokea msaada wa muda mfupi bila kupoteza uhuru wake. Tunalijua hili kutoka kwenye Biblia. Hakika hakuna mfano wa kusanyiko lolote katika Agano Jipya likipokea

miongozo kutoka kwa watu wa nje. Lakini tunasoma kuhusu kusanyiko kupokea msaada wa muda mfupi wa kifedha na msaada wa kiroho kutoka nje. Wazee na waangalizi wa Yerusalemu walipokea msaada wa kifedha wa muda mfupi kutoka Antiokia (Matendo 11:27-30). Paulo alipokea mali ya makanisa mengine alipokuwa akihubiri Korintho (2 Wakorintho 11:8). Kanisa la Filipi lilituma tena na tena mahitaji ya Paulo katika maeneo mengine (Wafilipi 4:15, 16). Kwa hiyo, kuna mifano ya kibiblia ya misaada ya kifedha ya muda mfupi, lakini hakuna mifano ya utawala wa nje wa muda mfupi ama mrefu.

***2. Kujihudumia lenyewe.*** Njia nyingine ambayo Mungu anakusudia makanisa kuwa huru ni katika kujihudumia kifedha. Paulo anaamuru kanisa la Filipi kumsaidia kifedha hata "mwanzo wa Injili" (Wafilipi 4:15). Kusanyiko haliwezi kuwa na uhuru kamili kama Mungu anavyotaka liwe hadi litakapojihudumia lenyewe kifedha. Msaada wa muda unaweza kuwa wa muhimu wakati mwingine, lakini kujihudumia lenyewe lazima kuwepo. Wakati wowote msaada wa nje unapopokelewa, kuna hatari ambayo mwongozo wa nje unaweza kufanywa. Baadhi ya makanisa yamejaribu hata kuyaruhusu makanisa mengine kuwafanyia maamuzi. Makusanyiko yanapaswa kusimama kwa miguu yake yenyewe.

Wazazi wanapomfundisha mtoto kutembea ni lazima wamruhusu mtoto apige hatua mwenyewe. Kama mtoto hajaribu kupiga hatua mwenyewe, kamwe hatajifunza. Lakini kwa kila hatua binafsi, anajifunza vizuri zaidi kutembea mwenyewe. Vivyo hivyo, kusanyiko lazima lichukue hatua lenyewe kuanzia mwanzo. Ikiwa makusanyiko mengine yanalibeba kifedha halitatembea lenyewe. Lakini kadiri linavyotembea lenyewe ndivyo linavyojifunza zaidi kwamba linaweza kutembea lenyewe. Linajifunza kujitegemea lenyewe kwa uzoefu. Mtetea pia anatakiwa kuwafundisha vifaranga kujitegemea kupitia uzoefu. Maadam huwatafutia chakula na kuwalisha mwenyewe, hawatajifunza kujitegemea. Lakini akiwalazimisha kujifunza kujilisha wenyewe watakuwa wakubwa haraka wakijitegemea na wenye nguvu. Ingawa baadhi ya vifaranga watakataa hapo awali kujilisha wenyewe,

mama yao atawalazimisha na kuwasukuma wakajitafutie chakula chao wenyewe. Mapema watajifunza kuwa kujilisha wao wenyewe ni mpango mzuri zaidi. Vivyo hivyo, baadhi ya makusanyiko yanalazimika kujitegemea. Baadhi yatahitaji kukemewa ili kufundishwa kujitegemea. Lakini ikiwa yanajaribu kwa bidii, yataona kuwa yatafanya vizuri zaidi kuliko walivyokuwa wanafikiri. Hivyo, yatakua na kuongezeka. Uhuru wa kweli ni pamoja na kujitegemea kifedha.

***3. Kujieneza lenyewe.*** Neno hili linamaanisha kujiendeleza. Kusanyiko linalojieneza linajitangaza lenyewe na kuieneza Injili ambayo inaanzisha makanisa mengine. Neno la Mungu ni mbegu ya ufalme au kanisa (Luka 8:11). Ndani ya mbegu yoyote kuna uhai wa muhimu kuzaa zao jingine. Hivyo, pia Biblia ina nguvu ya muhimu kuzaa na kulitangaza kanisa. Popote ilipo mioyo safi itakayolipokea Neno, makusanyiko yataongezeka. Kusanyiko halihitaji utawala wa nje ili liweze kukua au kuanzisha makanisa mengine. Kwa njia hii kila kusanyiko ni kama mgomba. Mara tu unapopandwa, una uwezo wa kukua bila msaada wa nje. Baada ya muda mchache utasababisha mgomba mpya kuchipua. Hii ndio maana ya kujieneza. Biblia inasema kuwa kanisa ni nguzo au msaada wa kweli (1 Timotheo 3:15). Kila kusanyiko linatakiwa kusaidia na kuieneza kweli. Hili sasa litasababisha makanisa mengine kuanzishwa. Pia yatasaidia kweli katika maeneo mengine. Kanisa la Yerusalemu lilitawanyika na kwenda kila mahali likihubiri Neno (Matendo 8:4). Mashirika ya nje ya umisheni au utawala wa kimadhehebu hayawezi kulieneza Kanisa la Bwana. Makusanyiko ya kanisa la Bwana yanajitegemea kwa kujitawala, kujihudumia na kujieneza.

## SOMO LA 11

# KWA NINI MUNGU ANATAKA MAKUSANYIKO YAJITEGEMEE?

MUHTASARI

1. *Hukuza viongozi na waumini.*
2. *Hukuza utoaji na kufanya kazi.*
3. *Huzuia kusambaa kwa uasi.*

**MJADALA**

***1. Hukuza viongozi na waumini.*** Ingawa hatuwezi kuelewa kwa nini Mungu anataka uhuru wa makanisa, lakini ni lazima tuendelee kutii mamlaka ya Biblia. Lakini tunaweza kuona sababu nyingi nzuri kwa nini Mungu amepanga hivyo, ni bora zaidi kwa makanisa. Sababu mojawapo ni kwamba hukuza viongozi na waumini wa kila kanisa. Wakati wowote viongozi wa kusanyiko wakiletwa kutoka nje, viongozi wa kusanyiko husika hawawezi kukua. Wakati wowote kazi za kusanyiko zinapofanywa na makundi kutoka nje, waumini wa kanisa husika hawawezi kukua kwa haraka. Ukristo unapaswa kuonyesha uwezo wa mtu. Mungu ameweka mpangilio wa kanisa ili kukuza waumini wa kila kusanyiko katika kiwango cha juu. Ikiwa wanaume wa kusanyiko husika wanaona kuwa viongozi wao watatumwa kwao na maamuzi yao yatafanywa kwa ajili yao, hawatajaribu kadiri wawezavyo kufanya sehemu yao. Mpangilio wa makanisa ya kimadhehebu unakatisha tamaa maendeleo ya kusanyiko. Katika Warumi 15:14 mtume Paulo anawaamuru ndugu walioko Rumi kujaa wema na elimu na waweze kuonyana. Watu hawa wamekua wenyewe katika kanisa huru. Lakini katika Waebrania 5:12-14, waumini wanakemewa kwa kutokukua. Waumini hawa wamekuwepo katika kanisa kwa muda

mrefu lakini hawana uwezo wa kufundisha. Wanaambiwa kuwa wanahitajika kuzoea kufundisha. Tunajifunza kufundisha kwa kufundisha. Uongozi katika kanisa unahitaji uzoefu. Mungu anataka makusanyiko yajitegemee katika uongozi ili likuze viongozi wazuri na haraka iwezekanavyo.

***2. Kukuza utoaji na kufanya kazi.*** Mpango wa madhehebu wa fedha na utawala mara zote unahitaji fedha itumwe makao makuu. Lakini katika makanisa huru ya Kikristo hatuna makao makuu ya aina hiyo hapa duniani. Mpango wa fedha ni wa kila kanisa na linatumia sadaka zake lenyewe katika kazi za kusanyiko la mahali pamoja la Bwana au liamue lenyewe fedha hizo zitatumika wapi. Hakuna viongozi waangalizi au makao makuu ambapo taasisi itasaidia. Mpango huu unahamasisha utoaji mzuri. Kama muumini atajua ya kuwa kila fedha anayoitoa katika changizo itatumika kwa kujenga kanisa husika, atakuwa na shauku ya kutoa zaidi. Ataweza kuona hitaji la wazi katika kijiji chake. Ataona ni kwa kiwango gani fedha yake inahitajika. Atahisi hisia ya kufanikiwa akiona mahitaji yakifikiwa kwa changizo zake. Njia bora zaidi ya kuhimiza utoaji wa kidhabihu ni kuweka hitaji kuu mbele ya watoaji. Mpango wa Mungu wa fedha katika kusanyiko husika unatoa motisha hii kwa mtoaji. Mpangilio wa Mungu vivyo hivyo huhimiza maslahi binafsi zaidi katika kazi zote za kanisa. Kila mwumini ataona kuwa hakuna kazi ambayo taasisi itafanya kwa ajili yake. Yeye mwenyewe anawajibika. Kama kazi itafanyika lazima aifanye. Hii itaacha majukumu katika waumini wa kusanyiko husika badala ya kuwa kwa baadhi ya makundi. Mpango wa Mungu wa makusanyiko huru ni mpango bora zaidi kwa kuendeleza utoaji na kufanya kazi.

***3. Huzuia kusambaa kwa ukengeufu.*** Ikiwa mawe kadhaa makubwa yamefungwa pamoja kwenye kipande cha kamba, mawe hayo hayako huru, ila yamewekwa pamoja. Kama mojawapo ya jiwe likianguka mtoni, litayavuta mawe mengine yaanguke pamoja nalo. Lakini kama mawe hayajafungwa pamoja, jiwe moja likianguka, mengine hayataanguka. Yako huru. Mlinganisho huu unaelezea sababu

nyingine ya makanisa kuwa huru. Mpangilio wa kimadhehebu huyafunga makanisa pamoja na kuchukua uhuru wao. Kama kusanyiko moja litakengeuka, litayavuta mengine yakengeuke. Au kama waangalizi wakuu wakifundisha mafundisho ya uongo, makanisa yote yatafuata kwa sababu yote yameunganishwa pamoja. Mpango wa Mungu ni bora zaidi kwa sababu unazuia kuenea kwa ukengeufu na mafundisho ya uongo. Hata kama makusanyiko mengi yakianza mafundisho yasiyo ya kimaandiko, makanisa mengine yatabaki kuwa waaminifu kwa sababu yako huru. Mungu anataka makusanyiko huru kwa sababu mpango huu huleta viongozi na waumini, huhamasisha kutoa na kufanya kazi, na kuzuia kueneza ukengeufu.

## SOMO LA 12

# KANISA LINALINGANA VIPI NA SERIKALI ZA KIRAIA?

MUHTASARI

1. Aina za serikali ya kiraia ni zipi?
2. Mihimili ya serikali za kiraia ni ipi?
3. Ni kwa namna gani ufalme wa Kristo ni ufalme kamili?

### MJADALA

***1. Aina za serikali za kiraia ni zipi?*** Ni vizuri katika kipengele hiki kujifunza kuhusu aina za serikali katika mataifa ili kuzilinganisha na serikali ya kanisa. Kuna aina kuu tatu za serikali za kiraia: (a) utawala huria (b) demokrasia, (c) kifalme. Utawala huria inamaanisha "hakuna utawala." Ni hali ya kutokuwa na mpangilio ambapo hakuna anayeongoza. Hakuna serikali na hakuna mwenye mamlaka. Katika hali

ya huria kunakuwa na mauaji mengi na udhalilishaji wa makundi. Hakuna nguvu ya askari au mamlaka kuilazimisha sheria na amri. Hakika kanisa halina hali ya aina hii. Biblia inawahukumu wale "wanaoidharau serikali" (2 Petro 2:9, 10). Ukristo umejengwa juu ya mamlaka ya Kristo na Neno lake. Hakika kanisa si huria. Demokrasia huongozwa na watu. Serikali ndiyo inayochaguliwa na kuhakikishwa na wale wanaoongozwa. Katika demokrasia kuna uchaguzi huru na wa wazi ili kila mwananchi awe na nafasi ya kuongoza au kuchagua atakayeongoza. Lakini kanisa si demokrasia. Kichwa cha kanisa ni Kristo, Kristo si somo la kubadilisha. Hakuna binadamu katika kanisa ambaye anaweza kuchukua nafasi yake. Washirika wa kanisa hawana haki ya kuchagua mfalme mwingine. Demokrasia ni aina nzuri ya uongozi kwa serikali za kidunia, lakini si kwa ajili ya kanisa. Mwili wa Kristo ni ufalme. Ufalme unaongozwa na mfalme. Ni serikali ambayo mtu mmoja ana mamlaka kamili. Ufalme wa kweli una mamlaka yote katika ufalme wake. Hakuna anayeruhusiwa kuuliza kuhusu haki au njia ya kuongoza. Hii inatusaidia kuona serikali ya ufalme wa Kristo, kanisa katika mwanga wake sahihi. Yesu ana mamlaka yote mbinguni na duniani (Mathayo 28:18). Yeye ni Mfalme na kiongozi wetu (Yohana 18:37). Tunawajibika katika ufalme wake au kanisa (Mathayo 16:18, 19). Kanisa ni utawala wa kifalme na Kristo kama Mfalme wa milele. Ana nguvu na mamlaka kamili.

**2. *Mihimili ya serikali ya kiraia ni yapi?*** Mihimilii au sehemu za serikali ya kiraia ni (a) bunge (b) mahakama (c) serikali kuu. Mhimili wa bunge hutunga sheria kwa ajili ya taifa. Kwa kawaida mhimili huu ni nyumba ya mkutano. Bunge ni baraza la taifa linalotunga sheria. Huandika sheria za taifa. Mhimili wa kimahakama huchunguza au kutafsiri sheria za taifa. Mhimili wa mahakama unaundwa na mahakama za ardhi zinazohukumu watu wa taifa kwa sheria zake. Mhimili mkuu wa serikali unatekeleza sheria za nchi. Unawakilishwa na mtendaji mkuu kama vile waziri mkuu. Mtu huyu ni mkuu wa majeshi na polisi. Hutekeleza sheria za nchi. Mhimili wa mtendaji ni mhimili wa utekelezaji katika kila serikali. Mhimili wa kutunga sheria

ndio unaotunga sheria, mahakama huitafsiri sheria na watendaji hutekeleza sheria za serikali yoyote ya kiraia.

***3. Ni kwa namna gani ufalme wa Kristo ni ufalme kamili?*** Ufalme wa Kristo au kanisa ni ufalme kamili kwa sababu tatu: (a) alizitunga sheria, (b) alizitoa na kuzielezea sheria, na (c) alizitekeleza sheria. Yesu hushika nafasi zote katika mihimili ya serikali katika kanisa. Anaitwa mwenye uweza wa pekee, Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana (1 Timotheo 6:15). Yeye ni Mkuu wa wafalme wa dunia (Ufunuo 1:5). Hakuna kundi la viongozi wa kanisa lililoandika sheria zake. Roho Mtakatifu alizifunua sheria zake kupitia Maandiko ya mitume (Yohana 16:13). Mafundisho ya Kristo yatamhukumu mwanadamu siku ya mwisho (Yohana 12:48). Wote tutakaa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo (2 Wakorintho 5:10). Yesu ni Mfalme, Bwana, Mkuu, na Kiongozi wetu. Kanisa lake ni ufalme ambao kupitia huo Wakristo wameokolewa (Wakolosai 1:13). Wote wanaoingia katika ufalme na watambue aina ya ufalme ambao wapo ndani yake. Hakuna anayeingia kanisani akawa kiongozi mkuu. Hakuna anayeingia kanisani kutunga sheria zake. Wote wanaoongezwa na Bwana katika kanisa ni watumwa wanyenyekevu na wanawajibika kwa Kristo Mfalme.

## SOMO LA 13

# NI KWA NINI WANADAMU HUWAFUATA VIONGOZI?

MUHTASARI

1. Hofu ya madaraka (nguvu).
2. Shauku ya kupewa zawadi (ajira au rushwa).
3. Kufuata kielelezo (kuiga)

## MJADALA

***1. Hofu ya madaraka (nguvu).*** Katika kila aina ya serikali mara zote kuna sababu kwa nini watu huwafuata viongozi wao. Mojawapo ya sababu ni hofu ya madaraka. Kama kiongozi ni mwenye nguvu sana kama vile mfalme, wafuasi wake watalazimika kumtii. Wafuasi wa aina hiyo watamuogopa sana kiongozi na wataogopa kutomfuata. Ukristo hautumii nguvu kuwasababisha waumini wake wawafuate viongozi wao. Mungu hajawahi kumlazimisha mwanadamu kumtii yeye. Ijapokuwa Yesu ana nguvu na mamlaka yote, halazimishi utii. Wafuasi wake wanamfuata kwa sababu wamechagua kumfuata. Hili pia ni kweli kwa viongozi katika kanisa. Hawana mamlaka ya kuwalazimisha waumini kutii. Haijalishi mamlaka ya kidunia kiasi gani mtu anayo, hawezi kuwalazimisha watu kanisani wamfuate. Hakuna kiongozi wa kanisa ambaye atajaribu kuongoza kwa kuwa waumini wengine wanamwogopa. Ni lazima Wakristo wamwogope Shetani, lakini hawahitaji kumwogopa mwanadamu. Yesu alisema tusimwogope yule auae mwili (Mathayo 10:28). Viongozi wa serikali wanaweza kuongoza kwa kulazimisha, lakini si viongozi katika ufalme wa Kristo. Biblia inasema katika pendo hakuna hofu, lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu (1 Yohana 4:18). Mwanadamu asifikiri kwamba anaweza kuwa kiongozi katika kanisa kwa sababu ya kulazimisha au wengine wataogopa nguvu zake.

***2. Shauku ya kupewa zawadi (ajira au rushwa).*** Sababu nyingine ambayo inampelekea mwanadamu kuwafuata viongozi ni shauku ya zawadi. Hii ni sababu mojawapo kwa nini mwanadamu hufuata maelekezo ya mwajiri wake. Anatafuta ujira ambao atalipwa. Hii ni sababu pia watu wanaweza kupewa rushwa ili wazitii amri za mtu. Wanatamani kupokea malipo ya rushwa. Kiuhalisia ajira inaheshimika. Hakuna kosa katika malipo ya mshahara katika kazi. Lakini hii si sababu ya kuwafuata viongozi katika dini. Waumini wengine watatafuta kumfuata mhubiri kwa kutarajia kupata Biblia ya bure au zawadi nyingine. Watu wanaweza kujifanya ni viongozi wa dini

ili wajipatie fedha. Lakini sifa hii si nzuri katika Ukiristo. Viongozi wanaamriwa kulichunga kundi "si kwa fedha ya aibu, bali kwa moyo" (1 Petro 5:2). Wakati mwingine mshirika mwenye uwezo anaweza kufikiri kuwa anaweza kuliongoza kanisa kwa sababu ya fedha zake. Anaweza kudhani kuwa matakwa yake yaheshimike kwa sababu anatoa changizo nyingi. Hii sio kanuni ambayo inaleta heshima katika kanisa. Kupenda fedha lazima kuondolewe katika kanisa. Fedha ndio shina la mabaya ya kila namna (1 Timotheo 6:10). Huwaharibu viongozi na huwaharibu waumini. Huwasababisha watu wasio na sifa kujinunulia nafasi za uongozi. Mtu na asiongoze au asije kanisani kwa sababu ya fedha.

***3. Kielelezo-kufuata (kuiga).*** Kanuni ya kweli ya uongozi katika kanisa ni kufuata kielelezo. Watu huwafuata viongozi wao katika Ukristo kwa sababu wanataka kuwaiga au kuwa kama wao. Huu ni mfano mkubwa wa sifa kuliko sifa nyingine. Aina hii ya uongozi huzalisha aina nzuri zaidi ya viongozi. Unafanya uongozi wa mtu utegemee sifa zake. Zaidi ya yote, kuonyesha mfano kunatoa hamasa nzuri kwa waumini. Ni rahisi kwa watu kufuata mfano mzuri. Kielelezo ni kanuni nzuri sana katika utawala wa kanisa. Kanuni hii hugusa mafundisho yote katika Biblia yanayohusu uongozi. Yesu alikuwa mfano mkuu ambao ulimwengu huu haukuwahi kutambua. Biblia inasema kuwa alianza kutenda na kufundisha kwa pamoja (Matendo 1:1). Hatujalazimishwa kuyatii mafundisho yake. Hajaahidi thawabu hapa duniani kwa waumini wake.  Lakini Yesu ni kiongozi Mkuu wa vipindi vyote. watu wengi wamejitoa kwake kuliko kwa kiongozi mwingine. Ni kwa sababu anawafanya watu wawe kama yeye. Anatuonyesha nguvu ya kielelezo. Kuiga mfano ni sababu kubwa sana na ya juu kwa wanadamu kuwafuata viongozi.

## SOMO LA 14

# KWA NINI MFANO NI MUHIMU KATIKA KANISA?

MUHTASARI

1. *Kwa sababu ya maana ya mfano.*
2. *Kwa sababu ya hitaji la mfano.*
3. *Kwa sababu ya nguvu ya mfano.*

**MJADALA**

***1. Kwa sababu ya maana ya mfano.*** Mfano ni picha ya kielelezo. Inaonyesha zaidi kuliko kusema. Ni kielelezo kinachowekwa ili wengine waone vizuri na kufuata. Biblia inasema kwamba Krisro alituachia kielelezo kwamba tufuate nyayo zake (1 Petro 2:21). Yesu alipita katika maisha haya kabla yetu ili atuonyeshe njia ya kupita. Njia tunayopaswa kupita ni rahisi kuielewa kwa sababu ametupa kielelezo safi. Huu ndio mfano. Neno "sampuli" na "mfano" yana maana sawa. Wote wafahamu kuwa sampuli ni nini. Mwuzaji anapouza sokoni, ataonyesha sampuli ya bidhaa zake. Atataka kuonyesha sampuli nzuri ili awashawishi wanunuzi watamani kununua. Hawalazimishi wanunuaji kununua, bali anawavutia wanunue kwa sampuli au mifano. Vivyo hivyo ni kweli kwa mfano wa maisha ya Mkristo. Ni lazima uwe mfano wa kuvutia ambao utawavuta wengine kwa Kristo. Mfano unaweza kuwa mzuri au mbaya. Biblia inasema miji miovu ya Sodoma na Gomora imewekwa ili iwe mfano kwetu (Yuda 7). Ni mfano mbaya. Ni mfano wa ghadhabu ya Mungu kwa waovu. Wana wa Israeli wasio waaminifu kule jangwani ni mfano kwetu (1 Wakorintho 10:6, 11). Mifano, halafu, picha, sampuli au kielelezo cha kile ambacho Mungu anataka tufanye au tusifanye. Kila Mkristo ni mfano mzuri au mbaya.

Anawaonyesha wengine kielelezo kizuri au kibaya. Mifano mizuri ni ya muhimu sana kanisani kwa sababu inaeleweka na kufuatwa kwa urahisi.

***2. Kwa sababu ya hitaji la mifano.*** Mifano mizuri ni ya muhimu pia kanisani kwa sababu inahitajika sana. Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee kwa sababu ulimwengu ulihitaji sana mfano kamili. Mungu amekuwa akishughulika na wanadamu kwa karne nyingi, lakini baada ya kuja Kristo mwanadamu angeweza kumjua na kumwelewa Mungu kwa urahisi. Dunia imeona waalimu na viongozi wengi wakubwa, lakini hakuna hata mmoja isipokuwa Yesu pekee ndiye awezaye kutoa kielelezo kamili cha maelezo yake. Dunia siku zote imetamani kuona masomo na kuyasikiliza. Bado hitaji ni kubwa leo. Wanadamu wamekuwa wakisubiri kuona mafundisho ya Yesu yakitekelezwa katika maisha ya wafuasi wake. Dunia imejawa na waalimu wenye kila aina ya mafundisho. Lakini mwalimu anayeishi kulingana na masomo yake ni wachache. Mhubiri Timotheo aliambiwa achunge nafsi yake na mafundisho yake ili ajiokoe nafsi yake na wale watakaomsikia (1 Timotheo 4:16). Kuna wanaume wengi kanisani ambao wanataka kuwa viongozi. Lakini wako wachache wanaotaka kuwa mifano. Hitaji ni kubwa ndani na nje ya kanisa. 1 Timotheo 12 inasema Timotheo anapaswa kuwa mfano "kwa" waaminio. Mstari huu katika toleo lililorudiwa linasema anapaswa kuwa mfano "kwa" waaminio. Kuna hitaji la viongozi kuwa mifano ndani na nje ya kanisa. dunia inahitaji mfano mzuri, na kanisa linahitaji mfano mzuri wa kuufuata. Mifano ni ya muhimu kwa sababu hitaji lake ni kubwa sana.

***3. Kwa sababu ya nguvu ya mifano.*** Mifano sahihi inahitajika kwa sababu ya nguvu zake. Paulo alisema hotuba na mahubiri yake si maneno ya kuvutia ya hekima za wanadamu, lakini yalikuwa "vielelezo vya kiroho na nguvu" (1 Wakorintho 2:40). Ushawishi wa Paulo ulikuwa mkubwa kwa sababu alikuwa mfano mkubwa. Wanadamu wanaweza kutoa hotuba bila kuzungumza neno moja. Biblia haisemi chochote kuhusu alichokisema Habili. Lakini kwa kufa kwake, bado anazungumza kwa mfano (Waebrania 11:4). Henoko, Ibrahimu na Yoshua hawakuwa wasemaji wazuri. Lakini walikuwa ni watu wa

vitendo. Zingatia nguvu ya mifano yao. Kanisa la Bwana leo lina wazungumzaji ambao wanasema lakini si watendaji. Uongozi wa aina hii ni dhaifu. Lakini kiongozi mwenye nguvu ni mtu anayeheshimika. Anaigwa kwa sababu ya tabia yake njema. Ana ushawishi na nguvu kubwa kwa wema. Maisha yake yana nguvu ndani na nje ya kanisa. Zingatia jinsi maisha ya Yesu yalivyobadilisha ulimwengu. Kwa zaidi ya karne kumi na tisa mamilioni ya wafuasi waliojitoa wamejaribu kuwa kama yeye.  Amebadilisha mkondo wa ulimwengu zaidi ya nguvu zote kwa pamoja. Majeshi na himaya kubwa zenye nguvu zimeanguka na kusahaulika, lakini ushawishi wa Kristo pekee unaongezeka. Hakuna kitu chenye nguvu ambacho maisha ya Yesu yanapaswa yabadilishe ulimwengu wa dhambi. Mifano ni ya muhimu sana kanisani kwa sababu ya nguvu zake.

## SOMO LA 15

# NI NANI AMBAO NI MIFANO KATIKA KANISA?

MUHTASARI

1. *Kristo*
2. *Wazee na mashemasi*
3. *Wainjilisti*
4. *Wazazi*
5. *Makusanyiko*
6. *Kila mshiriki*

## MJADALA

***1. Kristo.*** Biblia inaonyesha umuhimu wa mifano kwa kuonyesha ni kwa namna gani kila afisa na kila mshirika anatakiwa kuwa mfano. Wakristo hawawezi kuushawishi ulimwengu au kumshawishi kila mmoja kwa kulazimisha au kutoa rushwa. Ushawishi wao unatoka kwenye mifano yao. Yesu alijifanyia kwanza kila kitu ambacho Mkristo anatakiwa kufanya. Alianza kwa kutenda na kufundisha (Matendo 1:1). Alituachia mfano kuwa tuzifuate nyayo zake (1 Petro 2:21). Yeye ni Kuhani wetu Mkuu ambaye anaweza kuguswa na hisia za udhaifu wetu. Alijaribiwa katika kila hatua kama sisi tunavyojaribiwa na wala hakutenda dhambi (Waebrania 4:15). Yesu ni Mchungaji Mkuu anayewaongoza kondoo wake kuliko kuwasukuma (1 Petro 5:4). Wachungaji wa kipindi cha Yesu waliishi karibu na kondoo zao. Waliwajua kila mnyama mmoja mmoja. Mchungaji hupenda kondoo zake, na kondoo humpenda mchungaji wao na wanapenda kumfuata. Siku zote mchungaji huwa mbele ya kundi. Huwaonyesha njia ya kupita. Hawapigi wala hawalazimishi. Huwaongoza kwa upole kwa namna ambayo kondoo hutaka kumfuata. Hii ni aina ya Mchungaji ambayo Yesu alivyo. Hii ni aina ya viongozi ambao Wakristo wanapaswa kuwa.

***2. Wazee na mashemasi.*** Kama waangalizi na watumishi wa makusanyiko, wazee na mashemasi ni lazima wawe mifano katika kundi. Wazee kutoka Efeso waliambiwa wajichunge wao kwanza, ndipo walichunge kundi (Matendo 20:28). 1 Petro 5:3 inasema ***"Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi."*** Sifa za wazee ni njia ambazo ni lazima wawe mifano kwa waumini wengine na kwa ulimwengu. Mashemasi wa kwanza walichaguliwa kwa sababu walikuwa ni watu wenye ripoti ya uaminifu, waliojawa Roho Mtakatifu na hekima (Matendo 6:3). Mashemasi wanapaswa kuwa wamehakikishwa kwanza na hawalaumiwi wala hawana hatia (1 Timotheo 3:10). Wazee na mashemasi wanachaguliwa kwa sababu wanakuwa na sifa ya kuwa

mfano mwema. Kanisa litapenda kuwafuata kwa kuwa maisha yao ni mfano mwema. Hawatakiwi kuchaguliwa au kufuatwa kwa sababu nyingine yoyote. Serikali ya kanisa la Bwana inategemea mfano. Wazee au mashemasi wanapomkemea muumini mwingine, maisha yao wenyewe yanapaswa kuwa ni ya mfano mzuri. Biblia inasema kuwa mzee hawezi kuitunza familia ya Mungu kama haiongozi vizuri familia yake mwenyewe kwanza (1 Timotheo 3:4, 5). Ni lazima awe na ripoti nzuri kutoka nje ya kanisa (1 Timotheo 3:7). Wazee na mashemasi lazima wawe mfano mwema.

***3. Wainjilisti.*** Mfano mwingine wa muhimu katika kusanyiko ni mhubiri. Wainjilisti wameamriwa "wawe vielelezo" (1 Timotheo 4:12). Wawe kielelezo ulimwenguni, katika maisha, katika upendo, katika roho, katika imani, katika usafi. Paulo alimwambia Timotheo ajichunge katika mafundisho (1 Timotheo 4:16). Kwa kuweka kielelezo sahihi, pamoja na mafundisho, atajiokoa yeye mwenyewe na wale watakaomsikia. Lakini bila maisha mema au mafundisho mazuri, hataweza kujiokoa mwenyewe wala watakaomsikia. Paulo alisema kwa Wakristo wa Thesalonike ***"Mwajua wenyewe jinsi iwapasavyo kutufuata; kwa sababu hatakuenda bila utaratibu kwenu"*** (2 Wathesalonike 3:7). Paulo alieleza kuwa matendo yake yalimfanya awe kielelezo kwa watu (aya ya 9). Wainjilisti wanamuiga Kristo ili wawe kielelezo kizuri mbele ya kanisa.

***4. Wazazi.*** Baba na mama Wakristo ni lazima wawe vielelezo vizuri na vyenye nguvu kwa watoto wao. Kijana Timotheo alikuwa na mama na bibi waaminifu mbele yake (2 Timotheo 1:5). Hakuna kielelezo kilicho na nguvu kwa mtoto kama kile cha wazazi. Mtoto anajua kiukweli kile wazazi wanachokifanya nyumbani. Hawezi kudanganyika. Hili linawafanya wanawake wengi, wasioweza kusoma au kufundisha Biblia, kufundisha kwa kielelezo kizuri. Wazazi ni vielelezo au mifano mizuri katika kanisa.

***5. Makusanyiko.*** Kielelezo ambacho kusanyiko lote linaonyesha kwa wengine linaweza liwe zuri au baya. Kanisa la Thesalonike waliamriwa kuwa kielelezo kikubwa kwa waaminio wote

katika eneo lao (1 Wathesalonike 1:7). Makanisa mengine madhaifu watatiwa moyo kwa kielelezo kizuri cha kanisa imara. Wanaoandamana na wapagani wanaangalia kielelezo cha kila kusanyiko. Yesu alisema kuwa watu wake wanapaswa kuwa kama mji uliowekwa mlimani ambapo hauwezi kusitirika (Mathayo 5:14). Alisema kila Mkristo anatakiwa kuwa nuru, na wakikutanika pamoja, wanakuwa kama mji mzuri mdogo unaoweza kuonekana kwa mbali. Makusanyiko yanapaswa kuwa kielelezo kizuri.

***6. Kila mshirika.*** Kusanyiko haliwezi kuwa taa yenye nuru isipokuwa kwa kila mshirika kuangaza. Yesu alimwambia kila mmoja, ***"Nuru yenu na iangaze mbele ya watu"*** (Mathayo 5:16). Maisha ya kila Mkristo ni kitabu ambacho kinajulikana na kusomwa na watu wote (2 Wakorintho 3:3). Kila mshirika wa kanisa la Bwana ni lazima awe kielelezo cha mtu ambaye amefanana na Kristo.

## SOMO LA 16

# KUNA NAFASI ZIPI ZA KAZI KATIKA KANISA?

## MUHTASARI

1. *Wazee*
2. *Mashemasi*
3. *Wainjilisti*

### MJADALA

***1. Wazee.*** Tupo tayari sasa kujifunza maeneo ya kazi zinazofanywa na wazee wa kanisa. Tafadhali elewa kwanza maana ya neno "ofisi." 1 Timotheo 3:1 inasema, ***"Mtu akitaka kazi ya askofu,***

***atamani kazi njema."*** Hii inaonyesha kuwa maana ya ofisi katika kanisa ni kazi. Ofisi katika kanisa ni sehemu ya kuwajibikia au kazi. Watu wengi wanadhani kuwa wafanyakazi katika kanisa la Bwana ni sawa na wafanyakazi wa serikalini. Wanafikiri kuwa wana dawati na ofisi na huwaelekeza watu kitu cha kufanya. Ofisi nyingi katika biashara na serikali zimeharibika katika mataifa. Wengi wenye ofisi wametoa rushwa ili waweze kupata fedha kwa urahisi. Nafasi yao kwao ni njia ya kukwepa kazi. Wanafikiria ofisi zao kama nafasi ya juu yenye kuheshimika lakini yenye kazi chache. Wafanyakazi katika kanisa la Bwana wanaweza kufananishwa na watenda kazi wa mafuta ya mawese. Mmoja ana wajibu wa kupanda miti na kukata matunda. Mwanamke anaweza kuwa na kazi ya kubeba na kukusanya matunda ya chikichi. Halafu mtu mwingine ana wajibu wa kusaga na kupika mafuta. Ni lazima wote wafanye kazi kwa bidii katika maeneo yao waliyopangiwa. Kwa njia hii, wazee wana kazi ya kufanya, mashemasi wana kazi ya kufanya, na wainjilisti wana majukumu yao wenyewe. Kila mtu ana eneo la kujaza. Kila mmoja ana kazi maalum ya kufanya. Hii ndio maana ya ofisi yake. Ni kazi yake au aina ya kazi yake. Wazee katika kanisa wana kazi ya uangalizi (1 Petro 5:2). Wao ni waangalizi (Matendo 20:28). Wanachunga roho za waumini (Waebrania 13:17). Wao ni wachungaji wa kiroho wa kundi (Matendo 20:28).

***2. Mashemasi.*** Mashemasi ni watumishi katika kanisa. Neno "shemasi" lina maana ya "anayetumika." Ingawa Wakristo wote ni watumishi wanyenyekevu, mashemasi ni watu maalum wenye sifa ya kutumika katika mahitaji ya kanisa. Katika kanisa la Yerusalemu wanaume walitakiwa kuhudumia meza au kuangalia chakula cha waumini walio wahitaji. Kazi hii ilipewa kwa mashemasi wa kwanza (Matendo 6:1-6). Sifa za mashemasi zinaonyesha kuwa lazima wawe wanaume wenye sifa na shauku. Ni wanaume wanaoheshimika kanisani kwa sababu ya kazi na maisha yao (1 Timotheo 3:8-13). Wana nafasi yao ya kazi kanisani, kama vile wazee walivyo na kazi zao. Hii ndio maana ya "ofisi ya shemasi" (1 Timotheo 3:13). Wazee na mashemasi kulingana na Biblia ndio wenye ofisi. Ofisi nyingine nyingi na maofisa

wanaopatikana katika makanisa ya kimadhehebu hatujawasikia katika Maandiko. Katika Wafilipi 1:1 Paulo analiandikia kanisa lililoko Filipi pamoja na wazee na mashemasi. Wazee na mashemasi ni wafanyakazi katika kanisa la Bwana.

***3. Wainjilisti.*** Mwinjilisti si kiongozi kanisani, ila ana kazi maalum ya kufanya. Paulo alimwambia Timotheo afanye kazi ya uinjilisti (2 Timotheo 4:5). Mwinjilisti ni mhubiri. Eneo lake maalum la kazi ni kuhubiri na kufundisha. Ingawa kanisa la Filipi lilikuwa na wazee na mashemasi (aya ya 1), Timotheo alitumwa kwao na Paulo kufanya kazi ambayo wainjilisti walitakiwa kuifanya (Wafilipi 2:19). Wainjilisti wanajitiisha chini ya uangalizi wa wazee kama vile waumini wengine wanavyofanya. Mhubiri anayefanya kazi chini ya wazee anapaswa kuwa na heshima kubwa kwa wazee (1 Timotheo 5:17). Lakini mamlaka ya mhubiri sio neno la wazee, ila ni Neno la Mungu. Biblia inaonyesha kuwa mzee asiyeenda kwa utaratibu anaweza kukemewa pale inapohitajika ili wengine waogope (1 Timotheo 5:19-20). Mungu ana nafasi kwa wainjilisti na kwa wazee na mashemasi katika kanisa. Kila mmoja awe na sifa kamili na amejiandaa kwa kazi yake. Kila mmoja aijue nafasi yake ya uwajibikaji ili afanye kazi ambayo Mungu anatarajia yeye aifanye. Vivyo hivyo, makusanyiko yanapaswa kuelewa kazi ambazo wanaume hawa wanatakiwa kuifanya. Ni lazima kusiwe na maafisa au ofisi zilizoundwa ila zile za wazee na mashemasi. Mhubiri yeyote asitafute kuchukua kazi ya wazee katika kuliongoza kanisa. Ila kila mtu ajue na kuelewa nafasi ya kazi za Mungu katika kanisa. Pia kila mtu afanye kazi ile ambayo anaifanya kwa usahihi na ana sifa.

## SOMO LA 17

# MAJINA YA WAZEE NI YAPI?

MUHTASARI

1. *Wazee*
2. *Presbyters*
3. *Maaskofu*
4. *Waangalizi*
5. *Wachungaji ‘’pastors’’*
6. *Wachungaji ‘’shepherds’’*

**MJADALA**

***1. Wazee*. **Wazee katika kanisa la Bwana wana majina sita. Kila jina lina maana muhimu. Kwa kuchunguza maana ya kila jina, kuna mengi tunayoweza kujifunza kuhusu viongozi hawa. Jina la kawaida zaidi ni “wazee.” Neno “mzee” linamaanisha “mtu mwenye umri mkubwa.” Hii inarejelea mtu mwenye umri mkubwa katika imani na pia mkubwa kwa miaka. Wazee ni Wakristo walio na uzoefu na ujuzi mkubwa katika kanisa. Hawawezi kuwa walioongoka karibuni (1 Timotheo 3:6). Siyo eti kwamba mtu ni mzee katika kijiji chake, ikamaanisha kuwa atakubalika kuwa mzee katika kanisa. Anaweza hata kuwa ndiye mzee zaidi katika kusanyiko na bado asitambulike kama mzee wa kiroho. Anaweza hata kuwa mshirika wa kwanza kwenye kusanyiko na bado asiweze kuwa mzee wa Kibiblia. Biblia inasema kwamba Paulo aliwaita wazee wa kanisa la Efeso (Matendo 20:17). Katika miji kadhaa, wazee waliwekwa katika kila kanisa (Matendo 14:23). Tito aliachwa Krete ili kuweka wazee katika kila mji (Tito 1:5). Jina “wazee” linaonesha kwamba wanaume hawa ni wakubwa na ni

wakomavu katika imani. Wana heshima ambayo miaka ya uaminifu huleta.

***2.*** ***Presbyters.*** Jina lingine lenye maana sawa na wazee ni ‘’presbyters’’ hili ni jina lingine lenye maana ya ‘’mtu mzee,’’ limetumiwa mara moja tu kwenye Biblia (1 Timotheo 4:14). Lina maana sawa na neno “wazee” na linapaswa kueleweka wazi kutoka katika ufafanuzi ulio hapo juu.

***3.*** ***Maaskofu***. Jina lingine la wazee ni “maaskofu,” ambalo linamaanisha “waangalizi.” Linaonekana katika 1 Timotheo 3:1, 2; Tito 1:7; Wafilipi 1:1. Pia linatumika mahali pengine kumuelezea Yesu kama Mwangalizi wa roho zetu (1 Petro 2:25), na kwenye nafasi ya uangalizi ambayo Yuda Iskariote alianguka (Matendo 1:20). Jina hili la wazee linaonyesha kazi ya uangalizi ambayo wazee lazima wafanye. 1 Petro 5:2 inasema kuwa wanapaswa kuwa na uangalizi. Hii inasisitiza kwamba wazee wenyewe hawahitaji kufanya kazi zote za kufundisha na kuongoza. Lakini lazima wasimamie kazi zote za aina hiyo. Wanapaswa kusimamia au kuendesha kazi za kanisa la mahali pamoja. Kama ambavyo jinsi mashirika yote yanavyohitaji waangalizi, kanisa la Bwana lina maaskofu au waangalizi.

***4.*** ***Waangalizi.*** Kama ilivyoonekana hapo juu, neno hili lina maana sawa na maaskofu. Limeundwa na maneno mawili: “ona” na “juu.” Mwangalizi anatazama nje juu ya kanisa. Yeye ni mlinzi wa ustawi na shughuli za kusanyiko. Matendo 20:28 inasema kuwa Roho Mtakatifu amewaweka wazee wa Efeso kuwa waangalizi wa kundi. Walipaswa kujitunza nafsi zao na lile ***”kundi lote nalo.”*** Ilikuwa ni wajibu wao kuzuia walimu wa uongo ambao wangeweza kuja (Matendo 20:29, 30). Jina hili “waangalizi” linazungumzia kazi muhimu ya uangalizi ambayo ni ya lazima katika kanisa la Bwana.

***5.*** ***Pastors (Wachungaji)***. Jina hili kwa wazee linapatikana mara moja tu katika Agano Jipya (Waefeso 4:11). Ni neno jingine linalomaanisha “wachungi.” Viongozi wa kiroho wa watu wa Israeli

walikuwa wanaitwa “wachungaji” (Yeremia 2:8). Ole na laana zilikuwa zimetamkwa juu ya wachungaji wale waliokuwa wanaharibu na kuwatawanya kondoo wa Bwana (Yeremia 23:1-7). Neno “mchungaji” linafanana na neno “malisho.” Hii inathibitisha zaidi maana ya mchungaji na kondoo. Wachungaji wa madhehebu wana tofauti na wachungaji wa kibiblia. Wachungaji walikuwa wazee katika Biblia, na daima walikuwa zaidi ya mmoja katika kila kanisa.

***6.*** ***Wachungaji.*** Katika kuwaandikia wazee, mtume Petro anawaambia walishe kundi lililo kati yao. Kisha anasema kwamba wakati Mchungaji Mkuu atakapodhihirishwa (Kristo), watapokea taji isiyoharibika (1 Petro 5:1-4). Hii inaonyesha kwamba wazee ni wachungi katika kusanyiko chini ya Kristo, Mchungaji Mkuu. Huku kulinganisha wazee na wachungaji kunaleta maana. Wachungi katika nchi za Biblia walikuwa na shauku kubwa kwa kondoo zao. Waliwapenda na kuwalea vizuri (soma Zaburi 23). Wakati wote waliongoza kwa kukaa mbele yao, kamwe hawakuwasukuma kwa nyuma. Walijua tatizo la kila mnyama na waliwapenda wote. Waliwalinda, kuwalisha, na kuwanywesha maji. Mchungaji angepitia wakati mgumu kumtafuta kondoo aliyepotea au kulinda kundi lake dhidi ya hatari. Hii ndio aina ya viongozi Bwana anaowataka. Jina “mchungaji” na majina hayo mengine ya wazee wa kanisa hutusaidia kutupa uelewa mzuri kuhusu watu hawa. Wazee ni wazee wa umri, maaskofu, waangalizi, wachunaji au wachungi “shepherds”.

## SOMO LA 18

# NAMNA GANI MARA NYINGI WAZEE WANAKOSEWA KUFAHAMIKA?

MUHTASARI

1. *Majina yote sita yanamrejelea mtu mmoja.*
2. *Daima kuna mzee zaidi ya mmoja katika kila kanisa.*
3. *Wazee wote katika kanisa wana mamlaka sawa.*

## MJADILA

***1. Majina yote sita yanamrejelea mtu mmoja***. Kutokueleweka kwa baadhi ya mambo kumesababisha mkanganyiko kuhusu suala la wazee. Kutokueleweka kwanza kunatatuliwa pindi inapoeleweka kuwa majina yote sita ya wazee yanamrejelea mtu yule yule. Katika makanisa ya kimadhehebu kuna wazee ambao ni tofauti na wachungaji. Alafu pia maaskofu ni viongozi tofauti pia. Lakini majina sita tuliyojifunza katika Somo la 17 ni makundi matatu yenye majina mawili yaani "Wazee, na ''Presbyters" ni maneno mawili yanayomaanisha ''watu wazee'' "wasimamizi." na "maaskofu" na "wachungaji wa kanisa" wote wanamaanisha ''watunzaji wa kondoo." Sasa angalia jinsi hizi seti tatu za maneno zilivyounganishwa pamoja kuzungumzia mtu yuleyule mmoja. Katika Matendo 20:17, viongozi kutoka Efeso wanaitwa "wazee." Lakini mstari wa 28 unawaelezea watu hawa kama "waangalizi" na unasema kwamba wanalichunga

“kundi,” ambayo inawafanya wawe maaskofu au wachungaji wa kanisa. Kwa hivyo, wazee (presbyters) pia wanaitwa waangalizi (maaskofu) na wachungaji wa kanisa. Hizi si ofisi tofauti bali ni maneno tofauti yanayozungumzia ofisi moja. Andiko lingine linaloonesha kwamba majina sita ya wazee yote yanarejelea watu wale wale ni 1 Pet. 5. Mstari wa 1 unataja “wazee.” Mstari wa 2 unasema kwamba wazee hawa wanapaswa “kulisha kundi la Mungu,” ambayo inawafanya wawe wachungaji. Na pia mstari wa 2 unawaambia ‘’wasimamie’’ kundi, hii inawafanya wawe wasimamizi. Wazee, waangalizi, maaskofu, na wachungaji wa kanisa si viongozi tofauti tofauti. Haya ni majina sita tu ya viongozi wale wale katika utawala wa kanisa la Bwana.

***2. Daima kila kanisa lina wazee zaidi ya mmoja.*** Makosa mengine yanayofanywa mara nyingi katika makanisa ya kimadhehebu ni kule kuwa na “mchungaji” au “askofu” mmoja juu ya kanisa. Katika Agano Jipya kwenye makusanyiko, kulikuwa na wazee zaidi ya mmoja. Kamwe hatuoni katika Biblia kwamba katika kanisa kuna“mchungaji” mmoja. Badala yake, Biblia inasema kwamba “wazee” walichaguliwa katika kila kanisa (Matendo 14:23). Wazee sio (“mzee”) waliwekwa katika kila mji (Tito 1:5). Paulo aliwaita wazee au wasimamizi kutoka Efeso (Matendo 20:17, 28). Aliandika kwa “maaskofu” huko Filipi (Wafilipi 1:1). Huu ni mpango wa Kristo wa utawala wa kanisa. Kuna hekima kubwa katika mpango huu. Ikiwa mtu mmoja angekuwa akitawala kila kanisa, angeweza kwa urahisi kujiona kama “kiongozi mkuu” wa kanisa. Angejaribiwa kutafuta umaarufu kwa ajili yake mwenyewe. Asingehitaji kuwahusisha wengine katika maamuzi yake. Angekuwa na mamlaka peke yake. Mpango wa Kristo hauruhusu kiongozi kujifanya “kiongozi mkuu.” Mpango wa Biblia ni kundi la wazee kutawala katika kila kusanyiko kama hakutakuwa na wanaume wasiopungua wawili wenye sifa katika kanisa, kanisa hilo linapaswa kusubiri kuwa na wazee. Itakuwa ni kinyume na Maandiko kwa kusanyiko kuwa na mchungaji mmoja tu. Ikiwa mmoja wa wazee

wawili katika kanisa atakufa au kukosa sifa, mzee aliyebaki lazima ajiengue kuwa mzee hadi mwanaume mwingine apate sifa. Lazima kila kanisa kuwa na wazee zaidi ya mmoja.

***3. Wazee wote katika kanisa wana mamlaka sawa.*** Kosa la tatu linalofanywa mara nyingi ni mzee kujiona kuwa juu ya wengine. Huu ilikuwa moja ya ukengeufu wa kwanza wa kiutawala katika kanisa la awali. Baadaye ilipelekea wazo la "maaskofu" wa makanisa kadhaa. 1 Petro 5:4 inazungumzia kuhusu Kristo kama "Mchungaji Mkuu." Biblia haimuiti mzee wa kawaida "askofu mkuu." Kwa kuwa Kristo ndiye "Mchungaji Mkuu," tunapaswa kuamini kwamba Yeye ndiye Mchungaji Mkuu pekee. 1 Petro 2:25 inamwita Kristo "Mchungaji na Askofu wa nafsi zenu." Kamwe katika Biblia hatuoni mtu yeyote akiitwa kama "askofu" wa kanisa au kundi la makanisa. Kila kusanyiko lina "waangalizi," sio "mwangalizi" au "mchungaji." Zaidi ya hayo, wazee waliotumika kwa miaka mingi hawana mamlaka zaidi kuliko yule ambaye hana muda mrefu. Wazee katika kusanyiko kubwa hawana mamlaka zaidi kuliko wale katika kusanyko dogo. Mtume Petro alijitambulisha kama mzee mwenza wao alipozungumza na wazee wengine (1 Petro 5:1). Wazee wanatahadharishwa dhidi ya kujiinua kwa kiburi na kuanguka katika hukumu ya ibilisi (1 Timotheo 3:6). Shetani hufurahia kumfanya mzee awe na kiburi. Kiburi cha kibinadamu kinaweza kumharibu kiongozi yeyote kirahisi. Wazee wote katika kanisa wana mamlaka sawa. Hakuna ambaye ana nguvu zaidi kuliko mwingine.

## SOMO LA 19

# JINSI MADHEHEBU YANAVYOHARIBU UONGOZI WA KANISA

MUHTASARI

1. *Kufuata mamlaka ya kibinadamu badala ya mamlaka ya Biblia.*
2. *Kwenda zaidi ya mamlaka huru ya kanisa.*
3. *Kutumia viongozi na ofisi zisizo za kimaandiko.*
4. *Kubadilisha ofisi za kimaandiko.*

## MJADALA

***1. Kufuata mamlaka ya kibinadamu badala ya mamlaka ya Biblia.*** Katika somo hili na katika lile linalofuata tunataka kujadili jinsi utawala wa kanisa mara nyingi unayoharibiwa. Katika somo hili tutachunguza jinsi madhehebu yanavyoharibu uongozi wa kanisa. Katika somo linalofuata tutajifunza jinsi uongozi wa Kanisa unavyoharibiwa pia kwenye kanisa la Bwana. Sababu kuu iliyosababisha ufisadi wote huu kuingia katika uongozi wa madhehebu ni kufuata mamlaka ya kibinadamu badala ya mamlaka ya Biblia. Makosa yao makubwa ni katika kufuata katekisimu zao. Katiba za madhehebu zinaidhinisha mabadiliko mengi kwenye mpango wa Biblia kuhusu uongozi wa kanisa. Kwa kuwa katekisimu inafuatwa kama mwongozo wenye mamlaka, kwa hiyo mabadiliko na marekebisho yanafuata pia. Haiwezekani kuwarejesha watu katika mpango wa kweli wa utawala wa kanisa kadiri mamlaka ya kibinadamu ya katekisimu

yanavyozidi kuheshimiwa. Maandiko lazima yaheshimike kama mamlaka pekee katika dini. Maandiko yanatosha kabisa kumwongoza Mkristo katika matendo yote mema (II Tim. 3:17). Mamlaka yake katika uongozi wa kanisa, kama ilivyo katika kila jambo lingine la kidini, lazima yaheshimike.

***2. "Kwenda zaidi" ya mamlaka huru ya kanisa.*** Njia nyingine ambayo madhehebu yanaharibu uongozi wa kweli wa kanisa ni kushindwa kuheshimu uhuru wa kusanyiko husika. Kanuni kuu katika mpango wa Bwana wa kuongoza kanisa lake ni uhuru wa kila kanisa la mahali pamoja. Makanisa mengi ya kimadhehebu hayana utawala unaojitegemea wa kusanyiko. Aina yao ya uongozi ni tofauti kabisa. Lakini tunaonywa kutopita fundisho la Kristo (2 Yohana 9, 10). Lazima tudumu katika fundisho la Kristo kuhusu utawala wa kanisa, kama katika kila sehemu nyingine ya mpango wa Bwana kwa ajili ya kanisa lake. Tunaposhikilia mafundisho ya Biblia kuhusu utawala wa kanisa, tutakuwa na makusanyiko huru ya mahali pamoja. Wakati wanadamu wanapopita mafundisho haya na kuunda miongozo yao, hawadumu katika fundisho la Kristo. Makanisa ya kimadhehebu yameharibu mpango wa Bwana kwa kwenda zaidi ya uhuru wa kanisa la mahali pamoja.

***3. Kutumia viongozi na ofisi zisizo za maandiko.*** 1 Petro 4:11 inasema kwamba lazima tuzungumze kama maneno ya Mungu yanavyosema. Hii inamaanisha kufanya mambo ya kibiblia kwa njia za kibiblia na kuita mambo ya kibiblia kwa majina ya kibiblia. Ufunuo 22:18, 19 inatahadharisha kuhusu kuongeza au kupunguza Neno la Mungu. Kwa sababu hizi, kila sehemu ya kanisa la Bwana lazima ifuate Biblia kwa usahihi. Viongozi katika kanisa lazima wawe sawa na viongozi katika Biblia. Lakini makanisa mengi ya madhehebu yana ofisi na viongozi wasiokuwa wa kimaandiko. Hizi ni ofisi zilizoundwa na wanadamu na hazipatikani katika Biblia. Mfano ni ofisi za "katekista'', ‘’askofu'', ‘’mjumbe," ‘’askofu mkuu'', ‘’papa'' na

wengine wengi. Huku si kuzungumza kama Biblia inavyosema. Ni kuongeza kwenye Neno la Mungu. Kanisa la Bwana haliwezi kurejeshwa leo hii isipokuwa ofisi na maafisa wote ambao hawapatikani katika Agano Jipya waondolewe.

***4. Kubadilisha ofisi za kimaandiko.*** Njia ya nne ambayo madhehebu wanaharibu utawala wa kweli wa kanisa ni kwa kubadilisha ofisi ambazo zinapatikana katika Biblia. Yaani, jina la ofisi kutoka kwenye Biblia linaweza kutumika, lakini maana ya kibiblia haiheshimiwi. Hii ni kweli kwa askofu wa madhehebu. Ingawa askofu wanapatikana katika Biblia, lakini askofu wa madhehebu si kama askofu wa Agano Jipya. Hali kadhalika kwa mchungaji wa madhehebu. Katika Biblia, wachungaji walikuwa wazee katika kusanyiko. Katika makanisa ya kisasa, mchungaji ni mhubiri mwenye kuongoza kanisa moja au zaidi. Jina linabaki sawa, lakini ofisi ni tofauti. Mfano mwingine ni kuhani wa madhehebu. Katika Biblia, kila Mkristo alikuwa kuhani (1 Petro 2:5, 9). Lakini katika madhehebu makuhani ni viongozi maalumu katika kusanyiko hilo. Katika kesi hizi, tunaona kwamba jina la kimaandiko limetumika, lakini maana isiyo ya kimaandiko imetolewa. Makanisa ya madhehebu, kwa hiyo, yanaharibu utawala wa kanisa kwa kufuata mamlaka ya kibinadamu, kwa kukataa uwepo wa kanisa huru la mahali pamoja, kwa kutumia viongozi wasiopatikana katika Biblia, na kwa kubadilisha maana ya ofisi ambazo ziko katika Maandiko.

## SOMO LA 20

# JINSI MAKANISA YA KRISTO YANAVYOWEZA KUHARIBU UTALAWA WA KANISA

MUHTASARI

1. *Kuchagua viongozI wasio na sifa.*
2. *Kuwa na "wazee waigizaji."*
3. *Kubadilisha majukumu kuwa nafasi.*
4. *Kamati za kanisa.*

### MJADALA

***1. Kuchagua viongozi wasio na sifa.*** Uharibifu wa utawala wa kanisa unaweza kutokea katika kanisa la Bwana kama vile katika madhehebu. Makanisa mengine ya Kristo hayawezi kufuata mpango wa Biblia kwa makini. Kwa mfano, Biblia inatoa wazi sifa za wazee na mashemasi. Inasema kwamba mtu "lazima" awe na sifa hizi ili kuwa kiongozi (I Tim. 3:2). Neno hili "awe" linamaanisha "ni lazima." Hili ni neno zito linaloonyesha kwamba sifa hizo ni muhimu sana. Yesu alisema, "Lazima mzaliwe mara ya pili" (Yohana 3:7), ili kuingia katika ufalme wa Mungu, ni lazima kuzaliwa upya. Hakuna mbadala, vivyo hivyo, jambo hili ni sahihi katika sifa za wazee. Mtu lazima akidhi vigezo, kama sivyo hastahili. Neno "awe" linahusiana na kila sifa iliyotajwa. Ikiwa baadhi ya sifa zinafikiwa lakini nyingine hazifikiwi, mtu huyo hajakuwa na sifa. Ni ukiukwaji wa mafundisho ya Biblia

kuteua kiongozi ikiwa hakukidhi vigezo vyote muhimu. Hii itaharibu utawala wa kanisa la Bwana.

***2. Kuwa na "wazee waigizaji."*** Makosa mengine ambayo mara nyingi hufanywa katika makanisa ya Kristo ni kuwa na "wazee waigizaji." Kuna wanaume ambao hawana sifa za kuwa wazee, lakini wanataka kuitwa wazee. Si wazee wenye sifa, lakini wanataka kutenda kama wazee. Hii ni ukiukwaji wa Neno la Mungu. Mpango wa Kristo wa kuwa na wazee katika kila kanisa unategemea mfano wao mzuri wa maisha. Ikiwa mwanaume si mfano mzuri katika sifa zote zilizotolewa, hawezi kutenda kana kwamba yeye ni mfano mzuri. Fikiria ikiwa mtu si Mkristo, lakini anataka kuwa "Mkristo muigizaji." Je, kanisa linapaswa litamruhusu afanye hivyo ingawa kwa kweli si Mkristo? Hakuna mtu anayeruhusiwa kutumia jina "Mkristo" ambaye si Mkristo. Vivyo hivyo, hakuna mtu anayeruhusiwa kutumia jina "mzee" ambaye kweli si mzee. Kufanya hivyo ni kukiuka Maandiko. Hii ni uharibifu wa mpango wa Kristo wa kutawala kanisa lake.

***3. Kubadilisha kazi kuwa nafasi.*** Njia ya tatu ambayo makanisa mara nyingi uharibu mpango wa Kristo ni katika kuifanya kazi nzuri kuwa nafasi katika kanisa. Kazi ni shughuli. Mfano ni kazi au shughuli ya kuhesabu fedha za Bwana katika kanisa. Tunamwita mtu huyo "mhazini." Lakini mhazini si kiongozi. Anatekeleza tu shughuli ya kuhesabu na kutunza fedha. Kuhesabu fedha za Bwana ni kazi nzuri. Si nafasi katika kanisa. Hakuna ofisi ya kanisa inayoitwa "mhazini" katika Biblia. Lakini wakati mwingine wahasibu hupenda kubadilisha kazi zao kuwa nafasi. Hii ni kinyume na Neno la Mungu. Mtu anayetumia fimbo ndefu ili kuwafanya washirika wasilale wakati wa ibada si kiongozi. Anatekeleza shughuli au kufanya kazi inayohitajika. Lakini kwa mfano mtu huyo anaanza kujiona kuwa katika nafasi fulani katika kanisa. Fikiria anaanza kuvaa jina fulani na kuwa na mamlaka fulani. Amebadilisha kazi kuwa nafasi. Hali hiyo mara nyingi hutokea kwa kiongozi wa nyimbo. Mtu kama huyo anaweza kufanya kazi nzuri kwa

kuelekeza watu kuimba vizuri. Lakini anaharibu kazi nzuri kwa kuanza kujiona kama kiongozi katika kanisa. Katika 1 Wakorintho sura ya 14, tunasoma kuhusu washirika wa kanisa waliofanya mambo mengi kusaidia katika ibada. Lakini kwa sababu mtu alikuwa na sehemu ya kuongoza ibada haimaanishi alikuwa kiongozi. Alikuwa tu akifanya shughuli yake. Sehemu yake ilikuwa kazi, si nafasi. Kila Mkristo ana sehemu katika ibada na katika kazi za kanisa. Lakini hii haitufanyi sote kuwa viongozi. Shida huja wakati wanaume wanapofikiria zaidi kuhusu mamlaka wanayoweza kupata kuliko wanavyofikiria kuhusu huduma wanayoweza kutoa. Wanaume wengi wamekuwa na hamu zaidi ya kujulikana kuliko wanavyofikiria kuhusu kazi nzuri wanayoweza kufanya. Mtu kama huyu alikuwa Diotrefe, alipenda kuwa na hadhi (III Yohana 9). Kuna Diotrefe wengi wa kisasa katika kanisa. Ni wanaume wanaotafuta utukufu wao. Wanaharibu kanisa la Bwana kwa kutafuta kuwa "watu wakubwa." Wana anza kwa kubadilisha kazi kuwa nafasi katika kanisa. Wanaweza kuwa walikuwa wakifanya kazi nzuri, lakini wameiharibu kwa kujaribu kuitengeneza kuwa nafasi ya mamlaka. Uharibifu huu katika kanisa la Bwana ni mkubwa kama vile uharibifu wa madhehebu ulivyo mkubwa. Hatupaswi kupita fundisho la Neno la Mungu.

***4. Kamati za kanisa.*** Njia moja maalumu ambayo washirika mara nyingi hubadilisha kazi kuwa nafasi ni katika kamati. Neno "kamati" linamaanisha kundi la watu "waliowekwa" kwenye kazi fulani. Watu wanaoombwa na Kanisa kufanya kazi fulani wanaweza kujiona kuwa katika nafasi ya mamlaka. Hususani kwa mwenyekiti wa kamati. Mtu kama huyu anaweza kutamani umaarufu. Anaweza kutaka kujiita mwenyekiti wa kamati wa kudumu. Anaweza kujaribu kuwa na nafasi katika kusanyiko. Wanaume kadhaa wanaweza kuchaguliwa kurekebisha paa la jengo la kanisa. Hii ni nzuri mpaka wanaume hawa wanapojiona kama viongozi na kuwa na mamlaka juu ya wengine. Kanisa linaweza kutoa ombi kwa wanaume kadhaa kujaribu kutafuta

mchungaji wa kanisa. Kwa sababu wanapenda umaarufu, wanajiita "kamati ya wachungaji," na kudai nafasi ya nguvu katika kanisa. Hatari hii ni kubwa hasa ikiwa mtu anajiita "kiongozi wa kamati." Mtu huyu anajaribu kutawala kundi na kujitengenezea nafasi ya uongozi wa kudumu. Kamati ni hatari na zinapaswa kuepukwa kila wakati zinapowaruhusu wanaume kuwa na mamlaka na umaarufu (III Yohana 9). Mara nyingi zinakuwa za kudumu na kiongozi wao huwa afisa. Wanapenda kudai mamlaka badala ya kuwa wanyenyekevu na kufanya kazi inayohitajika. Wanageuza shughuli nzuri kuwa nafasi ya mamlaka. Kamati za kanisa mara nyingi zinachafua sheria ya kibiblia ya kanisa la Bwana.

## SOMO LA 21

# NI AINA GANI YA MAKUSANYIKO YANAYOJIANDAA NA UONGOZI?

MUHTASARI

1. *Yasiyo na mpangilio wa kimaandiko.*
2. *Yenye mpangilio mbaya usio wa kimaandiko.*
3. *Yasiyopangiliwa kimaandiko.*
4. *Yaliyopangiliwa kimaandiko.*

### .MJADALA

***1. Yasiyo na mpangilio wa kimaandiko.*** Makusanyiko yote yanapaswa kufanya kazi kuelekea kuwa na utaratibu mzuri wa uongozi wenye wazee na mashemasi wenye sifa. Lakini, hii inaweza kuchukua miaka mingi. Katika somo hili tunataka kuchunguza aina za

makusanyiko kulingana na maendeleo yao katika kujiandaa. Katika somo hili tutatumia maneno manne: "ya Kimaandiko" na "yasiyo ya Kimaandiko," "iliyopangiliwa" na "isiyopangiliwa." Maana ya "iliyo ya Kimaandiko" ni kwamba hali ya utawala wa kusanyiko ni sahihi kulingana na Biblia. "Isiyo ya Kimaandiko" inamaanisha kuwa hali hiyo si sahihi au ni dhambi. Neno "iliyopangiliwa" linamaanisha kwamba kanisa lina wazee na mashemasi. Kanisa "lisilopangiliwa" halina wazee wala mashemasi. Kanisa linaweza kuwa lisilopangiliwa lakini bado likawa la Kimaandiko. Hili ni kusanyiko lisilokuwa na viongozi wenye sifa, na kwa hiyo hakuna ambaye amewekwa. Kanisa hili ni la kimaandiko kwa sababu ni sahihi kutokuwa na viongozi kama hakuna wenye sifa. Ni mpango wa Kristo kwamba kila kusanyiko kutokuwa na viongozi katika kipindi chake cha mwanzo cha historia yake. Hii inatoa muda kwa wanaume wa Kikristo kuwa imara katika Bwana. Wakati huu, kanisa hujifunza na kujifunza kanuni za kimaandiko za utawala wa kanisa. Kanisa kama hili linaitwa "lisilopangiliwa" kwa sababu halina viongozi wenye sifa. Halijapangiliwa kikamilifu kama itakavyokuwa baadaye litakapokuwa na viongozi wenye sifa. Hakuna ubaya kwa kanisa kutokuwa na viongozi ikiwa halijapata muda wa kujiandaa. Katika Biblia, tunasoma kuhusu makusanyiko fulani yenye uongozi na mengine yasiyo na uongozi. Ni bora zaidi kutokuwa na uongozi kuliko kuwa na wale wasio na sifa. Kwa hiyo, kanisa la kimaandiko lisilo na mpangilio ni lile ambalo halina wanaume walio na sifa na viongozi ambao bado hawajateuliwa.

***2. Yenye mpangilio mbaya usio wa kimaandiko.*** Hili ni kusanyiko lisilo na mpangilio kwa sababu halina viongozi, lakini hali hii ni makosa au haifai. Sababu yenye kufanya kutokufaa ni kuwa na wanaume walio na sifa ambao wanapaswa kuwa wameteuliwa lakini hawajateuliwa. Kanisa kama hili limekuwa na miaka mingi ili kuwawezesha wanaume kuwa na sifa. Kuna wanaume wenye sifa,

lakini kanisa halijawateua. Hii ndiyo sababu inayoifanya isifae. Mara tu wanaume wanapokuwa na sifa, wanapaswa kuwa wameteuliwa. Kanisa haliwezi kufanya kazi vizuri bila uongozi kama litakavyoweza likiwa na wazee na mashemasi walio na sifa. Mpango wa Kristo ni kwamba kila kanisa liweke juhudi kuelekea mpangilio kamili wa wazee na mashemasi. Kanisa lisilo na mpangilio kimaandiko ni lile ambalo lina wanaume walio na sifa lakini hawajateuliwa kuwa viongozi

***3. Yasiyopangiliwa kimaandiko.*** Hili ni kusanyiko ambalo lina viongozi walioteuliwa na kwa hivyo limeandaliwa, lakini wanaume sio wenye sifa. Katika njia hii sio la kimaandiko. Makanisa mengine yana haraka ya kuandaa. Wanateua viongozi kabla ya kuwa na sifa. Katika hili, wanajiletea ufisadi na matatizo makubwa. Ni kimaandiko kutokuwa na viongozi ikiwa hakuna aliye na sifa. Lakini si kimaandiko kuwateua wazee isipokuwa wanaume kweli wana sifa. Hali kama hii ni mbaya zaidi kuliko kutokuwa na viongozi kabisa. Italeta matatizo makubwa na ufisadi katika kusanyiko. Kanisa lililo andaliwa lisilokuwa na sifa ni lile lililo na wanaume wasiokuwa na sifa walioteuliwa kama viongozi.

***4. Yaliyopangiliwa kimaandiko.*** Kanisa lililopangiliwa kimaandiko ni lile lenye wanaume wenye sifa walioteuliwa kuwa wazee na mashemasi. Kanisa limekataa kuwateua wanaume mpaka watakapokuwa na sifa. Kanisa kama hili limepangiliwa kwa sababu lina wazee na mashemasi. Ni la kimaandiko kwa sababu viongozi hawa wamewekwa vizuri. Na kila kanisa liwe likijifunza na kufanya kazi ili kupata viongozi walio wa kimaandiko. Lakini hakuna anayeweza kuharakisha katika kuwateua wanaume kabla ya kuwa na sifa sahihi. Katika 1 Timotheo 3 na Tito 1 zinaelezea sifa za wazee na mashemasi. Sura hizi zinahitaji utafiti mwingi. Katika somo linalofuata tutaanza kujifunza kuhusu sifa za mzee hatua kwa hatua. Makanisa iwe kimaandiko hayajapangiliwa, au hayajapangiliwa kimaandiko, au yamepangiliwa lakini si kimaandiko, au yawe ymepangiliwa

kimaandiko kulingana na maendeleo yao katika kuchagua viongozi, yanapaswa kufuata kanuni za Mungu.

## SOMO LA 22

# SIFA ZA WAZEE (I)

MUHTASARI

1. *Asiyelaumika.*
2. *Mume wa mke mmoja.*
3. *Kukesha.*
4. *Mwenye kiasi.*
5. *Mtu wa utaratibu.*

## MJADALA

Kabla ya kuanza kujifunza sifa za wazee hatua kwa hatua, kwanza kuna mambo machache ya utangulizi. 1 Tim. 3:1 inasema, ***"mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema."*** Kila mtu anayetaka kuwa kiongozi katika kanisa la Bwana inafaa kuwa na tamaa hii kwa sababu ni kazi njema. Haipaswi kutaka wadhifa huo kwa sababu ya umaarufu au mamlaka, bali kwa sababu ni njia ya kumtumikia Bwana. Lazima atake kuwa mzee ili aingie katika kazi hii ngumu, si ili kukwepa kazi, au kuwafundisha wengine jinsi ya kufanya kazi. Kazi ya mzee ni kazi inayohitaji juhudi, ikichukua masaa mengi na nguvu kubwa. Haipaswi kutafutwa kwa sababu ya tamaa ya umaarufu au nguvu. 1 Tim. 3:2 inasema, ***"Askofu ni lazima awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi, na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, na ajuaye kufundisha."*** Neno "lazima" linamaanisha "ni sharti, linahitajika, ni muhimu," au "ni lazima sana." Yesu alisema

kwamba chochote ambacho mitume watakifunga hapa duniani kitakuwa kimefungwa mbinguni (Mathayo 16:19). Sifa za wazee kwa hakika zimefungwa mbinguni na duniani. Kila moja “lazima” itimizwe. Haiwezekani kwa mtu kuwa kama mzee wa kimaandiko bila sifa zote.

***1. Asiyelaumika.*** “Hana hatia” inamaanisha “bila lawama.” Yule ambaye hana hatia hawezi kushitakiwa. Hii haimaanishi kuwa ni mkamilifu pasipo dhambi, kwa sababu wote wana dhambi (1 Yohana 1:8). Badala yake, inamaanisha kuwa mtu anayejaribu kwa bidii kushinda dhambi zake. Yuko tayari kutubu, kukiri, na kuomba msamaha anapojua makosa yake. Kwa njia hii, hawezi kulaumiwa au kushitakiwa kuwa ana tabia mbaya. Zakaria na Elisabeti walikuwa washika sheria wasiokuwa na hatia (Luka 1:6). Wajane ambao wanapaswa kusaidiwa na kanisa lazima wawe hawana hatia (1 Tim. 5:7). Sauli alikuwa hana hatia kuhusu haki ya sheria ya Musa (Fil. 3:6). Wakristo wote wanatakiwa wasiwe na hatia katika maandalizi ya kurudi kwa Kristo (1 Wathesalonike 5:23; 2 Pet. 3:14). Kutoka kwenye mistari hii tunaona kwamba inawezekana kutokuwa na hatia. Wazee lazima wasiwe na hatia au bila lawama katika tabia zao.

***2. Mume wa mke mmoja.*** Hii inahitaji mambo mawili; kwamba mwanaume lazima awe ameoa, na kwamba lazima awe na mke mmoja tu. Si kapera wala mwenye wake wengi hawezi kuwa mzee. Katika jambo hili, kama katika mengine yote, yeye ni mfano kwa kusanyiko lote (1 Petro 5:3). Kila mwanaume lazima awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke lazima awe na mume wake mwenyewe (1 Wakorintho 7:2). Ikiwa mume au mke ataoa mtu mwingine wakati mwenzi wa kwanza bado anaishi, ni uzinzi (Warumi 7:1-3). Yesu alisema kwamba huu ulikuwa mpango wa Mungu tangu mwanzo, ingawa aliruhusu mabadiliko chini ya Musa kutokana na ugumu wa mioyo ya watu (Mathayo 19:3-9). Mzee lazima awe mume wa mke mmoja.

***3. Kukesha.*** Kukesha maana yake ni kuwa macho au kuwa makini. Mlinzi wa usiku huwa macho. Yuko tayari kwa hatari zote zinazoweza kujitokeza. Walinzi kwenye kuta za miji ya Israeli walihitajika kutahadharisha kuhusu hatari inayokuja, au wangekuwa na hatia ya damu za watu ikiwa hawakuwaonya (Ezekiel 3:17-19). Waebrania 13:17 inasema kwamba wazee wanakesha kwa niaba ya roho za washarika kama wale watakaotoa hesabu. Wakristo wote lazima wawe makini, kwa maana Ibilisi kama simba angurumaye anamtafuta mtu apate kummeza (1 Pet. 5:8). Wazee wanapaswa kuhisi kwamba ni wajibu wao kuliangalia kundi.

***4. Mwenye kiasi.*** Kuwa na kiasi, ni uwa na uwezo wa kujidhibiti, kujitambua, na makini. Wakristo wanapaswa kuishi kwa kiasi katika ulimwengu wa uovu (Tito 2:12). Injili ina maneno ya ukweli na kiasii (Matendo 26:25). Hatupaswi kulala bali tukeshe na kuwa na kiasi (1 Wathesalonike 5:6). Akili zetu zinapaswa kuwa na kiasi (1 Pet. 1:13). Tunapaswa kuzingatia uzito wa maisha ya Kikristo (1 Pet. 4:7; 5:8). Mzee hapaswi kuwa hafikiri kuhusu ukweli mzito wa maisha. Lazima awe na mawazo makubwa, mwenye kufikiri, na mwenye busara.

***5. Mtu wa utaratibu.*** Ili kufuzu kuwa mzee, maisha ya mtu yanapaswa kuwa na nidhamu na mpangilio mzuri. Mtume Paulo alitoa mfano mzuri wa tabia sahihi mbele ya Wakristo wengine (1 Wathesalonike 2:10; 2 Wathesalonike 3:7). Mwenendo wetu wa maisha unapaswa kuwa wa ukweli na mzuri mbele za wasio Wakristo ili kuwashawishi kuja kwa Kristo (1 Pet. 2:12). Maisha ya mzee yanapaswa kuwa manyoofu nay a kweli ili kuwa mfano kwa wote wanaomjua.

## SOMO LA 23

# SIFA ZA WAZEE (II)

MUHTASARI

1. *Mkaribishaji.*
2. *Ajuaye kufundisha.*
3. *Asiyezoelea ulevi.*
4. *Si mpiga watu.*
5. *Si mpenda fedha. (asiye na tamaa).*
6. *Mvumilivu.*

## MJADALA

***1. Mkaribishaji.*** Somo la sifa za wazee linahitaji kusomwa kwa kina. Kila kipengele kinapaswa kueleweka vizuri. Sifa hizi kimsingi ni sifa ambazo kila Mkristo anapaswa kuwa nazo. Ni chache tu ambazo zinahusiana na mtu aliyeoa ambazo ni tofauti na tabia za Mkristo yeyote aliyekomaa. Vigezo vingi kila Mkristo lazima ajitahidi kuwa navyo. Moja ya hizo ni kuwa mkaribishaji. Tito 1:8 inasema kwamba mzee lazima awe mkaribishaji. Hii inamaanisha kumkaribisha nyumbani mtu mwenye uhitaji. Ni kuonyesha wema wa Kikristo kwa kushiriki chakula na makazi. Ukarimu unapaswa kuoneshwa kwa watu wote, lakini hasa kwa Wakristo wenzake (Wagalatia 6:10). Warumi 12:13 inasema, ***"Kwa mahitaji ya watakatifu; mkifuata ukarimu."*** Waebrania 13:2 inasema, ***"Msisahau kuwafadhili wageni: kwa maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika bila kujua."*** Kifungu kinarejelea wakati ambapo Ibrahamu alikuwa mkarimu kwa wageni ambao kwa kweli walikuwa malaika (Mwanzo 18:1-8). 1 Yohana 3:17 inasema, ***"Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni***

***mhitaji, akamzuilia huruma zake, je! Upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo?''*** 1 Pet. 4:9 inasema, ***"mkaribishane ninyi kwa ninyi, pasipo kunung'unika.''***

***2. Ajuaye kufundisha.*** Neno "ajuaye" linamaanisha kuwa na ujuzi. Mzee lazima awe mfundishaji mzuri wa Biblia. Hii inatokana na kujifunza kwa makini, maandalizi ya bidii, na uzoefu mwingi katika ufundishaji. Mwinjilisti pia lazima awe ajue kufundisha (2 Timotheo 2:24). Ukristo ni dini inayofundishwa. Yesu alisisitiza kuwafundisha mataifa yote, kubatiza watu, na kisha kuwafundisha tena (Mathayo 28:19, 20). Yesu alisema kwamba Mungu anawavuta watu kwa Kristo kwa kusikia na kujifunza (Yohana 6:44, 45). Paulo alimwambia Timotheo kufundisha mambo aliyojifunza kwa watu waaminifu ambao wangeweza kufundisha na wengine pia (2 Timotheo 2:2). Kanisa la awali halikukoma kufundisha na kuhubiri habari za Yesu Kristo (Matendo 5:42). Wakristo wa Kihebrania wangeweza kuwa walimu, lakini bado walihitaji mtu awafundishe kanuni za kwanza za neno la Mungu (Waebrania 5:12). Maandiko haya yanaonyesha umuhimu mkubwa wa ufundishaji mzuri na walimu wazuri katika kanisa. Mzee lazima awe mfano mzuri kwa wengine kwa kuwa mfundishaji mzuri na mwenye ujuzi wa Neno la Mungu. Lazima aweze kulilisha kundi (Matendo 20:28). Atahitajika kushinda ubaya na dhambi katika kanisa kwa ufundishaji imara. Lazima awe anajua kufundisha.

***3. Asiyezoelea ulevi.*** Hii inamaanisha kwamba mzee hapaswi kuwa na mwenendo wa ulevi au chochote kinachompelekea mtu kuwa mlevi. Paulo alisema kwamba hatatiwa chini ya uwezo wa kitu chochote (1 Wakorintho 6:12). Alisema kwamba walevi hawataurithi ufalme wa Mungu (1 Wakorintho 6:10). Walevi wanakabiliwa na umaskini, huzuni, maumivu, kuzungumza ovyo, majeraha yasiyo na sababu, na uwekundu wa macho (Mithali 23:21, 29-35). Divai ishukapo yenyewe taratibu huuma kama nyoka na kugonga kama fira. Hii ni divai inayosababisha ulevi. Divai inaweza kutumika ipasavyo katika Meza ya

Bwana (Mathayo 26:29). Inaweza pia kutumika kama dawa (1 Timotheo 5:23). Lakini kutumia divai inayompelekea mtu kuwa mlevi ni dhambi. Wazee wanapaswa kuwa mfano mzuri kwa kanisa kwa kutokuwa walevi.

***4. Si mpiga watu.*** Mzee si yule anayepiga wengine. Yeye ana uwezo wa kuwahamasisha wengine bila kutumia kiboko. Kamwe Mkristo asipige mtu yeyote. Yesu alifukuza wanyama nje ya hekalu kwa fimbo (Yohana 2:15). Wazazi wanapaswa kuwachapa watoto wao kwa ajili ya kufundisha (Mithali 13:24). Lakini wazee wanatumia nguvu ya mfano wao badala ya fimbo au kiboko. Adhabu ya kimwili inatumika na serikali (Warumi 13:3, 4). Lakini ufalme wa Kristo hautawaliwa kwa upanga (Mathayo 26:51, 52). Neno la Mungu ni upanga wenye nguvu zaidi kuliko upanga wowote wa kimwili (Waebrania 4:12). Kumgeuzia shavu lingine mtu anayekupiga kutashinda uadui kwa njia bora zaidi kuliko ubishani (Mathayo 5:39). Mzee ni mfano kwa Wakristo wengine kwa kukataa kuwa mpiga watu.

***5. Si mpenda fedha au mapato ya aibu.*** Mzee si mmoja wa wenye tamaa. Mapato ya aibu au faida ya ulimwengu. Mtu mwenye tamaa ni yule anayefikiri kwamba maisha yake yamejengwa katika wingi wa vitu anavyovimiliki (Luka 12:15). Anahifadhi hazina kwa ajili yake mwenyewe na si kwa ajili ya Mungu (Luka 12:21). Yesu alisema hatuwezi kumtumikia Mungu na mali (Mathayo 6:24). Wenye tamaa ni waabudu sanamu (Kol. 3:5). Hawawezi kuingia mbinguni (1 Wakorintho 6:9, 10). Lazima waondolewe katika kanisa (1 Wakorintho 5:11). Wakristo hawatafuti kuwa matajiri. Faida yao kuu ni utauwa. Wakiwa na chakula na mavazi, wanatosheka. Wanajiepusha na majaribu na tanzi za utajiri ziwanasazo watu katika uharibifu. Wanajua kwamba kupenda fedha ni shina la mabaya ya kila namna na kunawafanya watu kufarakana na imani na kujichoma kwa maumivu mengi (1 Timotheo 6:6-10). Tuzo ya Mkristo iko Mbinguni (Mathayo 5:12). Anakwepa ubinafsi na tamaa ambazo huletwa na tamaa ya fedha.

Wazee wanapaswa kuwa wanaume ambao wameweka mfano mzuri katika kujiondoa katika tamaa ya fedha na vitu vya kidunia. Hawana tamaa ya fedha na mapato ya aibu.

***6. Mvumilivu.*** Mzee ni mpole na mvumilivu. Yeye ni mwenye busara na mwenye huruma. Hubeba mzigo pasipo hasira. Hakati tamaa kirahisi akivunjwa moyo. Ni mwenye kuvumilia. Kila Mkristo anapaswa kuwa na uvumilivu (II Pet 1:6). Kujaribiwa kwa imani huleta uvumilivu (Yakobo 1:3). Kusaidiana katika matatizo hutupa ujasiri kwa Mungu, kwa sababu ya uvumilivu wa mzee humwezesha kufariji wengine wenye matatizo. Kwa sababu ni mpole na mwenye busara, washirika hutegemea ushauri wake wanapojaribiwa. Husaidia majadiliano ya kanisa yasilete migogoro. Hufanya kusanyiko liwe imara na lenye utulivu. Uvumilivu ni sifa muhimu inayohitajika kwa kila Mkristo. Wazee ni vielelezo vya uvumilivu.

## SOMO LA 24

# SIFA ZA WAZEE (III)

MUHTASARI

1. *Si mwepesi wa hasira (hakasiriki haraka).*
2. *Mwenye kusimamia nyumba yake vema.*
3. *Ana watoto waaminio.*
4. *Asiwe mtu aliyeongoka karibuni.*
5. *Ashuhudiwaye mema na watu wa nje.*
6. *Wakili wa Mungu.*

## MJADALA

***1. Si mgomvi (si mwepesi wa hasira).*** Tito 1:7 inasema lazima awe mtu asiye na mashitaka. Anaweza kudhibiti hasira yake. Hafanyi mazungumzo au matendo kwa hasira. Yeye ni mtu wa amani na anajitahidi kuleta amani. Yesu aliwabariki wapatanishi (Mathayo 5:9). Wakristo wanapaswa kuishi kwa amani na watu wote. (Rum. 12:18). Wana hekima ya kimungu ambayo inawapa unyenyekevu na rehema. Wanapanda katika amani matunda ya haki. Wanatafuta amani (Yakobo 3:17, 18). Tumeamriwa: ***"uchungu wote, na ghadhabu, na hasira, na kelele, na matukano yaondoke kwenu, tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi"*** (Waefeso 4:31, 32). Tunatakiwa kuwa wepesi wa kusikia, na si wepesi wa kusema; wala kukasirika; (Yakobo 1:19). mtu mgomvi ni yule anayependa migogoro. Anajulikana kwa kuleta machafuko na ugomvi. Mzee anachaguliwa kama mfano wa amani na unyenyekevu. Si mgomvi wala si mwepesi wa hasira.

***2. Mwenye kusimamia nyumba yake vyema.*** Mzee ni mume bora na baba bora. Tabia yake nzuri imeathiri familia yake kwa njia ya ucha Mungu. Familia ya mtu humwona na kumjua vizuri zaidi kuliko yeyote. Hivyo, wao ni tangazo zuri au baya ya tabia yake. 1 Timotheo 3:5 inasema kwamba ikiwa mtu hawezi kuongoza nyumba yake, atawezaje kutunza kanisa la Mungu. Nyumba na kanisa vinaongozwa kwa kanuni za Kikristo. Mfano na uwezo wa mtu vinaweza kufahamika na familia yake. Ikiwa mtu ameshindwa kuongoza vyema familia yake, amejidhihirisha kuwa hakuwa na uwezo wa kustahuli kuwa mzee. Kornelio alikuwa na hofu ya Mungu na familia yake yote (Matendo 10:2). Familia yake ilimheshimu na kufuata mfano wake wa kutaka kutenda mema. Mzee lazima aiongoze vizuri familia yake ili aweze kuwashauri wengine watakaohitaji msaada wake katika shida za

kifamilia. Kuhani Eli aliadhibiwa kwa sababu hakuwa na nidhamu nzuri kwa wanawe (1 Samweli 3:13). Hivyo, wanapaswa kwanza kujithibitisha katika nyumba zao ili kuweza kutosheleza kuwa wasimamizi katika familia ya Mungu, yaani, kanisa.

***3. Mwenye watoto waaminio***. Hii inaendeleza hitaji lililozungumziwa hapo juu. Watoto wa mzee wanapaswa ***"kutiishwa katika ustahivu"*** (1 Timotheo 3:4). Wanapaswa kuwa ***"watoto wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii"*** (Tito 1:6). Hivyo, watoto wa mzee wanaweza kusaidia kumpa sifa au kumchafua. Akina baba hawapaswi kuwachokoza watoto wao bali kuwalea katika adabu na maonyo ya Bwana (Waefeso 6:4). Baba anaonesha jinsi anavyoweza kufundisha na kunidhamisha wengine kwa jinsi anavyofundisha watoto wake mwenyewe. Hatakiwi kuwasimamia kwa njia ambayo itawaletea hasira bali ili kuwalea na kuwaadabisha kwa upendo na kwa kujali. Uongozi kama baba unampima mwanaume kama kiongozi mzee. Ikiwa watoto wa mwanaume ni fisadi na wasiotii, hii inaonyesha kuwa baba hajui jinsi ya kuleta utiifu. Hivyo, hana sifa ya kusimamia kusanyiko. Mzee lazima awe na watoto waaminifu ambao wapo chini ya nidhamu kwa ustahivu wote.

***4. Asiwe mtu aliyeongoka karibu.*** Mzee hawezi kuwa muongofu mpya. Muongofu mpya ni yule ambaye hana uzoefu na hafai kutokana na uchanga. Neno "mzee" lenyewe linamaanisha mtu mkomavu na mzoefu. Mshirika aliyeokoka hivi karibuni hawezi kuwa mzee. Muongofu mpya yuko katika hatari ya kujivuna na kuanguka katika hukumu ya Ibilisi. (1 Timotheo 3:6). Mkristo mpya bado hajawa tayari kwa uongozi. Biblia haisemi ni miaka mingapi inahitajika kwa ukomavu, lakini inaeleza tabia za ukomavu. Mtu mmoja anaweza kujenga tabia hizi kwa miaka michache, wakati mwingine inaweza kumchukua miaka mingi. Kijana mdogo anahitaji umri na uzoefu ili apate hekima. Mzee si mchanga.

***5. Ashuhudiwaye mema na watu walio nje.*** Mzee lazima awe na jina zuri kutoka kwa wasiokuwa washirika (1 Timotheo 3:7). Sifa yake haipaswi kuwa na lawama  kutoka kwa watu wa nje. Watu ambao anafanya nao kazi, marafiki, majirani na watu anaoshughulika nao watamheshimu kutokana na tabia yake nzuri. Atakuwa mwangaza kwa wale walio gizani (Mathayo 5:14). Anaangaza nuru yake ili watu waweze kuona matendo yake mema na kumtukuza Mungu (Mathayo 5:16). Wale wasioamini watamheshimu kwa maisha yake mazuri. Wasio Wakristo kila wakati wanaangalia ili kutuhukumu. Lakini wakati wanapotoa heshima kwa maisha ya Mkristo wa kweli badala ya mashitaka, inazungumzia mazuri kuhusu Mkristo huyo. Mtu wa aina hiyo lazima awe mzee. Atajulikana kwa maisha yake mema katika jamii anayoishi. Hii ndiyo maana ya kushuhudiwa mema kutoka kwa wale wanaomzunguka.

***6. Wakili wa Mungu***. Tito 1:7 inasema kwamba mzee lazima awe mtu asiyeshitakiwa neno kama wakili wa Mungu. Wakili ni yule ambaye amewekwa kuwa msimamizi wa mali. Yeye ni mtunzaji wa vitu vya thamani. Ana jukumu la kutunza mali za bwana wake. Ni lazima wakili awe mwaminifu daima (1 Korintho 4:2). Vitu vya thamani vilivyoachwa mikononi mwa mzee ni roho za thamani za washirika (Waebrania 13:17). Lazima awatunze kama mtu atakayetoa hesabu. Ameaminiwa kwa vitu vya thamani zaidi duniani (Mathayo 16:26). Jukumu lake ni kubwa. Kwa hiyo, ili kuwa mzee, mtu lazima ajue jinsi ya kuwa mwaminifu katika majukumu makubwa. Lazima awe mwaminifu na mali za thamani ambazo ni roho za wengine. Lazima ajisikie kuwa na nguvu kuhusu uwajibikaji wake. Mzee lazima awe na uzoefu kama wakili mwaminifu wa Mungu.

## SOMO LA 25

# SIFA ZA WAZEE (IV)

MUHTASARI

1. *Asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake.*
2. *Mpenda wema.*
3. *Mwenye haki.*
4. *Mtakatifu.*
5. *Mwenye kudhibiti nafsi yake.*
6. *Ashikaye Neno la imani.*

**MJADALA**

***1. Si mtu wa kujipendeza mwenyewe.*** Mzee hawezi kujipendeza nafsi yake mwenyewe (Tito 1:7) . Asiwe mbinafsi au mkaidi. Yuko tayari kuachilia matamanio yake binafsi badala ya kudai njia yake mwenyewe. Mtu asiyemcha Mungu na wa kidunia hujipenda mwenyewe (2 Pet. 2:10), lakini mzee hapaswi kuwa hivyo. Hafanyi neno kwa kushindana wala kwa majivuno, bali kwa unyenyekevu, huwahesabu wengine kuwa bora kuliko yeye mwenyewe. Anapendezwa na mambo ya wengine na si mambo yake tu (Flp. 2:3, 4). Yeye si mtu anayependa kuwa na ukuu (2 Yohana 9). Mshirika mwenye kujipendeza anaweza kuliharibu kusanyiko. Anakataa kushirikiana isipokuwa yeye mwenyewe ameridhika. Anadhani kanisa zima linapaswa kumtazama yeye. Kanisa haliwezi kuwa mtu wa aina hii. Utawala wao ni kwa mfano na unyenyekevu na si kwa ajili ya vurugu. Kiongozi mbinafsi husababisha matatizo na kutaka kufuatwa. Sababu ya Yesu kuwa kiongozi mkuu ni kutokuwa na ubinafsi na unyenyekevu wake. Hata kwa mamlaka na uwezo wake wote. Hakutafuta njia yake mwenyewe. Wachungaji wapo chini ya Mchungaji Mkuu, wazee wanapaswa kufuata kielelezo Chake. Hakuna kitu kinachohitajika sana kanisani

kuliko unyenyekevu. Wazee wanaonyesha njia ya kutokuwa na ubinafsi na upole. Wao si watu wa kujipendeza nafsi zao.

***2. Mpenda wema.*** Mzee anapenda yote yaliyo mema na adili (Tito 1:8). Anachukia yote yaliyo maovu (Rum. 12:9). Anapenda watu wema kama washirika. Washirika waovu huharibu maadili mema (1 Kor. 15:33). Anapenda maeneo na vitu vizuri. Yeye hujiepusha na kila aina ya uovu (1 Thes. 5:21, 22), na hushikilia sana lililo jema. Furaha yake ni katika kumcha Mungu. Wengi wanaweza kujifunza kuhusu aman kwa kujifunza kile anachofurahia. Tunaweza kujua tabia nyingi za mtu kwa kujua aina ya masahaba na matendo anayotenda. Mtu anayestahili kuwa mzee lazima awe mpenda watu wema na mambo ya haki.

***3. Mwenye haki.*** Mzee ni mwadilifu, mwaminifu, au mwadilifu (Tito 1:8). Matendo yake huwa ya haki siku zote. Haonyeshi upendeleo kwa kupendelea mshirika mmoja kuliko mwingine. Hataruhusu ufisadi wowote kumshawishi kufanya vinginevyo. Hukumu na maamuzi yake daima huwa katika uadilifu na uaminifu. Anatumia akili yake katika mambo ambayo ni ya kweli, ya uaminifu, ya haki, safi, ya kupendeza, yenye sifa njema, na wema (Flp. 4:8). Katika kazi yake kama mwangalizi atakuwa na vishawishi vingi vya ufisadi. Washirika wasiomcha Mungu au wasio washirika, wenye ubaguzi watajaribu kugeuza mawazo yake. Mara nyingi atatamani kupendelea jamaa au rafiki zake katika mambo ya kanisa. Atajikuta kwamba mara nyingi ni vigumu sana kujua ni nini haki na kisha ni vigumu zaidi kufanya kilicho sawa. Lakini lazima awe mtu ambaye washirika wanaweza kuwa na imani naye. Lazima wajue kwamba kwa yeye watatendewa sawasawa kila wakati. Hii ndiyo maana ya kuwa mwenye haki.

***4. Mtakatifu***. Mzee ni mtakatifu (Tito 1:8) . Maisha yake ni safi. Amejitolea. Wakati na juhudi zake zimetengwa kwa matumizi tofauti. Mwili wake unatolewa kwa Mungu kama dhabihu iliyo hai na takatifu (Warumi 12:1). Yeye hajichafui nafsi yake kwa tabia potovu, kwa maana Roho Mtakatifu anakaa katika hekalu la mwili wake (1 Kor. 3:16, 17). Kama mwangalizi anatafuta kuliweka kanisa kwa Kristo kama kanisa tukufu, lisilo na ila wala makunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa (Waefeso 5:27). Yeye huinua

mikono mitakatifu katika maombi (I Tim. 2:8). Anajua kwamba ameitwa kwa mwito mtakatifu (2 Tim. 1:9). Anawaongoza wengine kwenye utakatifu kwa sababu yeye ni mtakatifu.

***5. Mwenye kudhibiti nafsi yake.*** Mzee ni mwenye kiasi au mwenye kujizuia (Tito 1:8). Anatumia nidhamu binafsi. Yeye hajiruhusu kutokuwa na kiasi na kupita kiasi. Injili ni ujumbe wa haki, kiasi, na hukumu ijayo (Matendo 24:25). Kama vile mkimbiaji anavyopaswa kuwa na kiasi ili kujiandaa kwa ajili ya mbio, vivyo hivyo ndivyo anavyopaswa Mkristo awe, bali kwa taji isiyoharibika badala ya taji iharibikayo (1 Kor. 9:25). Ni lazima tujiweke chini ya udhibiti na kuitiisha miili yetu ili tusije tukapotea baada ya kuwahubiria wengine (1 Kor. 9:27). Roho Mtakatifu huzalisha kiasi kama kimoja cha matunda ya Roho (Gal. 5:23). Mzee anaweza kwa msaada wa Mungu kudhibiti hasira yake na hamu yake. Maisha yake ni ya kujizuia. Hajiruhusu kamwe kupoteza udhibiti. Jinsi gani makanisa yanahitaji mifano ya kiasi kutoka kwa wazee wao!

***6. Ashikaye Neno la imani.*** Tito 1:9 inafundisha kwamba mzee lazima ashike sana Neno la imani ili kwa mafundisho yenye uzima aweze kuonya na kuwashinda wale wanaopinga. Haya ni maagizo zaidi ya "kuweza kufundisha." Ni lazima awe na uwezo wa kufundisha wasioamini pamoja na waumini. Ni lazima ajue mafundisho ya uwongo na aweze kuyapinga. Ni lazima awe na sifa za kustahili kukutana na upinzani katika Neno la Mungu na katika roho ya kuhimiza. Hili linahitaji mzee afundishwe kwa uthabiti katika mafundisho yenye uzima (2 Tim. 1:13). Anapaswa kuwa na msingi mzuri kiasi kwamba wapinzani wote hawawezi kumuondoa. Ni lazima awe mwalimu thabiti lakini mkarimu na mwenye nguvu. Huku ni kushikilia Neno la Mungu aminifu. Hii inakamilisha utafiti wa viwango vilivyoorodheshwa vya sifa za wazee. Lakini hatua ya mwisho tunajifunza kutoka katika I Tim. 3:10 inayoonyesha kwamba wazee na mashemasi lazima kwanza 'wathibitishwe. Hii ina maana kwamba sifa hizi zilizosomwa hapo juu lazima zionekane wazi kwa mtahiniwa yeyote. Kanisa zima lilipaswa kushuhudia sifa hizi za maisha zikionyeshwa na kuthibitishwa mara nyingi katika maisha ya mzee mtarajiwa. Hii inaeleza tena kwamba kustahili kuwa mzee ni mchakato

unaochukua muda. Unahitajika wakati wa kutosha ili kanisa liwe na hakika na sifa hizi. Ikiwa hawezi kuonekana kuvaa sifa hizi kwa muda mfupi. Afadhali awe na muda wa kupimwa na kuonekana ili athibitishwe. Lazima kwa hakika na kwa dhati wawe mbali na tabia mbaya. Kuwa mzee hakika inawezekana, lakini si rahisi. Mahitaji ni ya ndani na nje. Hakuna ofisi nyingine au afisa wa aina yoyote ambaye analazimika kuwa na kiwango kama hicho. Lakini hii ni kwa sababu hakuna ofisi nyingine iliyo muhimu sana kuliko ile ya wazee.

## SOMO LA 26

# SIFA NA KAZI ZA MASHEMASI

MUHTASARI

1. *Wadhifa wao.*
2. *Kazi yao.*
3. *Sifa zao.*

### MJADALA

***1. Wadhifa wao***. Afisa mwingine katika makusaniko ya Agano Jipya alikuwa shemasi. Baada ya kutaja sifa za wazee, Biblia pia inatoa sifa za mashemasi (I Tim. 3:8-13). Mstari wa 10 unasema, ***"waitende kazi ya shemasi."*** Mashemasi, walikuwa maofisa katika kanisa la Bwana. Katika Fil. 1:1 mtume Paulo anaelekeza barua yake kwa watakatifu huko Filipi ***"pamoja na maaskofu na mashemasi."*** Hii inaonyesha kwamba mashemasi walihudumu kama maofisa pamoja na wazee (au maaskofu) katika uongozi wa kusanyiko. Kutokana na mistari hii tunajifunza kwamba ofisi ya shemasi ni ofisi nyingine katika kusanyiko na kwamba ni ofisi tofauti na ile ya wazee. Katika Matendo 6:1-6 tunajifunza juu ya uteuzi wa wanaume katika kanisa la Yerusalemu ili kuhudumia chakula na kusaidia washirika wenye uhitaji. Kazi yao ilikuwa kuwa ***"huduma ya kila siku"*** kwa wajane na

washirika wengine wenye uhitaji (Matendo 6:1). Mitume walihitaji mtu wa “kuhudumia meza” (Matendo 6:2) badala yao. Maneno haya “huduma” na “tumikia” ni neno lile lile la Kiyunani ambalo neno “shemasi linapotokea. Hii inatuambia kwamba wanaume saba waliochaguliwa walikuwa mashemasi katika kusanyiko la kwanza. Kwa hiyo, ofisi ya shemasi ni nafasi muhimu na ya lazima katika kusanyiko la kanisa la Bwana.

***2. Kazi yao.*** Mashemasi kamwe hawaitwi “waangalizi” wa kanisa. Wazee ndio waangalizi (I Pet. 5:1-2). Hawaambiwi kutawala kamwe, ingawa wazee wanapaswa “kutawala vyema” (I Tim. 5:17). Kazi ya mashemasi ni kazi tofauti na ya wazee. Kwa kuwa neno “shemasi” linamaanisha “kutumika”, tunaona kwamba mashemasi ni “watumishi” wa kanisa. Sehemu yao si uangalizi bali ni usaidizi. Kama vile mashemasi wa kwanza walivyochaguliwa kuwasaidia mitume, mashemasi wa siku hizi watawasaidia wazee ambao ni waangalizi wa kiroho. Kazi yao ni kufanya kazi na kuhakikisha ibada ya kusanyiko inaenda vizuri na kwa ufanisi. Popote inapowezekana watawasaidia wazee kufanya kazi muhimu zaidi ambayo wazee pekee wanaweza kufanya. Mashemasi wawili wa Yerusalemu pia walihubiri kama wainjilisti (Stefano na Filipo). Lakini hii haitakuwa hivi kila mara kwa kila shemasi. Kazi ya shemasi ni kuwasaidia wazee wa kusanyiko ili wasiwe na kulemewa na mambo ambayo wanaume wengine wanaweza kushughulikia. Kama ilivyokuwa kwa wazee, daima kulikuwa na "mashemasi" badala ya "shemasi" katika kila kanisa. Hakuna shemasi aliyekuwa na umuhimu zaidi kuliko mashemasi wengine. Wote walikuwa watumishi wanyenyekevu wa kusanyiko na wasaidizi wa wazee.

***3. Sifa zao.*** Maafisa wote katika kanisa la Bwana lazima wawe mifano, kama Yesu, kichwa, ni mfano mkuu. Kwa hiyo, mwanadamu lazima awe na sifa fulani kama kielelezo ili kuteuliwa kuwa shemasi. Mashemasi wa Yerusalemu walichaguliwa kwa sababu walikuwa watu wenye sifa nzuri waliojaa Roho Mtakatifu na hekima (Matendo 6:3). Pia walikuwa “wamejaa imani na nguvu” (Matendo 6:5, 8). "Ripoti yao ya uaminifu" ilikuwa jina na sifa nzuri ndani na nje ya kanisa. “Kujazwa na Roho Mtakatifu” kulionekana katika maisha yao

matakatifu. "Hekima" yao ilikuwa akili nzuri ya vitendo na uamuzi wa uangalifu katika kazi yao. Kwa kuwa “waliojaa imani na nguvu” walikuwa watu wa tumaini kubwa kwa Mungu, kwa hiyo, watu wenye uwezo na ushawishi ambao huletwa na imani. 1 Tim. 3:8-13 inatoa orodha kamili zaidi ya sifa, ambapo tunajifunza kwamba shemasi lazima awe “mstahivu” au mjuzi na mwenye busara. Hapaswi kuwa na “ndimi-mbili” au wa nyuso mbili, akisema mambo tofauti badala ya ukweli tu.

“Kutokunywa mvinyo nyingi sana” na “si mwenye pupa ya faida chafu” humaanisha kutojihusisha na ulevi au kutamani kama inavyojadiliwa kuhusu wazee. “Kushika siri ya imani katika dhamiri safi” ni kuunganisha maisha mema na safi pamoja na mafundisho ya Injili ambayo humwezesha mtu kuwa na dhamiri safi. Mashemasi pia lazima kwanza “wathibitishwe” na wawe “bila lawama” kama walivyokuwa wazee. Pia kama wazee lazima wawe waume wa mke mmoja” na “wanaotawala watoto wao na nyumba zao vema”. "Wake zao wawe wastaarabu, si wasingiziaji, watu wenye kiasi, waaminifu katika mambo yote." Hilo linaonyesha maana ya wanawake Wakristo waaminifu wazuri wakiwa wake wa wazee na mashemasi. Hawapaswi kuwa wasengenyaji bali wanapaswa kufanya sehemu yao kwa uangalifu na kwa uaminifu ili kuwatia moyo na kuwasaidia waume zao. Ikiwa kwa njia hizi mwanadamu ataonyesha kielelezo chake cha kiroho kwa kusanyiko, basi anastahili kuwa shemasi katika kanisa. Swali linaweza kuulizwa ikiwa mashemasi wanaweza kuteuliwa katika kusanyiko lisilokuwa na wazee. Jibu ni “hapana” kwa sababu hizi: (1) Hakuna mfano wa Biblia juu yake. Badala yake, siku zote wazee waliwekwa rasmi kwanza (Mdo. 14:23) na mashemasi daima hutajwa pamoja na wazee (Flp. 1:1; 3:1-13), isipokuwa Yerusalemu ambako inaonekana mitume walitumika wakiwa wazee. (2) Kwa kuwa mashemasi ni wasaidizi wa wazee, haiwezekani kuwa msaidizi wakati hakuna wazee wa kusaidia. (3) Mashemasi wakiwekwa kimakosa mahali ambapo hakuna wazee, watajaribu kutawala kanisa na kunyakua nafasi ya wazee. Kwa sababu hizo mashemasi wanaweza kutumikia mahali ambapo wazee wamewekwa rasmi. Lakini wazee wanaweza kutumika

mahali ambapo hakuna mashemasi bado wana sifa za kustahili, kwani kazi yao haiko chini ya mashemasi (Matendo 14:23).

## SOMO LA 27

# NJIA AMBAZO HAZIFAI KUCHAGUA VIONGOZI

## MUHTASARI

1. *Mshirika wa kwanza.*
2. *Mshirika tajiri zaidi.*
3. *Anayeigiza kuwa mzee.*
4. *Anayefanya siasa.*
5. *Anayependelewa na mhubiri.*
6. *Njia yoyote isipokuwa kielelezo.*

### MJADALA

***1. Mshirika wa kwanza.*** Ili kuona wazi jinsi maofisa wanavyopaswa kuchaguliwa, ni vyema kwanza kuona baadhi ya njia ambazo hazifai kuchaguliwa. Hizi ni mbinu za wanadamu na sio za Mungu. Ni mabadiliko na uharibifu wa mpango wa Mungu. Njia moja kama hiyo ni kuteua mshirika wa kwanza, wakati fulani huitwa "mshirika wa katiba", wa kanisa. Mwanamume aliyemleta mhubiri kijijini mara nyingi hujiona kuwa muhimu vya kutosha kuwa mzee. Lakini hatujasoma kamwe kuhusu “washirika wa mkataba” katika Biblia. Kuwa mshirika wa kwanza wa kusanyiko hakumfanyi mtu kuwa mashuhuri. Kubarikiwa kimaandalizi kutengana mwanzoni mwa kanisa hakufanyi mtu kuwa mzee au shemasi.

***2. Mshrika tajiri zaidi.*** Mara nyingi mshirika mwenye pesa au mali zaidi huchaguliwa kuwa mzee. Huenda kusanyiko likahisi kwamba

kumheshimu kutamfanya atoe mchango zaidi. Huenda pia wakamwogopa kwa sababu ya uwezo wake wa kiuchumi. Lakini Biblia inaonya dhidi ya utajiri (I Tim. 6:17). Mzee hawezi kuwa mchoyo au mchoyo wa faida chafu (I Tim. 3:3). Mtui hatakiwi kutafuta kazi ya mzee kwa ajili ya faida chafu (I Pet. 5:2). Kuwa kiongozi wa ulimwengu hakumfanyi mtu kuwa kiongozi wa kiroho, na mara nyingi huzuia. Kuwa na mali ya dunia haimaanishi kwamba mwanadamu ni tajiri kwa Mungu (Luka 12:21). Wengi ni matajiri wa mali lakini ni wanyonge, wenye huzuni, maskini, vipofu, na wa uchi kiroho (Ufu. 3:17). Utajiri wa kimwili haumstahilishi mtu kuwa mzee au shemasi.

***3.*** ‘***Kuigiza’ uzee.*** Wanaume wengi hujiita “makaimu wazee.” Hii ina maana kwamba wanafanya kama wazee wakati sivyo. Huenda mtu akajiita mzee kwa muda mrefu na hivyo akahisi kwamba anapaswa kuwekwa rasmi pindi wanapochaguliwa wazee. Lakini “wazee wa kujifanya” hupotosha na kuharibu mpango wa Mungu. Mapenzi ya Mungu ni kwamba viongozi wachaguliwe kwa sababu ya sifa zao wanazostahili, lakini “wazee waigizaji” hujaribu kupata baraka na heshima za mzee bila kutimiza matakwa. Ni kama kujifanya Mkristo bila kutii amri zinazomfanya mtu kuwa Mkristo. Ikiwa mtu angeanza kujiita “kaimu Mkristo” ingawa sivyo, kanisa lingefanya nini? Wangemkataa kama mdanganyifu. Vivyo hivyo lazima " makaimu wazee" wakataliwe. Kuteua "wazee waigizaji" ni kuongeza katika Neno la Mungu (Ufu. 22:18). Ni kupotosha Injili ya Kristo (Gal. 1:7-8). Ni mpango wa uongo kuchukua nafasi ya mpango wa Mungu wa kuwateua wazee na mashemasi.

***4.*** ***Siasa.*** Wakati mwingine siasa huingia katika uteuzi wa viongozi wa kanisa. Washirika wanajaribiwa kuchanganya mbinu za kisiasa na mbinu za kimaandiko. Wanaweza kufanya kampeni na kuvinjari kama vile walikuwa wakitafuta kura. Baadhi ya makanisa yanaweza hata kuwapigia kura viongozi wao. Rushwa inaweza kutolewa au vitisho vinaweza kutumika. Lakini kanisa si mahali pa kuchukua hatua za kisiasa. Mbinu zinazotumika katika kuchagua viongozi wa serikali ni tofauti kabisa na zile za kuchagua viongozi wa kiroho. Mwanamume anayestahili kuwa mzee hahitaji kujaribu kuthibitisha kwa wengine sifa zake za kustahili. Hana haja ya kutoa

hotuba na kujisifu. Kanisa tayari linajua maisha yake na kujua kama ana sifa. Zaidi ya hayo, yeye hashindani na wanaume wengine. Wanaume wote waliofudhu wanapaswa kuteuliwa, na hakuna anayeshindwa kwa sababu mwingine amechaguliwa. Wazee hawachaguliwi kwa kupigiwa kura bali kwa miadi. Kufanya siasa sio mpango wa Mungu wa kuwaweka wazee na mashemasi.

***5. Anayependelewa na mhubiri.*** Mhubiri anayefanya kazi na kanisa akichagua wazee anaweza kujaribiwa sana kuchagua mtu anayempenda zaidi kwa ajili ya kuteuliwa. Mtu huyu anaweza kuwa mtu ambaye amempa mhubiri neema nyingi. Mhubiri anaweza kuhisi kwamba anapaswa kumzawadia au kumlipa mtu huyo kwa wema wake kwake. Au mwinjilisti anaweza kutaka kumchagua mtu ambaye atakuwa “katika kundi” lake ili kuliendesha kanisa jinsi anavyotaka liendeshwe. Anaweza kukubali kumweka mzee ikiwa mzee huyo atafanya kama mhubiri anavyotaka wakati ujao. Kwa njia hizi na nyingine nyingi mwinjilisti anaeza kushawishiwa. Lakini kwa kufanya hivyo anajitenga na njia ya Mungu ya kutopendelea (Matendo 10:34). Mhubiri anakuwa mtazamaji wa watu. Ana hatia ya kuonyesha upendeleo. Kuwa kipenzi cha mwinjilisti hakupaswi kustahili mtu kuwa kiongozi katika kanisa.

***6. Njia yoyote isopkuwa kielelzo.*** Bila shaka, somo hili haliwezi kutaja njia zote zisizo za unyoofu na zisizo sahihi za kuchagua wazee. Lakini naweza kusema kwamba njia nyingine yoyote isipokuwa mpango wa Mungu wa mfano ni mpango wa uwongo. Mchakato wowote wa kuwateua wanaume kuwa viongozi ambao hawategemei kabisa sifa si za kimaandiko na si sahihi. Mawazo yoyote yanayoingia katika hilo si suala la tabia ya Kikristo ya mtu na uwezo wake ni msingi wa uwongo wa uteuzi. Mungu huweka viongozi kwa mfano: mipango ya wanadamu isijaribu kubadilisha hili.

## SOMO LA 28

# JINSI ROHO MTAKATIFU ANAVYOWEKA WAZEE

MUHTASARI

1. *Mafundisho sahihi.*
2. *Tamaa sahihi.*
3. *Uthibitisho sahihi.*
4. *Kutafuta wanaume.*
5. *Kuchagua au kuteua.*
6. *Kutambuliwa na kanisa.*

### MJADALA

***1. Mafundisho sahihi.*** Ukristo ni dini iliyofundishwa (Yohana 6:45). Waumini wanafundishwa kabla ya ubatizo na kufundishwa baada ya ubatizo (Mt. 28:19, 20). Kustahili na kuchaguliwa kwa wazee kunahitaji mafundisho marefu na makini. Roho Mtakatifu huwafanya wanaume kuwa waangalizi (Matendo 20:28). Njia ambayo Roho Mtakatifu hutumia kuwaweka wazee ni Biblia ambayo ni upanga wa Roho (Efe. 6:17). Roho Mtakatifu aliyavuvia Maandiko ambayo hutoa mafundisho ambayo huwafanya wanaume kuwa wazee katika kanisa. Lakini njia hii inaweza kuwa na matokeo ikiwa tu Biblia itafundishwa kwa usahihi. Kwa hiyo, ni muhimu kwamba maagizo ya Mungu ambayo yatawafanya wanaume kuwa wazee yasomwe katika kila kusanyiko. Mafundisho ya Biblia kuhusu mpangilio wa kanisa lazima yaeleweke vizuri. Kila mshirika lazima ajue nafasi na kazi za viongozi. Madarasa mengi, masomo binafsi, na mahubiri lazima yafundishwe ili kulitayarisha kanisa kwa ajili ya uongozi ufaao. Bila ya mafundisho sahihi hakuwezi kuwa na mpangilio sahihi. Mafundisho ya Maandiko ni hatua ya mwanzo kuelekea katika serikali ya kimaandiko. Uelewa

mzuri ndio msingi wa mpangilio mzuri. Roho Mtakatifu anaanza kuwafanya wanaume kuwa wazee kwa mafundisho sahihi.

***2. Tamaa sahihi.*** Hatua ya pili ni jibu sahihi la wale wanaofundishwa. Ni Mungu ndiye atendaye kazi ndani ya Wakristo kutaka na kutenda kwa mapenzi yake mema (Flp. 2:13). Washirika wanapofundishwa mapenzi ya Mungu wanaitikia kwa kutamani kufanya mapenzi yake. Mwanzo wa orodha ya sifa za mzee unasema, ***"Ikiwa mtu anatamani kazi ya askofu, atamani kazi njema"*** (I Tim. 3:1). Mwanadamu anapojifunza tabia za Mkristo aliyekomaa anajitahidi kuzifikia. Anasitawisha tamaa kubwa ya kuwa Mkristo mwenye nguvu, anayeweza kuwasaidia wengine wamfuate Kristo. Kwa njia hii Roho Mtakatifu anazaa matunda ya tabia ya Kikristo (Gal. 5:22, 23). Lakini si Roho Mtakatifu pekee anayeweka shauku ya kuwa mzee katika mtu. Shetani pia huwapa watu tamaa, lakini kwa nia tofauti. Ibilisi huunda tamaa ya umaarufu na utukufu usio na maana au hata pesa kama baadhi ya wanaume wanavyofikiria kuwa wazee. Kwa hiyo, si kila tamaa ya kuwa mzee ni tamaa ifaayo. Lakini ikiwa wanaume wanatafuta ofisi kwa sababu ya nia kama ya Kristo, kwa sababu wanataka tunda la Roho, basi Roho Mtakatifu atawaongoza kuelekea kuwa wazee. Tamaa hiyo inayofaa ni hatua muhimu kuelekea kuwa mzee.

***3. Uthibitishoa sahihi.*** Viongozi wa kanisa lazima kwanza wathibitishwe (1 Tim. 3:10). Hii ndiyo njia ya tatu ambayo Roho Mtakatifu hutumia ili kuwaweka wazee. Uelewa mzuri wa mtu na tamaa yake ifaayo humpelekea kujikuza na kuwa Mkristo aliyekomaa kikamilifu. Ukuaji wake na uwezo wake huja kuonekana na washirika wengine. Mtu anapozingatia maisha yake na mafundisho yake, maendeleo yake yanaonekana kwa wote (1 Tim. 4:15). Inachukua muda. Ukomavu wa kiroho hauji haraka. Miaka ya masomo, maombi, na ukuaji ni muhimu. Uzoefu mwingi unahitajika ili mtu astahili kuwa kiongozi na mwalimu wa Kikristo. Katika miaka hii mwanadamu anajithibitisha mwenyewe, yaani, anakuza tabia za Kikristo ambazo watu wote wanaweza kuziona. Matokeo yake, washirika wengine wanakuja kujua sifa zake kama kielelezo cha Kikristo na kiongozi. Sifa za kustahili za mzee zinapatikana na kuonekana hatua kwa hatua. Huu

ndio uthibitisho ufaao wa mwanamume anayestahili kuwa mzee. Kama ilivyoelezwa hapo awali, kuhusu mchakato huu

***4. Kutafuta wanaume.*** Mitume huko Yerusalemu waliamuru kwamba kusanyiko litafute idadi ya wanaume saba kabla ya kuwasimika kuwa mashemasi (Matendo 6:3). Hii ni hatua ya nne ambayo Roho Mtakatifu hutumia kuweka wazee. Wanaume wanaostahili wanapaswa kuchaguliwa kutoka kusanyikoni ili wafikiriwe kwa kuzingatia uwezekano wa kusimikwa. Ona kwamba hatua hii ni ya kusanyiko kuchukua. Kanisa zima, baada ya mafundisho sahihi, linapaswa kutafuta kutoka kwa washirika wake watu waliokomaa ambao wanakidhi mahitaji ya kuwa maaskofu. Kwa njia hii washirika wenyewe, badala ya mtu kuwa juu yao, huchagua viongozi wao wenyewe (Matendo 6:5). Wanachagua wanaume ambao wameona kuwa wamethibitika katikati yao. Wanachagua wale ambao wanafurahi kuwafuata. Wanawataja wale ambao watafurahia kuwaiga ili wawe kama Kristo. Hii ni hatua muhimu sana. Roho Mtakatifu anaongoza mchakato huu kupitia Maandiko katika mioyo ya washirika. Chaguo lao ni kulingana na maneno yaliyoongozwa na Roho wa Mungu. Wanafuata hekima ya Mungu inayopatikana katika Neno la Mungu (Kol. 1:9). Wanaomba kwamba Mungu awape hekima yake (Yakobo 1:5). Kwa maombi wanamwomba Mungu awaongoze katika chaguo lao kwa maongozi yake (Matendo 1:24). Hakuna muujiza unaofanywa ili kuonyesha chaguzi, lakini Roho Mtakatifu hata hivyo ndiye anayepaswa kuwa kiongozi kupitia Neno la Mungu. Kisha majina ya wanaume ambao wametajwa yanasomwa na kurekodiwa mbele ya kusanyiko. Kanisa zima linaona na kujua orodha ya wale ambao ni wahitaji wa nafasi hiyo. Hii ndiyo maana ya kutafuta wanaume.

***5. Kuchagua au kuteua.*** Biblia inasema kwamba wazee wanapaswa "kuwekwa rasmi" (Tito 1:5; Matendo 14:23). Toleo Lililorekebishwa linasema "aliyeteuliwa." Maneno haya yanamaanisha kutaja au kutambulisha. Maana ya kuwekwa wakfu imepotoshwa na makanisa mengi ya kimadhehebu. Pamoja nao inamaanisha kumpa mtu leseni ya kushikilia cheo katika "makasisi." Lakini Biblia haitaji kamwe "makasisi" wala "leseni ya makasisi". Kusimika katika kusanyiko la Agano Jipya ilikuwa ni kuashiria kwa maofisa ambao watu wenyewe

walikuwa wamewachagua. Ilifanyika na mwinjilisti (Tito 1:5), kwa kuwa alikuwa msemaji wa kusanyiko kabla wazee hawajawekwa rasmi. Lakini chaguo halikuwa chaguo la mhubiri. Uchaguzi haukufanywa na yeye. Hii sio maana ya kuamrisha. Mwinjilisti anaeleza tu chaguo ambalo tayari limefanywa na kanisa zima katika kuangalia na kuwaidhinisha viongozi wao. Baada ya kuwatazama wanaume wanaostahili, kusanyiko limejiruhusu wakati wa kuwaidhinisha au kuwakataa wanaotaka kuchaguliwa. Hakuna njia mahususi kwa hili isipokuwa kwa kila mshirika kuzingatia na kufikiria upya kila atamaniye ofisi hiyo kulingana na sifa za Biblia na kisha kuonyesha idhini au kutoidhinishwa. Kuidhinishwa kwa watahiniwa wanaozingatiwa kunaweza kuchukua wiki kadhaa ili kukamilika. Lakini viongozi hao wakishaidhinishwa hatimaye, uteuzi wao unafanywa ili kujulikana hadharani mbele ya kanisa na mwinjilisti au msemaji mwingine. Hii inajulikana kama maafisa wa kuteuliwa au wanaowekwa rasmi.

***6. Kutambuliwa na kanisa.*** Baada ya wazee kuzingatiwa, kuidhinishwa, na kuteuliwa na kusanyiko, kunabaki tu utambuzi wa kanisa kwa viongozi hao wapya. Mashemasi wa kwanza “waliwekwa” mbele ya mitume waliosali na kuweka mikono juu yao. Mitume katika siku za miujiza walitoa nguvu za kimiujiza za Roho kwa kuwawekea mikono (Matendo 8:18). Lakini kwa kuwa hakuna mitume na hakuna miujiza leo, kuwekewa mikono hakutumikii kusudi hili. Lakini kanisa la Antiokia liliweka mikono yao juu ya Barnaba na Sauli ili kuonyesha kibali chao kwao na kuahidi ushirikiano wao (Matendo 13:1-3). Kuwekea mikono kunaweza kutimiza kusudi hili kwa siku za leo. Ni ili (ingawa si muhimu) kuwatambua viongozi hao wapya kwa namna hii na hivyo kuonyesha kibali na utii wa kanisa. Kwa namna fulani kanisa linapaswa kuwatambua wazee wake wapya hadharani, kuwaombea, na kuwaahidi kuwa na imani na utii kwao. Huduma hii inapaswa kuwa rahisi na yenye maana. Haipaswi kuharibiwa kwa sherehe hususani sherehe isiyo na heshima. Hakuna sababu ya zawadi au karamu. Inapaswa kuwa tu ni wakati ambapo kanisa linawatambua hadharani viongozi wake.

## SOMO LA 29

# MAAGIZO YA MUNGU KWA WAZEE

## MUHTASARI

1. *Kuwa kielelezo kwa kundi.*
2. *Kulisha kundi.*
3. *Kuchunga kundi.*
4. *Kutazama kundi.*
5. *Kutawala vema.*
6. *Kukesha kwa ajili ya roho.*

### MJADALA

Baada ya kujifunza sifa za wazee, sasa tutajifunza kazi zao. Hili litaonekana katika agizo walilopewa na Mungu ambalo linaonesha majukumu yao. Kwa kujua kile ambacho wazee wanapaswa kufanya, basi tutaweza kuona vizuri jinsi ambavyo wazee wanapaswa kuwa.

***1. Kuwa mifano kwa kundi.*** Ingawa masomo haya tayari yameonyesha kwamba wazee lazima wawe mifano, ukweli huu mkuu lazima usisitizwe tena. Hakuna kitu muhimu zaidi katika kazi ya mzee kuliko mfano wake. Sifa zote zinatokana na msingi huu. Hii ndio sababu wazee wanaagizwa katika 1 Pet. 5:3. ***"Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi."*** Wafalme wanaweza kulazimisha mapenzi yao juu ya raia wao, lakini aina hii ya utawala haitimizi kusudi la Mungu kwa Wakristo. Mpango wa Mungu wa kuongoza na kufuata ni mpango mkuu na wa juu zaidi. Sio suala la nguvu bali upendo. Haitegemei nguvu za kimwili bali nguvu ya mfano. Aina ya uongozi wa Mungu ni kwamba wafuasi kwa hiari watake kumuiga viongozi wao. Hivyo ni lazima wazee wajitunze wao wenyewe kwanza kisha walitunze kundi (Matendo 20:28). Ni lazima waonyeshe kwa kanisa mfano ufaao ambao

washiriki watafurahia kuufuata. Wazee wasiwe mabwana juu ya kanisa bali wawe vielelezo kwa kundi.

***2. Lisha kundi.*** Jukumu la pili kwa wazee ni “kulilisha kundi la Mungu lililo kati yenu” (I Pet. 5:2). Sehemu kubwa ya wajibu wa wazee ni kulisha au kufundisha kanisa. Neno la Mungu ni chakula cha Wakristo. Kitawajenga kiroho (Matendo 20:32). Vijana walioongoka wanahitaji maziwa ili wakue (I Pet. 2:2). Wengine wanahitaji chakula kigumu kutoka katika Neno la haki (Ebr. 5:12-14). Ni lazima wazee waweze kuandaa chakula kwa ajili ya watoto na Wakristo wakomavu. Watafundisha Maandiko wenyewe, kwani lazima “wawe na ujuzi wa kufundisha” (I Tim. 3:2). Lakini pia watasimamia mafundisho ya walimu wengine kwa kuwatia moyo na kuwapa msaada wa kufundishia. Ni jukumu zito kuwa na jukumu la kutoa chakula cha kiroho kwa kanisa, zito zaidi kuliko kutoa chakula cha kimwili kwa familia. Hili likifanywa vyema kanisa litakua kiroho, lakini wazee wakishindwa, kanisa litadhoofika na kufa. Ibada inayofaa ya kiroho pia ni chakula cha nafsi ya Mkristo. Wakati wazee hawatoi huduma za ibada zenye lishe na zenye virutubisho, washirika wataugua na kulala kiroho (1 Kor. 11:30). Kwa hiyo, Mungu anawaagiza wazee walilishe kundi la Mungu kwa kuandaa chakula cha kiroho kilichotayarishwa vizuri kwa ajili ya nafsi zao.

***3. Kuchunga kundi.*** Mbali na kulisha kundi, wazee wanapewa jukumu la kulichunga. Wanapaswa "kuchunga" kundi kama wachungaji juu yake (Matendo 20:28). Neno la Kigiriki hapa linalotafsiriwa “lisha kundi” kwa kweli humaanisha “kutenda kama mchungaji katika kundi.” Kuchunga kundi kunamaanisha kuchunga. Katika Biblia tunaambiwa wachungaji waliishi na kondoo zao. Walijua udhaifu wa kila mmoja na walimpenda kila mnyama. Usiku mchungaji alilinda kundi, na wakati wa mchana aliwaongoza katika njia zinazofaa. Ikiwa mmoja angepotea, alimtafuta. Mmoja akiugua au kuumia, alimpaka mafuta katika vidonda vyake na kumuuguza hadi afya yake itengemae. Mchungaji daima aliwaongoza kondoo wake; hakuwahi kuwafukuza. Siku zote alikuwa mbele akiwaita na kuwaonyesha njia. Kondoo waliijua sauti yake na kumfuata kwa furaha kwa sababu walijua anawapenda na kuwapa kilicho bora zaidi. Katika njia hizo ni lazima wazee walichunge kundi la

Mungu kiroho. Ni lazima wajue na kumpenda kila mshirika. Ni lazima walinde, waongoze, na kutunza kundi. Ni lazima wawatafute wanaotangatanga na kuwajali walio dhaifu. Wazee daima watakuwa nje mbele ya kanisa kuonyesha njia, badala ya nyuma yake kuliendesha. Wataongoza kwa mbele ili kusanyiko liwafuata kwa shangwe, likijua kwamba ni kwa manufaa yao wenyewe kufanya hivyo. Kwa kusoma Zaburi 23 tunajifunza jinsi Mungu anavyochunga kondoo Wake na jinsi anavyomaanisha kwa upole na uangalifu, wazee pia wanapaswa kulilisha na kutegemeza kundi lao. Wazee wana madaraka ya kulichunga kundi la Mungu.

***4. Kuangalia kundi.*** 1 Pet. 5:2 inawaambia wazee, ***"Lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo."*** Wazee hapa wana wajibu wa kuchukua uangalizi na kusimamia kwa kusudi linalofaa na kwa roho ifaayo. Majina askofu" na "mwangalizi" yanaonyesha kwamba wazee wanapaswa kulisimamia kanisa. Wanaangalia ustawi wa kanisa. Wanasimamia shughuli zake. Kusimamia ni "kuona juu" au kuangalia hitaji la kiroho la kanisa. Roho Mtakatifu huwafanya wazee kuwa "waangalizi juu ya" kanisa (Matendo 20:28). Uangalizi haupaswi kuwa na kikwazo, lakini kwa hiari. Hiyo ni, wazee wanapaswa kuchagua kuwa waangalizi, badala ya kulazimishwa kinyume na mapenzi yao. Na uangalizi wao utakuwa ni aina ambayo haiwashurutishi wala kuwalazimisha wafuasi, bali kuwaongoza kufuata kwa kupenda. Ni lazima nia za wazee zisiwe kwa ajili ya pesa au kwa ajili ya umashuhuri, bali ni utayari wa akili kumtii Mungu. Mwangalizi wa kikundi chochote ana wajibu mzito zaidi. Lakini waangalizi wa makusanyiko ndio wenye majukumu mazito zaidi. Mchungaji Mkuu atawawajibisha kwa ajili ya ustawi na kazi ya kundi. Ni lazima watimize wajibu wao kwa uangalifu mkubwa na lazima wafanye hivyo kwa kasi ifaayo pamoja na nia ifaayo. Huku ndio kuchukua uangalizi wa kanisa.

***5. Kutawala vyema.*** Ni wajibu wa wazee pia kutawala kusanyiko vizuri (I Tim. 5:17). Kifungu hiki kinafafanua zaidi wale wanaotawala ***"kwa kuhutubu na kufundisha."*** Katika kutaja sifa za mzee Biblia inasema, ***"Kwa maana ikiwa mtu hajui kuisimamia nyumba yake***

***mwenyewe, atalitunzaje kanisa la Mungu"*** (I Tim. 3:5). Kwa hiyo, inaonekana kwamba kwa kutawala kusanyiko kunamaanisha kujitahidi kufundisha na kulitunza kusanyiko kama vile baba anavyoitunza familia yake. Kutawala haimaanishi kujitawala mwenyewe katika kanisa (I Pet. 5:3). Inamaanisha kuwajibika kwa ajili ya ustawi wa kanisa na kutawala mambo ya kiroho ya washirika. Wanaume wengine wana mawazo potofu ya utawala. Wanafikiri kwamba mtawala lazima atende kama mfalme anavyowatendea watumwa ambao ni raia wake. Hii si kweli kwa wazee wanaotawala kanisa. Biblia inasema watawale, ikimaanisha kwamba hawapaswi kuwa wazembe kuhusu shughuli za kanisa. Wanapaswa kuwa wasimamizi na wasipuuze mambo muhimu wanayoyasimamia. Wana jukumu zito. Wale wanaotimiza agizo hili vizuri wanastahili ***"heshima maradufu"*** kwa sababu wajibu ni mzito sana (1 Tim. 5:17). Wazee wameagizwa kutawala vema au kutawala kanisa la Bwana kwa namna hii.

***6. Kukesha kwa niaba ya roho***. Wazee wanapaswa kutiiwa na kunyenyekewa kama wale ***"kwa maana wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha, wala si kwa huzuni;"*** (Ebr. 13:1). Shitaka kubwa kuliko yote ni kwamba wazee wanapaswa kuangalia na kutoa hesabu kwa ajili ya roho za washirika. Wao ni kama walinzi kwenye kuta za Israeli ambao walipaswa kubeba damu ya watu mikononi mwao ikiwa hawakuwa macho na kuonya kuhusu adui (Eze. 3:17-21). Ni nini kinachoweza kuwa cha kutia moyo zaidi kuliko kutoa hesabu ya nafsi zilizoachwa katika malipo ya mtu? Si lazima tu mzee akeshe, lakini lazima atoe hesabu kwa ajili ya roho za washirika katika jukumu lake. Aina hii ya kukesha inahitaji bidii ya kudumu (I Pet. 5:8). Inadai uangalizi usiokoma juu ya kila kiungo hata kwa machozi (Matendo 20:31). Mzee anaagizwa kukesha kwa niaba ya roho na kutoa hesabu kwa Mungu.

**SOMO LA 30**

# DALILI ZA HATARI KATIKA MUUNDO WA KANISA

## MUHTASARI

1. *Taasisi yoyote iliyo juu ya makanisa.*
2. *Taasisi yoyote miongoni mwa makanisa.*
3. *Viongozi wa nje ndani ya makanisa.*
4. *Maagizo yoyote kutoka katika makanisa yanayojitegemea.*

## MJADALA

***1. Shirika lolote juu ya makanisa***. Kuna ishara fulani au dalili zinazoonyesha wakati shirika la kanisa linapopotoshwa. Hizi zinaweza kuitwa ishara za hatari, na zinaonyesha kwamba mpango wa Mungu unabadilishwa. Ishara moja ya hatari ni shirika lolote kuwa juu ya makanisa. Aina hii ya shirika inaweza kuonekana katika madhehebu mengi. Kuna shirika kubwa zaidi kuliko makusanyiko ya ndani. Ni mamlaka kuu yenye maafisa wa makanisa mengi. Baraza hili kubwa hufanya maamuzi kwa ajili ya makusanyiko. Linachagua mhubiri wao, linaelekeza shughuli za kufanywa, na linahitaji kodi. Makanisa ya Kristo yanaelezwa kuwa Kristo hafanyi shirika kama hilo. Lakini badiliko hilohilo katika nyakati fulani za matengenezo hutokea miongoni mwa watu wa Mungu. Kwa mfano, washirika wengi wanataka vyuo vya mafunzo ya Biblia kuwa shirika la utumishi juu yao. Wanataka ndugu wazungu wachague na kumlipa mhubiri wao. Tatizo la kanisa linapotokea, wanataka ndugu wa Marekani wawaambie la kufanya. Lakini shule za Biblia hazina mamlaka juu ya makusanyiko. Wamishonari wa kizungu hawawezi kufanya maamuzi ya makanisa. Ni lazima kuwe na uhuru kamili katika kila kusanyiko. Hakuwezi kuwa na

mamlaka ya nje au shirika juu ya makanisa. Wakati shirika lolote linapopata mamlaka juu ya makanisa, ni ishara ya hatari na ufisadi.

***2. Shirika lolote kati ya makanisa.*** Kwa sababu washirika wengi wametoka katika madhehebu, wanatamani kujipanga kama walivyofanya hapo awali. Ili kufanya hivyo wanatumia njia kama vile "mikutano ya Injili" ili kuunganisha makanisa. Wanatuma wajumbe au kamati kutoka katika kila kusanyiko na kukutana katika mkutano mkuu. Wanaweza kuchagua maafisa, kama vile mwenyekiti, katibu, au mweka hazina. Wanaweza kutathmini pesa kutoka kwa kila kanisa na kuwa na hazina. Wanaweza kujiita "Mkutano wa Injili wa Ngwa wa Mashariki," unaoonyesha kundi katika wilaya kama sinodi na wilaya za madhehebu. Kuna tofauti ya cheo kati ya mashirika haya na wilaya za kimadhehebu ya aina ya watu wa kujitolea. Na ingawa mikutano ya Injili inaweza kufanya matendo mema, ndivyo na vikundi vya madhehebu. Hii haiwafanyi kuwa wa kimaandiko. Hakukuwa na mikutano ya Injili iliyopangwa katika Biblia. Hayo ni machipukizi kutoka katika asili ya madhehebu. Washirika wengi wametoka katika madhehebu, lakini umadhehebu haujatoka kwao. Ingawa mabadiliko yanaweza kuwa madogo mwanzoni, lakini ni ya aina ambayo husababisha anguko zaidi. Mikutano ya Injili inaweza kubadilishwa na mihadhara katika makanisa binafsi. Matokeo yake, mambo yote mazuri ya mikutano ya awali yanaweza kuwekwa, huku mazoea hatari na ya dhambi yakipuuzwa. Ndugu watakuwa bado na ushirika mzuri wa Kikristo na mafundisho na watalitia moyo kanisa mahali ambapo mikutano inafanyika. Lakini wataweka njia na maafisa, hazina, na kuweka vikundi katika wilaya. Watafanya mikutano ya kufanya maamuzi kwa ajili ya makanisa. Biblia inatuamuru tuhakikishe mambo yote, tushike sana lililo jema, na kujiepusha na kila namna ya uovu (1 Thes. 5:21, 22). Mikutano ya Injili inapothibitishwa au kuchunguzwa, na kukuta dosari, itakataliwa ili uovu wao uepukwe. Lakini mazuri yanaweza kutolewa tena katika mihadhara ya makusanyiko na yanaweza kufanywa haraka na wale wanaoshiriki. Shirika lolote kati ya makanisa ni ishara mbaya na ya dhambi ya kuondoka kutoka katika Neno la Mungu.

***3. Viongozi wa nje makanisani***. Ishara nyingine ya hatari katika shirika la kanisa ni kuwa na maafisa wa nje makanisani. Maafisa hawa

wanaweza kuwa wa aina iliyotajwa katika mashirika juu ya makanisa (hapo juu). Au wanaweza kuwa viongozi au washirika kutoka kusanyiko lingine. Ikiwa kanisa kubwa, lenye nguvu kuliko kusanyiko dogo la karibu na lililo dhaifu, lile kubwa linaweza kujaribu kutawala lile dogo. Kanisa kubwa linaweza kufikiri kwamba maofisa wake ni maafisa wa kuyazungukia makanisa machanga. Hii si kweli. 1 Pet. 5:2 inawaagiza wazee "wachunge kundi lililo kati yao". Wazee katika kanisa hawatakiwi kuchunga mambo ya kusanyiko lingine isipokuwa lile lililo miongoni mwao, Matendo 20:28 inawafundisha wazee kulichunga kundi ambalo Roho Mtakatifu amewaweka kuwa waangalizi juu yake. Roho Mtakatifu alikuwa amewafanya kuwa waangalizi juu ya kusanyiko la Efeso pekee (Matendo 20:17). Hii haimaanishi kwamba wazee hawawezi kupendezwa na makanisa mengine au hawawezi kuwasaidia na kushirikiana nao. Kwa hakika wanaweza kuwa kiungo katika mwili mmoja wa Kristo pamoja nao (Efe. 4:16). Lakini wazee hawa husaidia na kutia moyo kama ndugu tu, si kama maofisa juu ya makanisa mengine. Utawala wao uko tu katika kusanyiko lao, na kila kanisa linaendesha mambo yake lenyewe. Kuwa na maafisa wa aina yoyote kutoka nje ya kusanyiko husika ni ishara ya hatari na upotovu wa mpango wa Mungu wa utawala wa kanisa.

***4. Mabadiliko yoyote kutoka kwa makanisa yanayojitegemea***. Mpango wa Mungu ni makanisa kujitegemea au kujitawala yenyewe. Kila kusanyiko liko huru chini ya Kristo. Limepangwa bila kanisa lingine au bila shirika lolote juu ya makanisa. Haliko chini ya maofisa wa kanisa lingine. Kila kanisa linafanya maamuzi yake lenyewe, linafanya kazi zake lenyewe, linapanga mambo yake lenyewe, linachagua viongozi wake lenyewe, linachanga fedha zake lenyewe, linaendesha ibada yake lenyewe, na kuwatia adabu washirika wake wenye kuasi. Huu ndio mpango wa Mungu. Hii ndiyo njia ya Biblia. Mbinu au mpangilio mwingine wowote ni ukiukaji wa mamlaka ya Mungu na upotovu wa kusudi la Mungu. Acheni tufanye mambo ya Mungu katika njia ya Mungu kwa kufanya mambo ya Biblia katika njia za Biblia. Njia ya Mungu na mpango wa Mungu ni bora zaidi.

## SOMO LA 31

# JINSI UTAWALA WA KANISA ULIVYOHARIBIWA MWANZONI

## MUHTASARI

1. *Utabiri wa Biblia kuhusu kuanguka.*
2. *Masomo kutoka katika historia ya kanisa.*
3. *Laana kwa  wachungaji wasio waaminifu.*

### MJADALA

***1. Utabiri wa Biblia kuhusu kuanguka.*** Somo letu la kwanza lilisema kwamba sababu moja ya muhimu kujifunza kuhusu mpangilio wa kanisa ni kwamba kuanguka kwa kwanza kulikuja katika utawala wa kanisa. Somo hili la sasa litaonyesha jinsi ufisadi huu ulivyokuja. Kwanza, tunaona utabiri wa Biblia kwamba kuanguka kungekuja. Mtume Paulo aliwaonya wazee wa Efeso kwamba mbwa-mwitu wakali wangeingia na kuliteka kundi. Hawa ni walimu wa uongo, ambao wangewavuta wafuasi nyuma yao (Matendo 20:29, 30). Huu ulikuwa ni unabii kwamba kanisa lingeharibiwa na walimu wa uongo. Ni muhimu kuwa Paulo alisema "miongoni mwenu" hawa walimu wa uongo wangetokea. Hii ilimaanisha kwamba uasi ungeanzia makanisani na kutoka kwa wazee au viongozi. 1 Tim. 4:1-4 ni onyo lingine kwamba wanadamu wangeacha imani. Tena walimu wa uwongo wanatajwa kama njia ambayo uasi ungetumia kuja. Katika 1 Kor. 1:10-13 tunaona kwamba migawanyiko ilikuwa tayari imeanza katika kanisa la Korintho. Migawanyiko hii ilikuwa imeletwa na washirika kufuata viongozi wao badala ya kumfuata Kristo pekee. Mgawanyiko na ufisadi viliunganishwa na uongozi wa kanisa. Onyo lingine ni 2 Thes. 2:3, 4, inayosema kwamba kuasi kungekuja na "mtu wa dhambi" ambaye angefunuliwa. Huyu angekuwa mtu ambaye angeketi hekaluni kama

mungu, akijionyesha kwamba yeye ni Mungu. Kuondoka huko kulisababishwa na viongozi wasiomcha Mungu, wengine kanisani na wengine nje. Maadamu uongozi wa kanisa uliendelea kuwa safi, kanisa halikuanguka. Lakini wazee na walimu walipoacha Neno la Mungu na kutoka katika mpango wa Mungu, upotovu ulikuja upesi. Biblia ilitabiri kuanguka huku kungehusisha uongozi. Tunaona matokeo ya kutisha katika migawanyiko na mafundisho ya uongo leo hii.

***2. Masomo kutoka katika historia ya kanisa.*** Biblia inamalizia kwa taswira ya makusanyiko saba katika Asia (Ufu. 1, 2, 3). Mengi ya makanisa haya yalikuwa yameasi kama vile unabii wa awali ulivyotabiri. Lakini tunapoendelea kujifunza kuhusu makanisa hata baada ya Biblia kufungwa, tunaona maonyo ya kuanguka yakitimizwa zaidi. Biblia inasema kwamba Shetani analipotosha kanisa kwa kuwageuza Wakristo kutoka kwenye ***"unyofu na usafi kwa Kristo''*** (2 Kor. 11:3). Hii hakika ilitokea katika shirika la kanisa la Bwana. Wanadamu hawakuridhika na mpango rahisi wa Mungu. Kwa sababu ya tamaa yao ya pesa na umashuhuri, waliongeza na kubadili mpango wa Biblia. Ifuatayo ni orodha ya masomo tunayoweza kujifunza kutoka katika historia ya kanisa tunapoona upotovu wa taratibu wa shirika la kanisa:

(1) Miongoni mwa walioanguka kwa mara ya kwanza kulikuwa ni utawala wa kanisa. Uongozi ulipoacha njia ya Mungu, makosa mengi yangeweza kuletwa kwa urahisi. (2) Nia ya wengi walioanguka ilikuwa nzuri. Hawakuwa na maana ya kwenda mbali. Walifikiri mabadiliko yao katika mpango wa utawala yangekuwa bora zaidi. Lakini walibadilisha njia ya Mungu kwa njia ya mwanadamu. (3) Mwanzo wa kuanguka ulikuwa mdogo sana. Hii ni kawaida. Wanadamu "hupeperuka" polepole kutoka katika mpango wa Mungu wakati mwingine bila kujua. (4) Mara tu safari zilipoanza, wengine walifuata. Ni kana kwamba lango limefunguliwa, na umati mkubwa wa watu unaingia ndani kwa kasi. (5) Ili kuhalalisha kuondoka, hoja zilitolewa kutokana na kuondoka mapema. Wanaume wangesema kwamba kwa sababu wengine walikuwa wamefanya jambo moja, basi wangefanya hata zaidi. (6) Hakuna mabadiliko makubwa yaliyofanywa haraka, lakini mabadiliko madogo yaliongezwa hatua kwa hatua. Watu

wanaweza kuona ufisadi mkubwa unaotokea mara moja. Lakini mabadiliko madogo yanapuuzwa, bila kutambuliwa kwa muda mrefu. (7) Watu hawakuridhika kuwa na mamlaka sawa kama wazee. Upesi walichagua "wazee wa mji," na baadaye wazee wakuu. (8) Wanadamu hawakuridhika kuwa na utawala katika kanisa moja tu. Upesi walikusanya kundi la makanisa mengine pamoja chini ya utawala wa wazee fulani. (9) Makanisa yenye nguvu yalitaka uangalizi juu ya makanisa mapya na dhaifu. (10) Wanaume wenye elimu walitaka kufanya maamuzi kwa ajili ya watu wa kawaida katika makanisa. (11) Viongozi walitaka umashuhuri kutoka kwa washirika wa kawaida, na ndivyo "makasisi" na "walei" wakaanza. Maneno haya ni maneno yasiyo ya kimaandiko. (12) Maandiko yalionwa kuwa magumu, na katekisimu ziliandikwa ili kuyafafanua. Hivi karibuni katekisimu hizi zilikuwa na mamlaka sawa na hata zaidi ya Biblia. (13) Mikutano ya wazee ilitumiwa kuamua kile ambacho mshirika anapaswa kuamini. Maamuzi na maoni yao yalifungwa kwa makanisa. (14) Serikali ya kanisa ilichanganyikana na serikali ya nchi. Kwa hiyo, kanisa liliacha nafasi yake ya kiroho na kuwa mamlaka ya kisiasa. Baadaye, ufisadi mwingi wa serikali uliongezeka katika kanisa. Hizi ni baadhi ya njia ambazo Shetani alizitumia kupotosha usahihi wa kanisa. Tunaweza kuona ndani yao unabii wa Biblia kuhusu kuanguka ulipotimia. Tunaendelea kuona magari haya ya kuanguka yakiwa yamepeperushwa mbali katika sura ya madhehebu ya leo.

***3. Laana kwa wachungaji wasio waaminifu.*** Ikiwa masomo yaliyotangulia yatakuwa ya thamani kwetu, viongozi wa makanisa leo lazima wachukue maonyo. Ni lazima wasifanye makosa yale yale ambayo viongozi hawa wa mwanzo walifanya. Sikiliza laana za Agano la Kale zilizotamkwa juu ya wachungaji wasio waaminifu wakati huo. Ni ole gani zaidi juu ya wachungaji wasio waaminifu leo, ***"Ole wao wachungaji wanaoharibu na kuwatawanya kondoo za malisho yangu! asema Bwana, …angalieni, nitawapatiliza uovu wa matendo yenu"*** (Yer. 23:1, 2). Viongozi wenye nguvu wanaweza kulizuia kanisa lisianguke tena. Viongozi dhaifu hawataweza. Mungu ameweka wajibu mzito juu ya wale wanaoongoza watu wake. Lakini pia ametoa baraka tukufu kwa wazee waaminifu. 1 Pet. 5:4 inawaahidi wale

wanaolisimamia kundi ipasavyo, ***“Mchungaji Mkuu atakapotokea, mtapokea taji ya utukufu isiyokauka.”*** Ni thawabu gani ya utukufu ambayo wazee wa kweli na wema watapokea kutoka kwa Mchungaji Mkuu na Askofu wa roho zetu (I Pet. 2:25). Itakuwa taji ya utukufu isiyofifia.

## SOMO LA 32

# NAMNA YA KUENDESHA KIKAO

## MJADALA

Somo la sasa linahitimisha somo hili la Serikali ya Kimaandiko ya Makanisa ya Kristo. Lakini kabla ya kufunga, baadhi ya mapendekezo ya vitendo kwa ajili ya mikutano ya kanisa yatatolewa. Mikutano kama hiyo inaweza kufanywa kwa njia kadhaa nzuri. Mapendekezo haya ni kanuni tu ambazo zinapaswa kukumbukwa katika utaratibu wowote unaotumiwa. (1) Mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu (1Kor 14:40). Hili linahitaji mipango mizuri. Maandalizi yanapaswa kufanywa mapema kwa mkutano unaokuja. Aya hii pia inahitaji utaratibu na mwenendo mzuri. Mtu mmoja anapaswa kuzungumza kwa wakati mmoja. Uungwana na heshima vinapaswa kutekelezwa. (2) Kila mtu na amtendee mwenzake kwa heshima, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake (Flp. 2:3). Hii inaepusha ugomvi, ukaidi, na vurugu. Kila mwanaume awe tayari kuacha maoni yake au upendeleo wake ili kuleta ushirikiano. (3) Mtu awaye yote asipende kuwa na ukuu (III Yohana 9). Kila mtu lazima atafute kuwa na tahadhari kwa ajili yake mwenyewe. Ondoa kiburi, ubinafsi na majivuno yote. Wote lazima wajivike unyenyekevu, kwa maana Mungu huwapinga wenye kiburi bali huwapa neema wanyenyekevu (I Pet. 5:5). (4) Kila mtu na atafute kuwatumikia wengine na kulitumikia kanisa. Yesu alisema kwamba aliye mkuu zaidi machoni pake ni mtumishi wa wote (Mt. 20:27) . Alionyesha hili kwetu

kwa kuosha miguu ya wanafunzi (Yohana 13:12-15). Kila mwanaume anapaswa kuingia kwenye mkutano wa kanisa akiwa na hamu ya kuwa mtumishi. Kila mmoja anapaswa kufanya huduma yoyote ambayo itasaidia kanisa.

(5) Fungua na ufunge kila mkutano kwa sala ya unyoofu. Katika nyakati muhimu kama hizo za uamuzi, hekima ya Mungu na maandalizi vinahitajika sana. Ameahidi kuwapa hekima wale wanaomwomba (Yakobo 1:5). Maombi yasiwe ni marudio yasiyo na maana. Ni lazima yawe maombi ya dhati na yenye ufanisi kwa Mungu kwa ajili ya msaada (Yakobo 5:16). (6) Acha kila mzee au kila mwanamume (ikiwa hakuna wazee) achukue zamu yake kama mwenyekiti. Hii inamzuia mtu mmoja kufikiria kuwa ni mwenyekiti wa kudumu. Inampa kila mmoja uzoefu unaohitajika katika kuongoza mijadala. Na huzuia ugomvi na husuda. Ni uzoefu mzuri na mafunzo kwa mwanamume kutumia busara na subira katika kuendesha kikao vizuri. Kazi hii si rahisi. Mwenyekiti, bila shaka, hana mamlaka zaidi katika maamuzi kuliko wengine. Ni kazi yake kuleta utulivu kwenye kikao. (7) Mtu anapaswa kuandika rekodi sahihi za kila kikao. Kazi hii pia inaweza kuchukuliwa kwa zamu. Mtu kama huyo hana mamlaka au umuhimu zaidi kuliko wengine. Anaandika tu kile ambacho mkutano unamwambia aandike. Yeye si kiongozi na hana ofisi. Mwishoni mwa kila kikao rekodi inapaswa kusomwa na kuidhinishwa na wote. Kisha mwanzoni mwa kikao kijacho inapaswa kusomwa tena.

Rekodi zote lazima zihifadhiwe kwa marejeleo ya siku zijazo ikiwa mtu atauliza uamuzi au hatua fulani. Rekodi ya kila kikao haipaswi kuwa ndefu na ya kuchosha. Kuwa na mpango mzuri wa kikao, na usiruhusu maneno yasiyo na msingi. Kurefusha kikao kwa muda mrefu wakati hakuna kitakachokamilika kutawachosha katika siku zijazo. (9) Sauti ya kila mtu na isikike katika majadiliano. Usiruhusu mtu mmoja au watu wachache kuchukua muda wote. Kila mwanaume aruhusiwe kujieleza kwa uhuru. (10) Kikao kinapaswa kujaribu kupanga mipango ya wakati ujao badala ya kusuluhisha kila mara matatizo ya zamani. Vikao lazima viwe vya kutia moyo badala ya kukatisha tamaa. Vikao vya wanaume vinapaswa kuunda bidii na shauku. Wafanye hivyo ikiwa itafanywa ipasavyo. Kusudi lao

linapaswa kuwa kusababisha kila mshirika "kuzidi sana katika kazi ya Bwana siku zote" (1 Kor. 15:58).

(11) Hakuna upigaji kura unaopaswa kufanywa. Badala yake, mjadala kamili unapaswa kuendelea hadi wote waweze kuja kwenye "nia moja na fikira moja" (1 Kor. 1:10). Ikiwa uamuzi wa mwisho hauwezi kufikiwa, ahirisha baadhi ya mambo hadi mkutano unaofuata ili kuruhusu ndugu kuja kwa nia moja (Matendo 4:32). Makubaliano yanaweza kufikiwa ikiwa ndugu wanataka "kuwa na nia moja, na wenye upendo mmoja (Flp. 2:2). Ugomvi kati ya ndugu huwafanya adui zetu wacheke (Zab. 80:6). Kwa sababu Wakristo ni ndugu, wanaweza kushinda tofauti zao na kutokuwa na ugomvi (Mwanzo 13:8). Wanaweza kutembea pamoja kwa makubaliano (Amosi 3:3). Nyumba iliyogawanyika yenyewe haiwezi kusimama (Mt. 12:25). Mungu anamchukia mtu apandaye mafarakano kati ya ndugu (Mit. 6:16, 19). Kati ya watu wote, ndugu Wakristo, ambao ni viungo vya mwili mmoja wa Kristo, wanaweza na kwa hakika wanapaswa kufanya kazi pamoja (1 Kor. 12:12, 25). (12) Jaribu kumpa kila mshirika kitu ambacho anaweza kufanya katika kazi ya Bwana. Ingawa kazi inaweza kuwa ndogo, lakini ni muhimu kwa mazoezi ya kiroho ya mshirika. (13) Jambo kuu mbele ya kila kikao linapaswa kuwa ujenzi wa nyumba ya kiroho ya Mungu, kanisa. Washirika hawapaswi kamwe kupendezwa zaidi na nyumba halisi (ujenzi wa kanisa) au jambo lingine lolote la kimwili. Kila uamuzi na kila tendo lazima liwe kwa ajili ya kulijenga kanisa kiroho. Mipango ya kimadhehebu inaweza kujenga nyumba ya kimwili, lakini mpango wa Mungu hujenga nyumba ya kiroho. Kisha nyumba ya kimwili hakika itajengwa mahali pake. (14) Kauli mbiu ya kila mkutano inapaswa kuwa kupanga kazi na kisha kufanya mpango. Kanisa ambalo linashindwa kujiandaa, linajitayarisha kushindwa.

## HITIMISHO

Hii inahitimisha mjadala kuhusu mpangilio wa kanisa. Mengi zaidi, bila shaka, yanaweza kufundishwa. Biblia imejaa na imekamilika kwa kila sehemu ya mpango wa Mungu kwa kanisa. Lakini inatumainiwa kwamba mafunzo haya yamemfanya kila msomaji kutaka kuendelea na kujifunza yote ambayo Biblia inafundisha kuhusu jambo

hilo muhimu. Inatarajiwa, pia, masomo haya yameleta kwa kila mmoja hamu ya kurejesha kabisa Ukristo wa Agano Jipya. Hili linaweza kufanywa ikiwa kila sehemu ya mpango wa Kristo itafuatwa na ikiwa Kristo kweli ni Bwana katika kila jambo. Kanisa la Bwana haliwezi kurejeshwa isipokuwa mpangilio wa kimaandiko umerejeshwa. Lakini kama serikali rahisi na uongozi wa kanisa la Agano Jipya utaondolewa tena leo hii basi itaenda mbali katika kuleta kanisa la kweli katika uhalisia wa siku hizi.

Kanisa ni kama jengo zuri lililojengwa kulingana na mpango mzuri au ramani. Yesu alijenga kanisa lake kama alivyoahidi (Mt. 16:18). Lakini walimu wa uwongo walilibomoa kanisa mahali pengi (Matendo 20:28-30). Sasa sisi leo lazima tuchukue tena mpango ule ule (Agano Jipya) na kufuata haswa kila sehemu na kwa hiyo turejeshe jengo lile lile la kiroho. Kurejesha mpango wa Bwana wa shirika safi la kanisa ni sehemu muhimu ya kurejesha jengo. Mpango wa Biblia ukifuatwa, Mungu ndiye mwandisi na mjenzi. Lakini ikiwa njia za wanadamu zitabadilisha, makanisa ya wanadamu yatatokea. Biblia inaonya hivi: ***"BWANA asipoijenga nyumba, waijengao wafanya kazi bure"*** (Zab. 127:1). Lakini kama mawe yaliyo hai na tujenge nyumba ya kiroho, tutoe dhabihu za roho, zinazokubalika kwa Mungu katika Kristo Yesu (1Pet. 2:5).